**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**SHULE YA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII**

**IDARA YA KISWAHILI**

# MCHANGO WA FASIHI SIMULIZI KATIKA FASIHI ANDISHI:

# MFANO WA VISASILI KATIKA *MAFUTA (1984)* NA *WALENISI (1995)*

**NA:**

**MILKAH KERUBO OKEMWA**

**TASNIFU YA UTAFITI ILIYOWASILISHWA**

**KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**SEPTEMBA, 2017**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote

Sahihi: ___________________________________ Tarehe: ________________________

Milkah Kerubo Okemwa

C50/CE/26956/2011

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioidhinishwa na chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahihi___________________________________ Tarehe:________________________

Dkt. Gakuo J. Kariuki

Idara ya Kiswahili.

Sahihi___________________________________ Tarehe:____________________________

Dkt. Richard M. Wafula

Idara ya Kiswahili

## TABARUKU

Kwa mama yangu Rudia Nyakerario na dada yangu Rael Nyaboke walionitia uchu wa kupenda elimu. Kwa mume wangu mpenzi Richard na watoto wangu Josiah, Fridah, Irene na Kevin, mlinitia ari na moyo wa kuendelea na masomo yangu.

**SHUKRANI**

Nashukuru mwenyezi Mungu kwa kunipa neema, afya na uwezo wa kuandika kazi hii hadi tamati. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu wa kazi hii, Dkt. E. Masinde na Dkt Gakuo J. Kariuki waliochukua muda wao kuniongoza kwa busara, ukakamavu na kujitolea. Ushauri wao uliniwezesha kudhibiti kazi hii.

Shukrani za dhati ziwaendee wahadhiri wangu Dkt Wafula, Dkt Mwihaki, Dkt Ngugi, Dkt Chacha, Bi Mdhume pamoja na wengine wa idara ya Kiswahili wa chuo kikuu cha Kenyatta. Walinitia moyo na hamasa nilipokua nikitafiti

Natoa shukrani zangu kwa dada zangu Esther, Nyaboke, Teresa na Wilkister kwa ushauri wenu wakati nilipokua nikitafiti. Nashukuru walimu wenzangu Zipporah, Kamalei, Nyaberi pamoja na Bwana Malungu kwa ushauri wenu wakati nilipokuwa nikitafiti.

Namshukuru mwalimu mkuu wa shule ya Sinyereri pamoja na naibu wake kwa ushauri waliotoa wakati nilipokuwa ninatafiti.

Nampa heko mume wangu kwa kunivumilia nilipokuwa nikishughulikia kazi hii. Sitasahau watoto wangu Fridah, Josiah, Irene na Kevin waliovumilia kutokuweko kwangu na shauku ya kutaka kuona hatima ya kazi hii.

Kadhalika, kongole zangu ziwaendee wanafunzi wenzangu Musila, Kamanjo, Sereti, Monicah, Makandi na wengine kwa kunitia shime wakati bahari ilipochafuka na barabara kuwa telezi. Walinihimiza wakati nilipohisi kulemewa. Mbali na hawa natoa shukrani zangu kwa wanafunzi wengine wote ambao tulishiriki nao katika masomo ya shahada hii ya uzamili.

Mwisho, natoa shukrani zangu kwa Bi Makori, Bwana Tom na mtoto wangu Kevin kwa kujitolea kuipiga chapa tasnifu hii dhidi ya vikwazo mbalimbali.

Shukrani pia ziwaendee wengine wote ambao walichangia kwa namna moja au nyingine katika ufanisi wa tasnifu hii.

# IKISIRI

Utafiti huu ulitathmini mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi. Utafiti ulilenga kubainisha umuhimu wa visasili katika utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Malengo ya utafiti yalikuwa ni kuonyesha ubainikaji wa visasili, mchango na umuhimu wake katika utunzi wa riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Riwaya hizi ziliandikwa na Katama Mkangi. Utafiti uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na mwananadharia Kristeva (1966). Kuingiliana kwa matini katika kazi ya fasihi kuna maana ya kazi moja ya kifasihi kuwa na sifa za tanzu nyingine ndani yake ili kupitisha ujumbe. Visasili viliteuliwa kimakusudi kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Utafiti ulifanywa maktabani kwa kusoma vitabu viteule kwa kina, miswada, majarida, tasnifu na makala mbalimbali yenye data iliyohusu mada hii. Mtafiti pia alizingatia matumizi ya mtandao ili kupata ujumbe zaidi. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kuongozwa na nadharia ya utafiti. Aidha, data ilichanganuliwa kwa kuainishwa kwa misingi ya ubainishaji wa visasili, mchango na umuhimu wake. Kisha, uchanganuzi wa data uliongozwa na maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa mbinu ya kimaelezo na kwa kutoa mifano mwafaka ya aina za visasili katika riwaya teule.Tunatumai kwamba kazi hii itatoa mchango maalum kwa wanafunzi, walimu, wahakiki wa fasihi, wasomi pamoja na wakuza mitaala kwa kuwapa mwanga zaidi kuhusu mchango wa fasihi simulizi katika kukuza na kuendeleza uhakiki wa riwaya teule. Kadhalika, unaangazia suala la kuchanganua visasili kama kipengele cha mwingilianomatini katika ufundishaji na ujifunzaji wa riwaya.

# ABSTRACT

This research evaluated the contribution of oral literature to written literature.The research aimed at depicting the contribution of myths made to the development of novels in Kiswahili. The objective of this research was to show the manifestation of myths and their contributions towards the themes, their significance and importance in understanding the novels of *Mafuta (1984)* and *Walenisi (1995).*The research was lead by the theory of intertextuality that was validated by the theorist Kristeva (1966).intextuality means and implies that one text is anchored in another. So, when reffered to intermingling of texts in literature we meant the work of literature having characteristics of one text within another. The myths were purposively sampled as per the requirements of the research objectives. The research has been done in the library through reading the specified books in details, proposals, magazines, newsletters, journals and related documents concerning the research topic. The researcher also included the use of the internet to get more information. Data analysis was classified based on myths manifestation, their contribution and importance. Finally, the analysis was guided by the research questions, objectives and tenets of the theory of study. The research findings were presented using the description method, giving of relevant examples of the types of myths in the sampled texts. It is to our expectations that the contribution of the study has benefited teachers, literature critiques, academicians, curriculum developers and learners.It has also given insight into identification of myths in novels as well as analysing it as an intertextuality

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Mwingiliano**: Ni hali ya kuwa pamoja na kufahamiana baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

**Mwingilianomatini:** Hii ni nadharia inayotumiwa kuelezea maana ya matini kwa kurejelea matini zingine. Kwa mfano jinsi fasihi simulizi iliingiana na fasihi andishi.

**Msimbo:** Alama iliyotumiwa kuwakilisha dhana fulani.

**Ngano**: hadithi fupi za kimapokeo ambazo wazee aghalabu huwasimulia watoto

**Simulizi:** Kazi ya fasihi kama vile hadithi, ngano na visasili iliyohifadhiwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

**Visasili:** Ngano za kihistoria zinazoelezea asili ya jamii na tamaduni mbalimbali katika jamii ile na namna ilivyofika katika eneo lake la sasa.

**Visakale:** Hadithi za mashujaa wanaosifiwa katika jamii.

# YALIYOMO


**CHUO KIKUU CHA KENYATTA** ........ i

**UNGAMO** ........ ii

**TABARUKU** ........ iii

**SHUKRANI** ........ iv

**IKISIRI** ........ vi

**ABSTRACT** ........ vii

**MAELEZO YA ISTILAHI** ........ viii

**SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI** ........ 1

**1.0 Utangulizi** ........ 1

**1.1 Suala la Utafiti** ........ 3

**1.2 Maswali ya Utafiti** ........ 3

**1.3 Malengo ya utafiti** ........ 3

**1.4 Sababu za Kuchagua Mada** ........ 4

**1.5 Upeo na Mipaka** ........ 5

**1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada** ........ 5

**1.7 Msingi wa Nadharia** ........ 9

**1.7.1 Mihimili ya nadharia** ........ 11

**1.8 Mbinu za Utafiti** ........ 12

**1.8.1 Muundo wa utafiti** ........ 12

**1.8.2 Mahali pa utafiti** ........ 12

**1.8.3 Sampuli lengwa** ........ 12

**1.8.4 Njia na vifaa vya kukusanya data** ........ 13

**1.8.5 Uchanganuzi wa data** ........ 13

**1.8.6 Uwasilishaji wa matokeo** ........ 14

**1.9 Hitimisho** ........ 14

**SURA YA PILI: KUBAINISHA VISASILI KATIKA RIWAYA TEULE** ........ 15

**2.0 Utangulizi** ........ 15

**2.1 Maana ya Visasili** ........ 15

**2.2 Visasili na uamilifu wake katika jamii** ........ 18

**2.3 Ubainikaji wa visasili katika *Walenisi (1995)*** ........ 21

**2.3.1 Kisa cha Moto** ........ 21

2.3.2 **Kisa cha Mchawi** ........ 26
2.3.3 **Kisa cha Mabavu** ........ 29
**2.4 Kubainisha Visasili katika riwaya ya *Mafuta (1984)*** ........ 32
2.4.1 **Kisasili cha Mafuta** ........ 32
2.4.2 **Kisasili cha Matope** ........ 35
2.4.3 **Kisasili cha mama Fofi** ........ 38
**2.5 Hitimisho** ........ 40
**SURA YA TATU: VISASILI KATIKA KUTOA MAUDHUI NA DHAMIRA** ........ 42
**3.0 Utangulizi** ........ 42
**3.1 Visasili kudhihirisha maudhui katika riwaya ya *Walenisi (1995)*** ........ 42
3.1.1 **Maudhui ya Dhuluma** ........ 46
3.1.2 **Maudhui ya ukoloni mamboleo** ........ 48
3.1.3 **Maudhui ya uvumbuzi** ........ 49
3.1.4 **Nafasi ya mwanamke katika jamii.** ........ 50
3.1.5 **Maudhui ya ulaghai** ........ 51
3.1.6 **Maudhui ya siasa na utawala** ........ 53
3.1.7 **Maudhui ya maendeleo.** ........ 54
3.1.8 **Maudhui ya Uongo na Ujinga** ........ 55
**3.2 Visasili katika kudhihirisha maudhui na dhamira katika riwaya ya *Mafuta (1984)*** ........ 57
3.2.1 **Hali ya utabaka** ........ 57
3.2.1.1 **Tabaka Teule** ........ 58
3.2.1.2 **Tabaka la chini** ........ 60
3.2.2 **Maudhui ya mapenduzi** ........ 61
3.2.4 **Maudhui ya Uongo** ........ 62
3.2.5 **Maudhui ya Ubwanyenye** ........ 63
3.2.6 **Maudhui ya Udhuluma na Ukatili** ........ 66
**3.3 Hitimisho** ........ 67
**SURA YA NNE: MCHANGO WA VISASILI KATIKA *WALENISI (1995)* NA *MAFUTA (1984)*** ........ 68
**4.0 Utangulizi** ........ 68
**4.1 Mchango wa visasili katika riwaya ya *Walenisi (1995)*** ........ 69
4.1.1 **Kisasili cha moto** ........ 70
4.1.2 **Kisasili cha mchawi** ........ 73
4.1.3 **Kisasili cha Mabavu** ........ 75

**4.2 Mchango wa visasili katika riwaya ya Mafuta** ........ 79
**4.2.1 Kisasili cha Mafuta** ........ 80
**4.2.2 Kisasili cha matope** ........ 84
**4.2.3 Kisasili cha mama Fofi** ........ 88
**4.3 Hitimisho** ........ 90
**5.0 Utangulizi** ........ 91
**5.1 Muhtasari** ........ 91
**5.2 Matokeo** ........ 94
**5.3 Mapendekezo** ........ 96
**5.4 Hitimisho** ........ 96
**MAREJELEO** ........ 98

# SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu (Wallek na Warren, 1949). Ni aina ya sanaa inayotumia lugha ili kueleza tajiriba za binadamu kama ilivyoelezwa na (Njogu na Chimera, 1999:1994). Utanzu wa riwaya uliwahi kutungwa kwa mitindo mbalimbali ya kimaisha katika mazingira ya watunzi. Mtunzi wa riwaya kama ilivyo kazi zingine za kifasihi, anahitaji kuchagua mtindo uliofaa wa kuwasilisha kazi yake. Kuna vipengele vingi vya kimtindo, mojawapo ikiwa ni visasili. Ni katika misingi hiyo ambapo utafiti huu ulifanywa ili kuchunguza mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi jinsi ulivyotumiwa na mtunzi wa riwaya ya *Mafuta na Walenisi.*

Mada ya mwingilianomatini kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi si ngeni katika fasihi simulizi na andishi ya Kiswahili. Wataalamu wengi wameshughulikia mada hii na kubainisha kuwa fasihi simulizi huingiliana na fasihi andishi akiwemo Mulokozi (1983), Mbughuni (1978) na Said (2002) kati ya wengine. Kwa hivyo, utafiti uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini kuonyesha jinsi visasili vinavyochangia katika fasihi andishi.

Mtunzi wa kazi za kisanaa huwa na funzo kwa jamii. Namna alivyoshughulikia masuala ya jamii inategemea matukio ya jamii, dhamira yake kwa walengwa, imani yake kuhusu masuala aliyoshughulikia na athari aliyonuia kwa wasomaji, au hadhira yake lengwa. Haya yote hubainika kupitia mitindo aliyotumia (Masinde, 1992). Kadhalika, katika kiwango cha jamii, mtunzi hujaribu kutumia visasili kudumisha na kukuza uhusiano baina ya mwanadamu na jamii yake, kutoa mafunzo na maadili yanayojenga mshikamano wa jamii na kutetea masilahi yake ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Riwaya ya Kiswahili ina historia ndefu na iliwahi kutungiwa masuala mengi kwa njia tofautitofauti. Watafiti wengi kama vile Vonyoli (2004) alishughulikia maudhui katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*, Musembi (2008) aliangazia maudhui ya taswira na ukinzani katika riwaya za *Mafuta na Walenisi*, Magaju (2004) alishughulikia uhalisiajabu katika riwaya ya *Babu alipofufuka* ya S.A Mohamed na Binadamu ya Wamitila. Tafiti hizi ni miongoni mwa zingine ambazo zilishughulikia suala la mtindo katika utunzi wa riwaya zilionyesha kwamba vipengele vya mtindo katika utunzi ni vingi na muhimu katika uibushaji wa ujumbe. Inadhihirisha kwamba utafiti kuhusu visasili ulihitajika kufanywa ili kuelewa namna visasili vilibainika katika utunzi wa riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi* na umuhimu wake kama kipengele cha kimtindo.

Kuna umuhimu wa utafiti kufanywa ili kubainisha namna visasili kama kipengele cha kimtindo cha mwingilianomatini vilivyobainika katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*. Vile vile kuna haja ya kufanya utafiti ili kubainisha mchango wa visasili katika utunzi wa riwaya ya *Mafuta na Walenisi* .

Fasihi simulizi huwasilishwa na kusambazwa kwa masimulizi, mazungumzo, kuimba, kughani miongoni mwa zingine. Visasili katika sehemu hii ni muhimu, ni masimulizi ya kiungu yanayoelezea jinsi ulimwengu na binadamu walivyobadilika hadi hali ya sasa. Ni hadithi inayotumika kuelezea asili ya ulimwengu, binadamu na mazingira yake. Tylor (1971) anaelezea kisasili kama jaribio la tafsiri halisi la ajabu ya asili isiyoweza kufikirika kama sheria za asili za watu kwa kuhusisha nafsi ya vitu vilivyo na maumbile ya wanyama. Kulingana na Tylor, fikira za mwanadamu hubadilika kwa hatua kadha wa kadha ikianza na dhana ya kimitholojia na hatua kwa hatua kuelekea kuwa fikira za kisayansi. Matteru (1987) anasema visasili ni visa vya mianzo. Hushughulikia mianzo ya matendo yaliyozoewa.

Visasili ni kipera cha fasihi simulizi ambacho huelezea matukio ambayo yameingiliana katika kutekeleza ujumbe. Utafiti kuhusu mchango wa visasili katika riwaya teule ni muhimu kufanya kubainisha visasili katika riwaya teule, maudhui na dhamira pamoja na mchango wake katika uandishi wa riwaya hizo. Kuna umuhimu wa utafiti kubainisha namna visasili vinavyoingiliana na nadharia ya mwingilianomatini katika riwaya hizo.

## 1.1 Suala la Utafiti

Utafiti ulichunguza mchango wa visasili katika riwaya ya *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Ulibainisha visasili katika riwaya hizi, maudhui, dhamira pamoja na vilivyochangia katika ufanisi wa riwaya teule. Ni muhimu kueleza mchango wa visasili na sababu za mwandishi kutumia visasili katika kuendeleza riwaya zake.

Mwandishi Mkangi amechukua mkabala maalum kwa sababu madhubuti anazozitaja. Jambo ambalo halibainiki kwa watunzi wa riwaya. Pengo hili lilitoa nafasi ya uchunguzi ili kubaini visasili katika riwaya, kudhihirisha maudhui katika kutoa ujumbe na mchango wake katika kufanikisha malengo yake. Katika kufanya hivyo, kipengele hiki cha visasili kitaeleweka vizuri.

## 1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kujibu maswali yafuatayo,

1. Je, visasili vinabainikaje katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)?*
2. Visasili vimedhihirisha maudhui na dhamira zipi katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*
3. Visasili vimetoa mchango gani katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)?*

## 1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti ulikusudia kutimiza malengo yafuatayo

1. Kubainisha jinsi visasili vilivyotumiwa katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*.

2. Kudhihirisha maudhui na dhamira katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*.

3. Kutoa mchango wa visasili katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*.

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Watunzi wengi wa riwaya za Kiswahili walitumia mbinu hii ya visasili katika kuandika kazi zao mathalan *Dunia Yao* (2006) Mohamed, *Babu Alipofufuka* (2001) Mohamed, *Binadamu* (2002) ya Wamitila, *Kusadikika (1991) na Kufikirika (2008)* na Robert miongoni mwa zingine. Hivyo basi, utafiti huu ulitusaidia kujibu swali, kwa nini watunzi wengi wa riwaya ya Kiswahili walitumia mbinu hii ya visasili?

Kulingana na Okpewho (1983) visasili ni malighafi ambayo wanajamii hutumia kuelezea utamaduni wao kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Kwa hivyo dhana hii ilifaa kutafitiwa ili kuendelea kupokezana na kuhifadhi utamaduni katika jamii husika.

Visasili hutumika kwa misingi kwamba fasihi simulizi na fasihi andishi hutumia lugha kwa ubunifu katika kuendeleza ujumbe kwa muktadha wa jamii. Hivyo basi, utafiti huu ni muhimu ili kuonyesha kwamba visasili katika riwaya ni kigezo muhimu katika kusawiri na kuibua ujumbe.

Mtindo hujumuisha vipengele vingi katika utunzi, Visasili ikiwa mojawapo kati ya vipengele hivi. Utafiti ulifaa kufanywa ili kuona namna visasili kama kipengele cha kimtindo hutumiwa ili kufanikisha uibuaji wa maudhui, dhamira na ujumbe anaonuia mtunzi. Aidha, kupitia mtindo, falsafa, msimamo, hisia na mwelekeo wa mtunzi waweza kutambulika. Vilevile, mtindo ni muhimu katika kueleza jinsi msanii alivyoteua maneno na kuyapanga ili kujenga ujumbe wake.

## 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti ulilenga kuchunguza mchango wa visasili katika fasihi andishi ya Kiswahili. Ulishughulikia riwaya mbili *Mafuta (1984)* na *Waleniai (1995)*. Riwaya hizo zote ziliandikwa na Katama Mkangi. Ulichunguza jinsi mwandishi alivyotumia visasili kwa kuzingatia ubainikaji, maudhui na dhamira pamoja na mchango wake ili kufanikisha malengo.

Uchunguzi ulitazama jinsi visasili vilivyotumiwa na pale ulipotumiwa katika mwingilianomatini wa riwaya. Nadharia hii ya mwingilianomatini itatoa mwongozo kamili katika vipengele vya visasili. Mtafiti alijikita maktabani kusoma vitabu viteule, majarida, tasnifu za awali pamoja na makala mbalimbali yaliyotoa wazo kuhusu mada ya utafiti.

## 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Tafiti kadhaa zimeshughulikia utanzu wa riwaya hizi katika matumizi ya mitindo mbalimbali. Vitabu hivi vimefanyiwa utafiti tayari ingawa katika vipengele tofauti tofauti. Baadhi ya watafiti wa awali ni kama vile Musee (2007), Vonyoli (2004) kati ya wengine.

Okpewho (1983) alifanya utafiti mpana juu ya visasili vya kabila la Lo Dagaa linaloishi katika sehemu za kaskazini mwa nchi ya Ghana. Kisa hiki kimehifadhiwa kimaandishi katika kitabu kilichohaririwa na Jack Good kinachoitwa 'The Myth of Bagre'. Kisasili cha Bagre ni kati ya ndugu wawili waliokuwa wakiishi kwa taabu na uhitaji mwingi. Baada ya ndugu hawa kuamua kupitia msituni na porini ambamo walikutana na viumbe vya ajabu ajabu, waligundua ufunuo wa kunga mbalimbali za kukabiliana na kuepukana na majanga ambayo yalikuwa yamewalemea hapo awali. Tajiriba walizopitia ndugu hawa zilizua utaratibu wa matukio. Kisasili hiki kitatoa mchango katika kuangazia mchango wa visasili katika riwaya teule. Hii ni kwa sababu kama

utaratibu ungefuatwa katika mviga wa baadaye katika kabila la Lo Dagaa ungeweza kuvipa vizazi vilivyofuata ufanifu usiokwisha.

Wamitila (1999) alitumia nadharia ya mwingilianomatini katika kuchanganua kazi za kifasihi. Alitumia nadharia hii kuchunguza mtagusano na mwingiliano wa wahusika katika fasihi ya Kiswahili. Katika kufikia azma yake, alirejelea riwaya ya *Asali Chungu* (S. Mohamed) na *Maumbile si Hoja* (John Habwe). Mbali na wahusika, Wamitila alichunguza mwingiliano wa kipengele cha mandhari na vipengele vya mitindo kama vile hadithi ndani ya hadithi. Mhakiki huyu, aidha alipanua uchanganuzi wake kwa kushughulikia mwingiliano kati ya fasihi ya Kiswahili na fasihi ya maeneo mengine kwa mfano, alilinganisha wahusika Mvita na Kidura katika *Kisa Katika Nuru*. Kazi hii inaingiliana na utafiti huu kwa vile alitumia nadharia ya mwingilianomatini ingawa kwa vitabu tofauti. Kwa hivyo, kazi yake itatoa mchango wa mwingilianomatini katika vitabu viteule, katika kuchunguza mwingiliano wa fasihi simulizi katika fasihi andishi. Kazi yake itatoa mchango katika kuelewa nadharia ya mwingilianomatini. Nadharia hii ndiyo itakayoongoza utafiti huu kwa kina. Itaeleza jinsi kazi hii inaingiliana kimaandishi na kutoa mwongozo kikamilifu

Vonyoli (2004) Katika M.A yake, alishughulikia hadithi kama chombo cha maudhui katika fasihi. Uchunguzi wake ulizingatia riwaya za Mkangi, *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995).* Alichanganua kazi yake akitumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Nadharia hii inazingatia kiwango cha ubunifu na uhalisia wa maisha. Katika kazi yake, amesawiri mbinu ya sosholojia. Ameonyesha jinsi fasihi hutekeleza jukumu la kijamaa. Kazi ya Vonyoli itatoa mchango katika utafiti huu kuelewa maudhui katika jamii ya mwandishi pamoja na majukumu ya visasili katika riwaya teule.

Bogonko (2005) alishughulikia uhakiki wa usimulizi katika riwaya ya *Walenisi (1995)*. Bogonko alijadili na kuweka wazi maana na mtazamo na kuonyesha tofauti kati ya mtazamo na usimulizi. Vilevile alionyesha aina za usimulizi na jinsi zinavyodhihirika katika riwaya hii. Alitoa fikira, wakati, mpangilio na uwasilishaji kama kipengele cha usimulizi. Bogonko alitumia nadharia tete kusimulia usimulizi katika *Walenisi (1995)*. Alisema kuwa katika riwaya hii kuna mtindo changamano. Alionyesha hadithi katika riwaya hii imewasilishwa ambapo kuna mimesia na daigesia kama mbinu ya uwasilishaji. Kwa hivyo, kazi hii ya Bogonko ilitoa mchango katika kuchambua visasili katika riwaya ya *Walenisi (1995)*.

Musee (2007) alishughulikia matumizi ya majazi kama mkakati wa kuepuka upigaji marufuku katika riwaya za G.K Mkangi za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Musee alitumia nadharia ya mtindo katika kuhakiki kazi zake, kuonyesha jinsi mwandishi alivyotumia lugha ili kuwasilisha kazi yake. Mtafiti huyu alitumia mbinu ya majazi jinsi ilivyotumika katika riwaya mbalimbali. Utafiti huu kwa kiasi, unaingiliana na utafiti huu kwa vile alitumia vitabu sawa. Dhana ya mtindo katika kazi hii itatusaidia katika utafiti huu kurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya fasihi. Hata hivyo, visasili ni mojawapo ya vipengele vya kimtindo. Kadhalika, itatusaidia kudondoa mwingilianomatini wa visasili katika uandishi wa riwaya teule.

Musembi (2008) alishughulikia matumizi ya taswira na ukinzani kama kichocheo cha zunduko katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Musembi alitumia nadharia za uyakinifu wa kijamaa na nadharia ya uhakiki wa kimtindo kubainisha aina ya ubunifu wa taswira zinazojitokeza katika riwaya za *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Alionyesha jinsi taswira zilivyotumiwa na mwandishi kama kichocheo cha zinduko katika riwaya hizo. Musembi pia alichunguza sehemu ambazo Mkangi ametumia ukinzani katika riwaya hizi kwa nia ya kumzindua msomaji. Kwa hivyo, kazi hii itatoa mchango katika kudhihirisha maudhui na

dhamira na pia kuelewa malengo ya mtunzi katika kazi yake katika kuelewa kusudi la mtunzi na kuelewa ni nini hasa alitaka kuiambia jamii husika kupitia visasili. Mwisho itatusaidia kutoa majukumu ya visasili katika jamii.

Ireri (2011) alifanya utafiti wa tamthilia kama utendi, uchanganuzi linganishi wa tamthilia za *Kinjekitile* na *Mzalendo Kimathi*. Alitumia nadharia ya mwingilianomatini ambayo ni mkabala wa kuelezea maana ya matini. Ireri alitumia mbinu ya utendi katika kazi zake. Ingawa Ireri alitafiti tamthilia, alitoa mchango mkubwa katika kuelezea maana na matumizi ya nadharia ya mwingilianomatini. Kazi yake itatupea mwelekeo kuhusu nadharia ya mwingilianomatini. Nadharia hii itatoa mwongozo dhabiti katika kufanikisha malengo ya utafiti.

Waruguru (2014) alishughulikia lugha ya mafumbo katika riwaya za Mkangi *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Waruguru alitaka kubainisha mifano ya matumizi ya lugha ya kimafumbo ya kisasa. Kwa hivyo, kazi yake itatoa mchango muhimu katika kubainisha visasili katika vitabu viteule. Visasili alivyoandika mwandishi vimeandikwa kimafumbo. Kazi hii itasaidia kuvifafanua ili viweze kueleweka kikamilifu. Hata hivyo, mwandishi Mkangi anapenda kuandika kazi yake kimafumbo.

Kang'e (2014) alichunguza na kuchanganua mwingilianomatini katika tamthilia ya Mashetani (1971) na Kijiba cha Moyo (2009). Viwango na aina za mwingilianomatini zilichunguzwa na kubainishwa. Alitumia mbinu ya klitahamano na kuongozwa na nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na Kristeva (1966). Vifungu vilivyodhihirisha uhusiano wa kimatini vilidondolewa kutoka kwa tamthilia zote mbili. Alibainisha kwamba kuna mwingilianomatini baina ya tamthilia ya mashetani (1971) na kijiba cha Moyo (2009). Pia alibainisha kwamba maudhui na fani zimechangia viwango vya mwingilianomatini katika tamthilia hizi mbili zilizochunguzwa.

Ilibainika kuwepo kwa mwigo na wigobezi kama aina ya mwingilianomatini za tamthilia hizi mbili. Kwa hivyo, utafiti wa Kang'e (2014) unatarajiwa kutoa mwongozo wa kuelewa nadharia ya mwingilianomatini kwa mtafiti, wahakiki, wahadhiri, walimu na wanafunzi wa somo la fasihi.

Omotimba (2015) alishughulikia usimulizi katika riwaya za *Adili na Nduguze, Walenisi* na *Babu Alipofufuka.* Alitumia nadharia ya miundo na maumbo tengamano iliyoasisiwa na Parry (1992). Nadharia ya muundo tengamano ni kitengo cha naratolojia. Lakini ikija kwa upande wa fasihi simulizi, Olriki (1999) ambaye ni mojawapo wa waasisi walioboresha nadharia hii alitaka kubaini kama iwapo kulikuwepo na sifa bainifu za aliyoita masimulizi yaliyojumuisha visakale, visasili, mighani na nyimbo. Mtazamo huu ulijikita katika usimulizi na ulinganifu wake na utamaduni. Hata hivyo, ulipuuza fasihi andishi. Olriki (1999) aliona kuwa masimulizi fulani yalipoingia katika fasihi andishi yalielekea kupoteza baadhi ya sifa bainifu. Kazi hii itatusaidia kuelewa tofauti iliyoko kati ya visakale, visasili na mighani. Itatusaidia kuelewa kuwa visasili kama kipengele mojawapo cha fasihi simulizi na kinatolewa kwa njia ya masimulizi. Itatuongoza kubainisha visasili katika riwaya teule.

## 1.7 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Nadharia ya mwingilianomatini hujihusisha na ule uwepo wa sifa mbalimbali au zaidi katika kazi fulani ya fasihi kama vile matumizi ya nyimbo, matumizi ya barua, masimulizi za hadithi ndani ya hadithi na kadhalika. Kwa hivyo, kuingiliana kwa matini katika kazi za fasihi humaanisha kazi moja ya kifasihi kuwa na sifa za tanzu nyingine ndani yake ili kupitisha ujumbe.

Mwingilianomatini ni mkabala wa kuelezea maana za matini kwa kurejelea matini zingine. Aidha, yaweza kumaanisha hali ya mwandishi kuazima na kukarabati matini kwa kurejelea matini ya kitambo au msomaji kurejelea matini moja katika kusoma nyingine.

Nadharia ya mwingilianomatini ina asili yake katika isimu ya karne ya ishirini hasa katika kazi ya mwana isimu wa Kiswisi Ferdinand de Saussure (1982). Msisitizo wake de Saussure (1982) wa sifa taratibu za lugha ulijenga uhusiano wa maana wa matini. Kwake de Saussure, ishara za kiisimu hupata maana kwa sababu ya uhusiano wa kishirika na kimuungano na ishara zingine za kiisimu. Ishara huishi katika mfumo wa kutoa maana kwa mujibu wa kufanana au kutofautiana na ishara zingine.

Hata hivyo, kuna madai kuwa ‘mwingilianomatini’ pia ulitokana na nadharia ambazo zinahusu kuwepo kwa lugha katika hali maalum za kijamii. Mwananadharia wa kifasihi, Bakhtin 1978 alieleza kuwa maneno huishi katika maeneo fulani za kijamii na kitambo cha matamko na kupokelewa kwa matamko hayo.

Istilahi ya mwingilianomatini ilibuniwa na mwananadharia Julia Kristeva, mwaka wa 1966. Kiini chake ni jaribio lake Kristeva (1966) la kuainisha umuundo-semiotiki wa de Saussure (1982) na usemesano wa Bakhtin. Kulingana na Kristeva (1966), dhana ya mwingilianomatini ilichukua nafasi ya dhana ya mwingiliano dhanifu. Fauka ya hayo, Kristeva (1966) alisisitiza kuwa maana haihamishwi moja kwa moja kutoka kwa mwandishi hadi kwa msomaji lakini ilitafakarishwa kupitia kwa msimbo wanayopata mwandishi na msomaji kutoka matini zingine. Kama alivyosema Barthes (1972), maana ya kifasili haiwezi kudhibitiwa na msomaji kwa kuwa sifa za kimwingilianomatini za kazi ya kifasihi humrejelesha msomaji mahusiano mapya ya kimatini.

Matini za kifasihi hubeba maana ambazo wasomaji huzichambua. Ikumbukwe kuwa kazi za kifasihi zilijengwa kutokana na mifumo, misimbo na desturi ambazo ziliimarishwa na kazi tangulizi za kifasihi. Mifumo, misimbo na desturi za sanaa zingine pamoja na utamaduni kwa jumla ni muhimu katika maana ya kazi ya kisanaa.

Matini ziwe za kifasihi au zisizo za kifasihi ziliangaliwa na wananadharia wa kisasa kukosa maana inayojitegemea. Sanaa ya usomaji hutuelekeza kwenye utando wa mahusiano ya matini. Uchanganuzi wa matini na kubainisha maana yake (zake) kunahusu kufumbua maana za matini hizi. Ni kwa mujibu huu ambapo utafiti huu ulichunguza mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi wa riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995).* Waandishi wa kifasihi hawachagui tu maneno kutoka mfumo wa lugha, masimulizi, sura za wahusika hata virai na sentensi kutoka matini tangulizi za kifasaha na desturi ya kifasihi.

### 1.7.1 Mihimili ya nadharia

Mihimili ya nadharia ya mwingilianomatini ni tatu. Mtafiti ananuia kutumikiza mihimili hii kwa ambavyo kimsingi lengo lao litakuwa kudhihirisha kuwepo kwa visasili katika kusawiri ujumbe na mchango wake katika fasihi andishi. Mihimili hii pia inamfaa mtafiti katika kuhitimisha na kutoa mapendekezo. Mihimili ya nadharia hii ni,

1. Maana ya matini hujihusisha na ule uwepo wa sifa mbalimbali au zaidi katika kazi fulani ya fasihi. Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza dhana ya visasili na kubainisha jinsi vilivyotumiwa katika riwaya teule.
2. Kazi za kifasihi zilijengwa na mfumo, misimbo na desturi ambazo ziliimarishwa na kazi za kifasihi zilizotangulia. Mhimili huu ulitusaidia kudhihirisha maudhui na dhamira ya visasili katika kufanikisha ujumbe alionuia mwandishi wa riwaya teule.

3. Maana ya matini haihamishwi moja kwa moja bali ilitafakarishwa kupitia msimbo kutoka matini zingine. Hata hivyo maana ya kisasili haiwezi kudhibitiwa bali humrejelesha msomaji mahusiano mapya ya kimatini. Mhimili huu ulitusaidia kuonyesha mchango wa visasili katika riwaya teule.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii vipengele vya muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, sampuli lengwa, njia ya kukusanya data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ulijadiliwa.

### 1.8.1 Muundo wa utafiti

Muundo wa utafiti ulitoa maelezo kuchunguza sifa zinazobainika katika jambo fulani linalochunguzwa. Dhima yake ni kuchunguza hali ya mambo jinsi ilivyo katika mazingira fulani. Lengo kuu katika muundo huwa ni kukusanya data na kubainisha uhusiano baina ya vigezo husika. Kupitia muundo huu, maelezo kuhusu visasili katika riwaya yalipitiwa na kisha maelezo kuhusu utafiti kwa jumla yalitolewa kwa kuzingatia mada za kimsingi.

### 1.8.2 Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani katika chuo kikuu cha Kenyatta. Usomaji wa kina ulifanywa kwa kusoma vitabu, majarida na marejeleo mengine kuhusu mada. Usomaji wa maktabani pia ndio ulioniwezesha kupata pengo la utafiti kwa kusoma vitabu, majarida na tafiti mbalimbali zinazozungumzia mada hii. Vilevile, ni katika usomaji maktabani ambapo data muhimu kuhusu mada ilipatikana pamoja na msingi wa nadharia iliyoniongoza katika utafiti.

### 1.8.3 Sampuli lengwa

Sampuli lengwa huweza kuteuliwa kwa misingi ya malengo ya utafiti ili mtafiti aweze kuafikia malengo yake. Mtafiti hulazimika kuteua sampuli lengwa kimakusudi kwa vile akitumia njia

zingine atapata sampuli isiyofaa utafiti wake. Hii ni kwa sababu malengo yake huwa yamelenga sampuli maalum katika sampuli pana. Mtafiti kwa hivyo hulazimika kuteua kimakusudi sampuli ambayo kwa maoni yake anafikiri itamfaa. Sampuli lengwa ilikuwa vitabu vya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Vitabu hivi vilichaguliwa kimakusudi kwa vile vina data iliyohitajika kutimiza malengo ya utafiti.

### 1.8.4 Njia na vifaa vya kukusanya data

Data ilikusanywa kwa kusoma kwa kina vitabu viteule pamoja na uhakiki wake wa kina. Usomaji huu ulifanywa kwa kusoma kwa ndani vitabu hivi kwa kuzingatia mtazamo wa jumla na kisha kuvisoma kwa kuzingatia muundo na maumbo ya visasili vinavyohusiana navyo. Usomi huu pia ulifanywa kwa kuzingatia mfumo wa nadharia ya mwingilianomatini pia data ilikusanywa kwa kusoma majarida, tasnifu pamoja na Makala mengine yaliyozingatia malengo ya utafiti kwa kuzingatia mchango wa visasili katika fasihi andishi na mahali ambapo mtindo huu ulitumika.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa data

Data iliyokusanywa, kwanza ilipangwa kwa kuzingatia mchango wa visasili katika riwaya teule. Kisha, uchanganuzi ulifanywa kwa kuzingatia jinsi dhana ya visasili ilijitokeza katika riwaya, mchango wa visasili katika kuendeleza maudhui na kutoa mchango wa visasili katika riwaya hizo. Pia uchanganuzi ulizingatia maswali ya utafiti, malengo kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ambaye ndiyo iliyokuwa mwongozo wa kuweka utafiti katika mizani ifaayo. Mwisho uchanganuzi ulifanywa kwa kuongozwa na maswali ya utafuti ili kuweza kuleta ule uhusiano uliopo kati ya malengo na matokeo ya kazi yetu.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa matokeo

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo.Aidha, mifano ya sehemu za visasili ilinukuliwa ili kubainisha mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi. Vilevile, matokeo yaliwasilishwa kwa kuzingatia maswali na malengo ya utafiti na ufafanuzi wa mbinu katika kuendeleza riwaya hizo.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imerejelea mambo ya kimsingi yanayohusu utafiti kwa jumla iliangazia suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mihimili yake pamoja na mbinu za utafiti. Hii ni sehemu inayoweka msingi dhabiti wa utafiti huu kwa jumla. Ni sehemu muhimu katika utafiti huu kwa vile uliweka nguzo ya kurejelewa kila mara katika utafiti huu. Inaonyesha malengo yatakayoendeleshwa na maswali yatakayojibiwa hadi mwisho wa utafiti.

# SURA YA PILI: KUBAINISHA VISASILI KATIKA RIWAYA TEULE

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inadhihirisha na kubainisha visasili katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Visasili ni ngano za kihistoria zinazoelezea chimbuko la jamii au la kabila fulani, tamaduni mbalimbali katika jamii ile na namna jamii hiyo ilivyofika katika eneo lake la sasa. Visasili husaidia kuelezea asili ya mambo yasiyoelezeka kama vile kifo, tohara na mengine. Kadhalika, huelezea matukio mbalimbali katika jamii na mazingira ya mwanadamu.

Sehemu hii pia itatoa maana ya visasili na uamilifu wake katika jamii na kutafuta jibu kwa maswala yanayotatiza binadamu katika ulimwengu unaomzunguka.

## 2.1 Maana ya Visasili

Visasili vimeelezwa kwa njia mbalimbali kimapokeo. Baadhi ya maelezo yanasema kwamba ni hadithi ambazo huwa na wahusika wa aina tofautitofauti hasa miungu na binadamu, husimulia juu ya matukio ya kiada (Matteru 1987). Kama jina la utanzu huu linavyoakisi, visasili ni visa vya mianzo. Hushughulikia mianzo ya matendo yaliyozoewa kama unyago, ndoa, tohara na imani mbalimbali. Mbali na kufafanua mianzo ya desturi, hutoa utaratibu unaofuatwa katika utekelezaji wa desturi hizo. Wakati mwingine, matukio yanayotambwa katika visasili hufumwa katika lugha ya kimafumbo.

M. Muller (1861) aliita kisasili 'ugonjwa wa lugha.' Alieneza habari kuwa visasili vilitokana na ukosefu wa majina yaliyofupishwa na yasiyochukua shamirisho la jinsi katika lugha za jadi, zikiwa na maumbile ya kibinadamu za usemi zinazohitajika katika lugha hizo. Baadaye zilichukuliwa hivi hivi, na kuelekea kwa dhana kuwa ajabu za asili vilivyokuwa viumbe vyenye hisia za miungu.

Tylor (1871) alitafsiri kisasili kama jaribio la tafsiri halisi la ajabu ya asili isiyoweza kufikirika kama sheria za asili kati ya watu. Wanadamu wa kwanza walijaribu kueleza ajabu ya asili kwa kuhusisha nafsi na vitu vilivyo na maumbile ya wanyama. Hii hupeana asili ya unyama. Kulingana na Tylor, fikra za mwanadamu hubadilika kwa hatua kadha wa kadha ikianza na dhana za kimitholojia na hatua kwa hatua kuelekea kuwa fikra za kisayansi. Si wasomi wote, si hata wasomi wa karne ya kumi na tisa wamekubaliana na mtazamo huu. Kwa mfano, Lucien Levy-Bruhl alidai fikira za akili ya mwanadamu, sio hatua ya maendeleo ya kihistoria.

Frazer (1922) anavieleza visasili kama uigaji wa matukio kitamathali ambayo hapo awali yalihusishwa na sherehe kama uganga, uchawi na uramali. Kadhalika, aliongezea kuwa visasili huliwekea mantiki tukio la kiada, chanzo chake na jinsi ulivyopokewa na vizazi mbalimbali vya jamii husika.

Graves (1969) anasema visasili ni durusi za kidini au kishujaa zilizo za kigeni kwa tajriba ya mwanafunzi kiasi kuwa huwezi kuzisadiki kuwa kweli. Kisasili kina majukumu mawili. Kwanza, ni kujibu maswali magumu wanayouliza watoto kama vile; "Nani aliumba dunia? Itaishaje? Nani binadamu wa kwanza? Nafsi huenda wapi baada ya mauti…" Jukumu la pili la kisasili ni kuyakinisha mitindo ya kijamii iliyoko na kanuni za tamaduni na mila. Graves katika 'Larousse Encyclopedia of Mythology' (1969) anasema visasili ni vitu ambavyo havikutokea lakini daima vipo.

Stevenson (1969) ansema usasili wa Kigiriki umeumbika kwa kiasi kikubwa kutokana na hadithi za miungu ya kike na kiume, na isisomwe kama namna ya Biblia ya kigiriki. Kwa mujibu wa dhana za kisiasa zaidi, kisasili halisi hakina uhusiano wowote na dini. Ni maelezo ya kitu kikawaida jinsi kwa mfano chochote kina kila kitu kilivyokuja kuweko; watu, wanyama, miti na

maua. Visasili ni sayansi ya awali, matokeo ya majaribio ya watu kujaribu kuelezea kile walichokiona katika mazingira yao. Lakini kuna vile vilivyoitwa visasili visivyoeleza chochote kabisa. Ni visa ambavyo wangeambiana mmoja kwa mwingine msimu mrefu wa baridi jioni.

Dundes (1984) anaeleza kisasili kama masimulizi ya kiungu yaliyoelezea jinsi ulimwengu na binadamu walivyobadilika hadi hali yao ya sasa. Alielezea kuwa ni hadithi iliyotumika kuelezea asili ya ulimwengu wa utamaduni kwa kuelezea vipengele vya ulimwengu, desturi, usawa na matendo ya jamii.

Ions (1987) anaeleza kuwa visasili ni jamii ya kale iliyo katika hali yake asilia na siyo tu ya kisa. Hadithi hizi zina ukale na uhalisi ulio muhimu ambao maisha ya sasa, jaala na binadamu hutawaliwa. Ufahamu huu humpa binadamu nia kwa tamasha na adili.

Mulokozi (1989:6) anasema kuwa visasili ni hadithi za kale zenye kuwakilisha imani na mtazamo wa jamii inayohusika kuhusu asili ya ulimwengu na mwenendo wake, kuhusu asili yao wenyewe, na maana na shabaha ya maisha yao. Mara nyingi hadithi hizi huaminiwa kuwa kweli tupu na hutumika kuelezea au kuhalalisha baadhi ya mila na madhehebu ya jamii husika.

Austin (1990) ametoa hoja kwamba kisasili kimekusudia kutoa maelezo toshelezi kuhusu kila kitu kwa vipengele na sheria za desturi, kwa mipangilio ya kijamii, mifumo ya kijamii na uwezo wa kufikiri. Hivyo basi, kisasili ni usemi wa kitamaduni ulio na uasilia wa kitu kilicho na umuhimu kwa jumla.

Hatab (1990), anasema kuwa kisasili ni masimulizi yaliyofichua dunia iliyotukuka kiungu.

Ngure (2003) anaelezea visasili kama neno linavyoelezea kufafanua maana kuwepo kwa vitu, uhusiano wa vitu au hali mbalimbali.

## 2.2 Visasili na uamilifu wake katika jamii

Fasihi simulizi hudai ukale na huonekana katika jamii zote. Visasili huibuka na kuoana na utamaduni wa jamii husika na uhusiano wa watu pamoja na jumlisho la amali zao. Katika amali zetu za kale kabla ya jamii kukumbwa na mifumo ya kibepari ambayo ilizaa matabaka katika jamii, kulikuwa na msisitizo wa ari na juhudi za kazi pamoja na uendelezaji wa sehemu kadha za utamaduni kama vile mambo ya ndoa, uzazi, malezi, marika, mafunzo mbalimbali ya mazingira na shughuli nyingine kama jando, sherehe maalum na pia amali zinazohusiana na imani katika miungu, mashetani na mizimu. Kwa wakati wote huo, visasili vimekuwa chombo cha kuhifadhi, kulinda, kutunza na kuendeleza amali hizo ambazo zilikuwa msingi wa maisha ya wanajamii.

Amali hizi ni tamaduni, mila na desturi, dini, siasa, uchumi na kadhalika. Amali hizi sharti zihifadhiwe katika uasili wake. Kujenga na kuhifadhi lilikuwa jukumu la taaluma ya visasili. Dhima nyingine ya visasili ilikuwa ni kutafuta ukweli kwa kuvihakiki na kuvichambua vipengele vyote vya kimaisha. Kutokana na dhima hiyo, visasili viliweza kutumika kama chombo cha uhusiano bora na chombo chenye nguvu na misingi imara. Jamii haiwezi kukua na kuendelea bila fasihi, visasili ikiwemo. Visasili katika jamii hutumika kama chombo ambacho humchora na kumwonyesha mwanajamii vile alivyo na uwezo wa kushirikiana na wenzake pamoja na kushirikisha elimu na ujuzi alionao kwa manufaa ya jamii. Visasili vilitumiwa kama chombo cha kurekebisha na kuunda upya hadhi na utu wa wanajamii katika nyanja mbalimbali za maisha yao. Kutokana na hadhi hiyo twaweza kudokeza kwamba visasili ni sanaa madhubuti inayokua na kukomaa kufuatana na mabadiliko ya wakati, jamii na mazingira. Hekima na mantiki ipatikanayo katika tanzu mbalimbali za visasili ni amali kubwa kwa mwanajamii aliyetalamikia kuweza kuitumia kwa kutatua matatizo mbalimbali kama vile ya ndoa, ujinga, maradhi, uchumi,

siasa na umaskini. Visasili hutumika kama ghala ya rasilimali na amali za uafrika na hivi leo yatumika kama chemichemi ya fasihi andishi, kama Sengo (1973: 77) anavyotuelezea.

Visasili hutumika kama mtumishi wa maisha ya watu au wanajamii. Inatumika kama chombo cha pekee na kujenga umoja katika jamii husika. Kwa mujibu wa maoni ya Plekhanov (1957) fasihi (fasihi simulizi ikiwemo) ni chombo mojawapo katika harakati dhidi ya mazingira. Mtazamo huu unashikilia kwamba sanaa haina budi kutumiwa kumsukasuka na kumzindua mwanajamii ili apambane na mazingira machafu. Ili visasili iwe na manufaa katika jamii ni lazima iwe na jukumu la kuieleza jamii, kuichambua, kuikosoa na kuiongoza katika lengo lake la kupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii.

Mbali na hayo, visasili hutumiwa kama chombo cha kutoa pongezi kwa watu binafsi ambao wametoa mchango wa kuiendeleza jamii. Kwa wembe huohuo, inatumiwa kushtumu wanajamii ambao nia yao ni kuipotosha jamii. Visasili kwa karne mingi katika janibu mbalimbali za ulimwengu, imetumika kama chombo cha wanyonge ambao ndio wengi katika jamii za kiulimwengu. Fasihi hii hutumiwa kutoa hisi za wale ambao hawawezi kujieleza kwa njia za maandishi. Kwa vile umma wa watu walio wengi hawajui kusoma na kuandika, wanajamii hawa hawana njia nyingine za kutoa hisi za mawazo zao isipokuwa kwa kutumia chombo hiki cha Sanaa.

Visasili ni mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi vinavyotumia lugha ya mfululizo. Kipera hiki kilizuka tangu jadi. Mara nyingi husimuliwa jioni. Huu ni wakati ambapo jamii huwa inapumzika baada ya kazi za siku kutwa. Kushuka kwa utanzu huu kunaonyesha jamii ilikuwa imetulia na hii ndiyo ilikuwa njia ya pekee ambayo ingetumiwa kuelezea dhana tofauti, desturi

na amali mbalimbali za jamii kwa njia ya kinathari. Visasili hivi vilikuwa mali-bia, yaani zilikuwa mali ya jamii.

Visasili vilitumiwa kuipa jamii mwelekeo. Kuna methali isemayo kwamba mwacha asili ni mtumwa. Jamii inayoipuuza kale yake au fasihi yake hukosa mwelekeo. Visasili hufumbata mtazamo wa jamii pamoja na falsafa yake nzima. Falsafa hii huwa kielekezi cha jamii husika.

Hutumiwa kuyaendeleza maadili ambayo huwa kama nguzo kuu ya wanajamii. Kila kisasili huwa na funzo maalum. Funzo hilo hutokana na mambo yanayopatikana katika hadithi hiyo. Kwa mfano, chanzo cha wivu na matokeo yake, uadui kati ya ndugu na majamaa ulianzaje?

Visasili kadhalika huonya, huadhibu, huelimisha, hushauri na kuinasihi jamii. Visasili huwa na wahusika wenye wasifu fulani wanaotumiwa kuelekeza kwenye sifa nzuri au zinazopaswa kupuuzwa. Hao wenye sifa nzuri huweza kuangaliwa kama vielelezo bora vya jamii ifaayo.

Visasili hutumiwa kurithisha jamii elimu, thamani na amali muhimu toka kizazi kimoja hadi kingine. Tumetangulia kuona kuwa fasihi simulizi ina nafasi kubwa katika tamaduni simulizi yaani tamaduni ambako taarifa na elimu hutegemea sana fasihi simulizi. Tanzu ya visasili huwa nyenzo kuu kurithishwa elimu ya jadi katika jamii husika.

Visasili pia hutumiwa kama burudani. Katika jamii nyingi, utambaji wa visasili huwa wakati wa jioni hasa baada ya kazi kutwa. Usimulizi huu ulikuwa njia nzuri ya kuwaburudisha wasikilizaji.

Tunaweza kusema kuwa visasili hutumiwa pia kuendeleza uhusiano uliopo kati ya wanajamii na hasa uhusiano wa kushirikiana. Hii ni kwa sababu utambaji wa visasili unahusisha hadhira pana, tofauti na usomaji wa kitabu. Wakati wa kusimulia kwa hadithi, watu walijumuika pamoja na kwa njia hii kujenga msingi imara wa ushirirkiano wa kijamii.

Usimulizi wa visasili una jukumu kubwa la kukuza uwezo wa watoto wa kuyakumbuka mambo, yaani unaboresha uwezo wao wa kumbukumbu. Hali hii hutokana na tabia ya kuwasimulia watoto au vijana visasili na kuwataka wasimulie visasili hivyo kwa wenzao.

Visasili hutumiwa kuelezea sababu za hali zilizoko au hali zake za sasa. Kwa mfano, kuelezea asili ya matukio fulani ya kimaumbile au tabia fulani ya kitamaduni.

Visasili hutumiwa kukuza na kuendeleza ufahamu mpana au maarifa ya wanadamu. Kutokana na visa hivi, mwanajamii anaukuza uwezo wake au fahamu zake za kujua jinsi ya kuiepuka mitego ya kiujanja.

## 2.3 Ubainikaji wa visasili katika *Walenisi (1995)*

Sehemu hii imeshughulikia ubainikaji wa visasili jinsi vilivyotumika katika riwaya ya *Walenisi (1995)*. Visasili hivi ni kisa cha moto, kisa cha Mchawi na kisa cha Mabavu. Vimebainishwa kama ifuatavyo.

### 2.3.1 Kisa cha Moto

Katika kisa hiki mzee Moto aligundua moto kwa bahati tu. Siku moja, alikuwa ameketi chini ya kivuli cha mbuyu. Alikuwa akifanya hivyo kwa kungojea kulungu kunaswa na mtego wake. Hapo mbuyuni ndipo palikuwa na njia ya kulungu ya kwenda mtoni kunywa maji. Haikuwa mara yake ya kwanza kutega kulungu. Alikuwa amewanasa wengi kwa muda mrefu sana. Alifurahia nyama yao. Kwa sababu ya vifaa butu vya mawe, haikuwa rahisi kuwachuna. Pia alikuwa akiwala wabichi.

Ili kujipa kazi akiwasubiri, akaonelea amtengenezee utunda mpenzi mkewe. Hakuwa na shida kuamua utunda huo ungekuwa wa aina gani. Nyakati hizo, shanga zilikua bado hazijavumbuliwa. Ni jiwe na mti tu ndivyo vilikuwepo, navyo ndivyo vilikuwa malighafi.

Kwa ala yake, jiwe la kuchonga na Moto akakata vijiti viwili. Dhamira yake ilikuwa ni kutengenezea mkewe ushanga na tembe zikiwa za mti. Kwa vijiti hivi viwili kikubwa akakiita ‘mama’ na kile kidogo ‘baba’. Akiweka kijiti mama chini, alitumia kijiti baba kupekecha tundu. Alifanya hivi kwa nguvu zake zote. Haja ilikuwa ni atoboe matundu mengi halafu ayakate na kuyaviringisha na baadaye ayaunge na uzi wa mmea ili apate huo ushanga. Akizidi kupekecha na jasho kumtoka, na huku mawazo yake yote yakiwa juu ya uso wa mkewe, hakuwa ameona cheche zikianguka juu ya majani makavu yaliokuwa katikati ya mapaja yake. Alichokihisi kwa ghafla kilikuwa ni kuchomeka na kuona moshi ukifusika. Alishtuka na akaruka kwa woga. Hakuwa ameshawahi kuona kioja kama hiki maishani!

Cheche hiyo ikaanza kusambaa. Ilijieneza kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Ikawa imepata nguvu na kuenea kwa upesi na kumeza vichaka na misitu iliyokuwa mbele yake. Kutoka kwa upande wa mtegoni, kukajaa harufu nzuri ya kunukia. Mzee Moto alifuata na alipofika akaona kulungu ambaye alikuwa ameshikwa na mtego, ameokwa vizuri sana na nguvu hizo ngeni. Hakujua zinaitwaje wala hakujua aziiteje. Hakuwa ameshawahi kuona ama kuonja kitu cha kuchoma na je cha kupikwa?

Harufu ya kuila kulungu na kudondoka kwa mafuta ya kunona vilimtia ujasiri mtu Moto. Kwa hatua za woga, akanyatanyata na akanyafua kinyofu na kukionja. Kwa utamu huo aliousikia sasa akanyafua jinofu. Halafu akaingilia maini, moyo na mafigo. Kulungu akamshinda ingawaje alimla maradufu ya kawaida yake. Aliyebaki alimfunga ndani ya majani ya mgomba na kuwapelekea watu wake, akawa amechukua pia kinga kilichokuwa kikiwaka na vile vijiti viwili ambavyo baadaye kijiti mama alikuja kukiita ‘wimbombo’ na kijiti baba ‘ulindi.’

Asubuhi moja alfajiri watu walistukia “tatata” za kualikwa kwa kuni na kulipuka kwa moshi kutoka nyumbani kwa moto. Nyumba yenyewe ilionekana ikiwa na nuru nyekundu ya ajabu na ya kutisha. Walinyatanyata kuelekea kwenye kioja hicho.

Walivutiwa zaidi kwani walivyozidi kukisongelea ndivyo jinsi baridi ya asubuhi ilivyozidi kuwatoka. Mvuto huo ukawapumbaza. Walipumbazika zaidi walipoona nyuma ya kioja hicho na kupita pazia la moshi, Moto ameketi.

Macho ya mtu Moto yalionekana mekundu mno. Hii ilikuwa ni kwa sababu ya moshi lakini hawakuwa wakijua hivyo. Kiwiliwili chake kilionekana kikiyumbayumba nyuma ya miale. Haya yote yakamfanya kutisha wenzake wasijue la kufanya kwa sababu ya bumbuazi. Wakawa wamesimama tuli wameduwaa. Hapo ndipo waliposikia sauti ikinena, “Mimi ndimi moootoo…., naivisha na kuunguza, natekeza na naoteka, anitakaye nitakuja kwake na nimpe uwezo huu wangu…”

Kuwaogofya zaidi, akaupulizia nao ukaalika kwa moshi na cheche nyingi ziliwafanya wenzake kurudi nyuma kwa hofu. Kuona hivi akaendelea kuwatia woga kwa kuwaonyesha nguvu za moto na kuwahimiza waje ili awageuzie maisha. Aliwagawia sehemu ya nyama ya kulungu na akawaambia wale. Kila mmoja wao akakubali kuwa ilikuwa tamu sana. Naye ndipo alipowaambia siri ya kioja. Hakuwaambia ule ukweli wa mambo badala yake aliwaambia ati ni malaika ndiye aliyewatunukia uwezo huo! Aliwalambisha kwa kuwapa kaa kuchukua makwao. Nao kwa kukosa jina la kufaa, wakaliita, ‘moto’.

Punde tu, watu walizoea moto na wakawa wanakuja kwake. Hakutaka uenee vivi hivi tu. Kwa hivyo akaweka masharti. Moto ulipatikana kwake tu kila jioni na uzimwe mara moja baada ya matumizi. Ni hapo kwake tu ambapo ‘moto mpya’ ungeweza kupatikana. Moto hauibiki wala

haufichiki, akawakanya. Na ambaye angefanya ujasiri wa kuiba ama kuuficha basi asije kulia baadaye.

Watu walifuata masharti haya mtu Moto akawa mgawaji wa moto wa pekee. Uwezo huu ulimtia hisia za ukubwa na utukufu. Watu sasa wakawa bila moto hakukuliwa kitu na basi kumtegemea yeye kukazidi. Hapa ndipo aliwageukia na kuwaambia, "ili kuulinda huu moto mtakatifu usife, imenibidi kuacha kazi zangu. Lakini siko radhi kuendelea kufa njaa na familia yangu".

Watu walizidi kumgawia chakula chao ili azidi kuuchunga huo moto mtakatifu usife. Basi kwa kila mtu kumpatia theluthi ya chakula chake, mtu Moto akapata uwezo wa kurundika ziada. Watoto wake na mkewe wakawa hawana haja ya kufanya kazi. Watu hawakukoma kumpatia "kodi ya moto" ndivyo yeye na kizazi chake walivyozidi kujiepusha na kufanya kazi huku wakizidi kuzua masharti magumu ya kuficha "utukufu wa moto".

Kisa cha moto kimeingiliana katika uandishi na ukoo mmoja wa kichuna ambao ulizuka kujipatia utukufu uwezo na hekima kwa kutumia hila zilizoweza kuwapa utawala juu ya wenzao na kula jasho lao. Uvumbuzi wa moto ni tukio la zamani sana ambao ulitokea kighafla tu bila mtu kupanga wala kutarajia. Mwisho ukawa na maana katika jamii nyingi za kiafriika. Wachuna pia walizuka kighafla kama cheche za moto, mwishowe walienea kote duniani kama moto ndani ya msitu na kunyakua ardhi nzima bila kujali manufaa ya wengine. Walilamba kila kitu na kujinyakulia mali yote huku wengine wakiteseka.

Mwandishi anadhihirisha kisasili cha moto kama ishara ya wageni hasa waliotawala bara la Afrika. Kinaeleza jinsi Wachuna walivyoimarisha falme zao. Walishuka kama moto na kusambaa kila mahali duniani. Wachuna walitumia ulaghai ili waweze kujidumisha. Uchuna ulipoendelea zaidi, kukatokea falme mbalimbali za Wachuna. Ndipo tunaelezwa juu ya madola

manne yaliyopimana nguvu. Dola la mashariki, dola la magharibi, dola la kusini na dola la kaskazini. Kila dola lilijaribu kujipanua kushinda mengine. Wakati huu mila, desturi, utamaduni na lugha za watawala ndizo zilitambuliwa. Watawaliwa wakaanza kuwaiga watawala katika mambo hayo yote.

Mwandishi alitumia neno hili Wachuna kimajazi katika kudhihirisha kisasili cha moto kumaanisha ni kumnyanyasa mtu na kumdhulumu kwa kila namna. Kadhalika, amelitumia kimajazi kudhihirisha kazi yake ili aweze kufanikisha malengo aliyokusudia.

Uchuna katika kilele chake ukakiuka haki za mahitaji ya kimsingi kwa binadamu. Anasema si lazima kila mtu ale ashibe. Kula kwategemea bahati ya mung utu. Kazi ni bahati na sibu wala si ya kuadhimisha ubinadamu. Nyumba si kwa wote bali kwa wale walio na bahati kuzinunua. Kwa hivyo, Wachuna waliweka sheria ngumungumu ili kujinufaisha wao wenyewe.

Tambo ya moto ilihusu ufundi, uhandisi na teknolojia. Aidha, utawala wao ulikita nyoyoni na akilini mwa waja wao walipotumia mafiga ya ulafi, ujinga na uongo. Baada ya muda mrefu wa watawaliwa na kunyanyaswa hivi, watu walierevuka wakauona unyama waliokuwa wakitendewa. Mtunzi kwa kutumia kisasili cha moto aliwaerevusha wenyeji. Kwa kutumia silaha zile zile zilizowanyanyasa wakapata ujasiri, ukinaifu na ufahamu. Umma ukashuka na kufanya mapenduzi yaliyowakandamiza ili kuonyesha mwanzo mpya katika maisha yao. Haya ndiyo mtunzi alidhamiria kufanikisha katika riwaya ya *Walenisi (1995).* Alidhamiria kutuonyesha jamii yenye utu na usawa unavyoweza kuumbwa.Kupitia kisasili hiki mwandishi anatoa dhamira ya riwaya kubainisha ujenzi wa jamii mpya.

Kisasili cha moto kinatusawiria Wachuna kama watu wabaya kutoka ulaya, wakatili na vitendo vyao ni viharibifu, wanyanyasaji, walafi na wenye utabaka wa kimwinyi. Kisa hiki kimeingiliana

kimatini katika kukabiliana na udhalimu vilivyo kwa njia zozote ziwezekanazo. Shabaha yake Mkangi ikiwa ni kujenga ulimwengu mpya (uk 195).

Mwandishi wa riwaya hii ameathiriwa na kazi ya Shaaban Robert (1951) hasa kwa upande wa matukio ya kusimulia wajumbe waliotumiwa katika nchi tofauti. Yaliyotokea kisadfa kama vile uvumbuzi wa moto ni matukio ya kihistoria yaliyotokea miaka milioni moja iliyopita wakati jamii ziliishi kwa kutegemea nguvu zao za kuwinda na kujikinga dhidi ya mazingira makali. Haya ni mabadiliko katika maisha ya binadamu kufanya maisha kuwa bora.

Kutokana na mabadiliko, wenyeji sasa wanakua wakijikinga dhidi ya wanyama wakali wa mwituni. Licha ya hayo, kundi la mabwanyenye na mabepari wamewaingilia. Wanajamii bila kujua wamepoteza ile haki yao ya ujima na wakajipata wanalipa kodi na kutoa vipeto vya vyakula kwa matumizi ya moto.

### 2.3.2 Kisa cha Mchawi

Kisasili cha pili kilichozua Wachuna wa ukoo wa uganga kilitokana na mtu mmoja aliyejulikana kwa jina la Mchawi. Tunaelezwa kuwa Wachuna waliweza kueneza uchuna baada ya kumiliki tambo la uchawi kutoka kwa Mchawi. Tambo la uchawi lilihusika na uganga, dini na sayansi.

Siku moja, Mchawi akiwa kichakani amechutama aliweza kuona mambo ambayo yangemgeuzia maisha yake na jamii kwa jumla. Mahali pale palikuwa pazuri kwa sababu ya kivuli cha kupumzikia. Miti midogo na mikubwa ilikuwa imeshikamana kufanya hapo chini kuwa bila nyasi. Ghafla alisikia “chakarachakara”..

Aliona majoka mawili yakipindana. Hakujua kwa nini walikuwa wakizozana. Kutisha kwa kioja hiki kukamfanya kutulia tuli na kukazia macho yake kwa hayo majoka. Hizo pingilipingili zao zilizidi kupindana, na kwa ghafla yakaanguka pale karibu alipokuwa.

Pingilipingili hizi zilikuwa ni vita vya kumalizana kati ya bafe na chatu. Chatu alimuuwa bafe lakini akawa hajiwezi kwa sumu nyingi. Alijivuta akachimba mizizi ya mti fulani na kubambua maganda yake na kutafuna halafu akapona.

Mchawi baada ya kuhakikisha kuwa chatu ametoweka alifyatuka kwa haraka kuchimba mizizi kupambua magamba na kuchunia majani yake. Vyote hivi akavitia bindoni na kuelekea kwake.

Kabla ya siku hii mtu yeyote aliyeumwa na nyoka, lake lililobaki ni kuandika wosia wake.

Ilikuwa ni kawaida wenzake wakimjia na kumpa pole kama njia ya kumpa kwaheri.

Haikupita siku nyingi jirani ya Mchawi akaumwa na bafe, lililobaki ni kuandika wosia ili asiache vurugu baada ya kifo chake. Huku watu wakijiandaa kuomboleza, Mchawi aliingia akibeba mizizi, magamba na majani. Aliyasaga unga na yale majani akayaingiza ndani ya chungu cha maji na kuyavuruga vuo.

Baada ya matayarisho haya akamnywesha, muda usiokuwa mrefu mgonjwa akapata nafuu. Kisa hiki kikaenea kwa marefu na mapana. Watu wakamiminika kwake kumletea wagonjwa walioumwa na nyoka.

Mchawi kuona hivyo naye akatumia mizizi na maganda hayo kutibia watu walioumwa na nyoka. Baadaye, akaeneza utabibu wake kujumlisha kila aina ya ugonjwa. Watu wakampa vyakula ili asiende shambani. Ziada zikarundikana na akawa tajiri na kupata utukufu pamoja na familia yake.

Kama Moto naye pia akawaambia watu kuwa hangeweza kuendelea na kutoa huduma za matibabu kwa kuwa ilimbidi naye pia aende kwake makondeni. Alianza kutoa tisho lake. Watu walimwambia watamlisha. Utajiri huo ukamtia hisia za kifalme, utukufu na mjua yote. Kama

Moto akarithisha watoto wake wa kiume tu siri hii. Aliwalisha kiapo ili wasitoe kwa mtu ama ukoo mwingine asilani.

Hiki ni kisasili kingine kinachohusu mtu kwa jina Mchawi ambaye anavumbua dawa ya kutibu sumu ya nyoka kutokana na vita kati ya bafe na chatu. Kisasili hiki kimeingiana kimaandishi katika kuelezea hali hii inayomfanya ainusuru jamii yake ambayo ilikuwa inapoteza watu wengi kutokana na sumu ya nyoka.

Mchawi alionekana akiingia kumganga mtu (uk160-161). Alama ya nyoka ni taswira kuonyesha magonjwa tofauti kwa sababu nyoka huwa na sumu tofauti kutegemea aina ya nyoka na pia mahali ambapo anapatikana. Sumu tofauti huonyesha magonjwa tofauti. Jinsi nyoka walivyo wengi na tofauti ndivyo magonjwa hayo yalivyo.

Uvumbuzi huu wa madawa umeleta uponyaji kwa wengi. Kabla ya uvumbuzi huo, watu walikuwa wanakufa ovyo ovyo. Ukiumwa na nyoka, wanajamaa hawakuwa na matumaini bali tayari walikuwa wanaandaa mazishi. Mwandishi ametumia kisasili hiki kuonyesha umuhimu wa kugundua mambo mapya ambayo yanakuwa ya manufaa katika jamii.

Tukimrejelea historia ya Walter Rodney (1989;26) anasema watoto wengi wa kiafrika hufa kabla ya kufikia miaka mitano. Ukosefu wa madaktari ndio hurudisha nyuma juhudi za kupambana na maradhi. Mchawi aliweza kuridhisha ujuzi huu kwa wavulana pekee yake, kazi ya ufundi kwa watu fulani. Hii ni dalili kwamba taaluma ya udaktari hulindwa sana. Wachache walihitimu kutoka vyuo vikuu. Baada ya kuacha kazi ya kondeni, Mchawi aliletewa vyakula vya ziada. Mchawi akaanza kunyonya jamii na kujitwika mamlaka makubwa makubwa. Mwishowe akawa mfalme aliyeheshimika katika jamii. Mkangi alituchorea utabaka ulioshuka kupitia kwa Mchawi. mwandishi anashtumu utabaka na kusisitiza hali ya ujamaa ambapo hakutakuwa na utabaka.

Anadhihirisha kisasili cha Mchawi kuhimiza wanajamii washirikiane kwa niaba ya jamii nzima kubadilisha maisha yao. Anadhihirisha maisha yaliyo na usawa.

### 2.3.3 Kisa cha Mabavu

Mabavu alikuwa mwindaji hodari na shujaa wa kupambana na wanyama wakali. Mabavu, sifa zake zilienea kama moto katika nyika wakati wa kipupwe. Msasi huyu alimpenda msichana kwa jina Kadzo.

Kadzo alikuwa kipenzi na tunu ya jamii. Uzuri wa Kadzo ulijulikana kila pembe za kijiji. Umbo la Kadzo liliwateka wengi. Mabavu alikuwa kila mara haachi kumkonyezea jicho alipomwona lakini Kadzo hakumpenda bali alimpenda kijana aliyeitwa Dutu. Hili halikumpendeza Mabavu mpaka siku moja akataka kujua kwa nini yeye ni shujaa lakini Kadzo hakumpenda. Kadzo alimweleza kuwa Dutu alimpa nyama ya ulimi. Mabavu kwa kutojua maana ya nyama ya ulimi aliingia msituni na kuwinda wanyama ili kumletea Kadzo ndimi. Mabavu anasema,” Haya shika, nini zaidi wataka?” akamwuliza kwa sauti ya ushindi. Kadzo alimweleza Mabavu maana ya nyama ya ulimi.

Katika usiku wa manane kijiji kilishambuliwa na simba ambaye aliwahepa mashujaa wa kijiji waliokuwa wanamwinda. Ghafla bin vuu wakasikia kiambaza kimevunjwa na Kadzo akipiga mayowe. Alikuwa amenyakuliwa na simba. Mashujaa wa kijiji hawakuweza kumwokoa Kadzo ambaye alikuwa lulu ya jamii. Mabavu alisema kwamba wamwambie Dutu aende akamuue huyo simba. Umma haukujua mzaha huu wa Dutu lakini wazazi wa Kadzo walimwendea kwa unyenyekevu na kumwelezea ikiwa Kadzo angepatikana uhai basi angeozwa awe mkewe Mabavu. Ahadi hii ilimtoa Mabavu chapuchapu hadi mlimani alikomwandama simba. Aliweza kumuua na kumchukua Kadzo akiwa mzima.

Hapo ikawa Kadzo ameokolewa kutoka kwa kinywa cha simba. Kadzo akaishia kuolewa na Mabavu, mwandishi anasema kwamba alizidi kutumia ujanja huohuo kujipatia wasichana warembo wote. Kwa hofu, watu hawakukosa kumjia wakitafuta ulinzi (uk 165).

Mabavu sasa alikataa kwenda mawindoni. Alihitaji watu wamletee chakula kama fidia ya ulinzi atakayotoa. Alitunga sheria na watu wakalazimika kuitikia. Ulaghai huu ukazidi kuendelea na kukakosa mtu jasiri wa kumpinga. Kwa hivyo, akaendelea kujijenga na kupata ufahari wa chapa ya ‘simba’ kama kitambulisho cha utawa wa nasaba.

Kisa hiki kilirejelea ukoo mmoja wa Wachuna. Wachuna ni istiara ya wageni hasa waliotawala bara la Afrika. Tuki (2006) anasema istiara ni tamathali ya usemi yenye maana ya kukihusisha kitu kimoja na kingine kwenye sifa zilizofanana. Mwandishi ametumia mbinu hii ya fasihi simulizi (istiara) katika fasihi andishi. Wachuna ni istiara ya wageni hasa waliotawala bara la Afrika. Pili ni majazi lililotokana na kitendo kuchuna yaani kutoa ngozi mnyama. Majazi ni mbinu nyingine ya fasihi simulizi katika fasihi andishi. Majazi ni sifa ya kuwapa wahusika majina ambayo yametoa sifa zao. Katika muktadha wa dhamira ya maandishi iliweza kutafsiriwa kama kuvua hadhi, mali na heba na kumwacha mtu bila stara. Hivyo ni kumfukarisha mtu na kumnyima utu. Wachuna wadhalilisha, wakawabagua, kunyanyasa na kuwadhulumu watu kwa kila namna.

Kwanza kabisa ‘Mabavu’ ni jina la kimajazi lenye maana, kutumia nguvu. Jina la “Mabavu” lilitumika kimajazi kumpa mhusika jina ambalo linatoa sifa lake. “Mabavu” lilishirikiana na fasihi andishi kueleza nguvu ya kutoa ulinzi kwa wanyonge. Kuna kabila la mabwenyenye na umwinyi kwa utawala wao wa nguvu, wachache wanamiliki mali nyingi na wengine wanakula

taabu. Kisasili hiki kinaning'inia juu ya mfumo wa uzalishaji mali. Majazi aliletewa mali hasa vyakula ili aweze kutoa ulinzi kwa wahusika.

Kuna siasa za kijamaa kama siasa mwafaka kwa nchi zilizotaka kupiga hatua kimaendeleo na siasa za kimabavu. Wachuna walionekana kuwa watu wabaya kutoka ulaya.Wana vitendo vya ukatili. Waliharibu mali kwa kufyeka misitu na kunyanyasa wenyeji mashamba yao.

Kuna mwingilianomatini wa kimabavu na matabaka ya kimwinyi. Huu ni mwingiliano wa kihistoria. Wachuna walitawala nchi kimabavu. Utawala huu wa Wachuna ulilinganishwa na utawala wa kikoloni ambao ulileta athari kubwa Afrika hasa ulisababisha uigaji wa mila, utamaduni, desturi na lugha za watawala huku watu wakidhania kuwa huo ndio ustaarabu.

Chapa ya simba ni taswira kuonyesha bendera ya Waingereza ambapo bendera yao 'The Union Jack' ina ishara ya simba. Pia inaweza kuwa taswira ya nchi za kigeni zilizogawana na kutawala nchi mbalimbali za bara la afrika lililojulikana kwa kuwa na malighafi yake tele. Malighafi hii inamezewa mate na akina Mabavu, mataifa ya kigeni na akina Dutu ni mataifa maskini ya bara ya Afrika. Maskini wa Afrika walipewa maneno matamu ya uongo mtupu. Kumbe waswahili hawakukosea waliposema 'maneno matamu humtoa nyoka pangoni'. Mwishowe mwafrika maskini alikubali na kunyang'anywa mali yake yote. Waliwekwa chini ya utawala wa mabepari. Mwishowe walianza kuwahudumia kwa kufanya kazi ngumu ili waweze kuwalisha na kuwatajirisha. Bila kujua wakawa watumwa katika nchi yao yenye rotuba nzuri. Mabwenyenye pamoja na jamii zao walikaa kujiburudisha bila kufanya chochote. Mali yao yote waliyarundika kwa tabaka hili la matajiri.

Msichana Kadzo ambaye anamezewa mate ni nchi ya Afrika pamoja na malighafi yake. Nchi iliyo na rotuba nzuri ya kutamanika na kila mtu hasa nchi za kigeni zilizo na nguvu za kimabavu.

Walipochukua sehemu fulani walienea kama moto msituni na kutawala kila mahali. Wenyeji wasio na uwezo waliangalia bila lolote. Mabavu aliletewa mali hasa vyakula ili aweze kutoa ulinzi kwa wahusika. Jambo hili linatupeleka kwa mifumo ya ukabaila, ubwenyenye na umwinyi. Watu wachache wanamiliki mali nyingi, na wengi wanakula taabu.

## 2.4 Kubainisha Visasili katika riwaya ya *Mafuta (1984)*

Katika riwaya ya *Mafuta (1984)* kuna matukio ya visasili tofauti yaliyojikita katika hadithi moja kuu. Hadithi hizi zina ujumla wa muungano wa matukio mbalimbali yajengayo tukio moja muhimu ambayo huelezwa kwa muda mfupi. Mkangi amebainisha visasili muhimu kama vile kisasili cha matope, kisasili cha mafuta na kisasili cha mama Fofi. Kulingana na usomaji na uchanganuzi wa riwaya ya *Mafuta (1984),* mtafiti alitambua visa vifuatavyo;

### 2.4.1 Kisasili cha Mafuta

Hadithi ya mswada uliopatikana ndani ya koti la mhusika Jali ndilo lilianzisha hadithi ya mafuta. Wahusika hawa wawili, Mtue na Msali wanajadili juu ya dhana ya mafuta na kitanda. Baada ya majadiliano yao hawafiki kwenye jibu la kukilalia kitanda kwani hawana uwezo wa kuyapata mafuta.

Kitanda hiki kina wenyewe ambao wanakilalia. Kuna wengi ambao wanatamani kukilalia lakini hawana uwezo huo. Mtu yeyote anayekilalia kitanda lazima awe mteule. Mafuta ndiyo nguzo, ndiyo kata itenganishayo. Kama uwezo wako wa kuyapata ni haba huwezi kuyapata. Ukweli ni kwamba inamlazimu mtu kuwa amepakwa mafuta kwanza kabla ya kukilalia kitanda.

Uteule huu wa mafuta uliwatatiza wengi kwa sababu kitanda chafaa kulaliwa na yule alikihitaji. Usingizi na uchovu hauna simile, vimkumbapo mtu hana budi ila kujitupa kitandani. Katika hali

hii aliye na mafuta hana budi kwa kuwa hii ni sheria ya maumbile hata kama usingizi ni usingizi na si kwa mtu mnyama au mdudu.

Mazingira ya wateule yalitandazwa kwenye uwanja mkubwa sana. Halaiki ya watu wenye sura za furaha. Wote walikuwa wakimeremeta kwa mafuta waliyojipaka. Kila mahali walikuwa wanakaa vikundi vikundi, vitambi na vishavu vilivyonang'anika kwa sababu ya mafuta. Wana mazungumzo ya faragha na ya utaratibu sana. Ni mahali hapana kelele kamwe. Ni mahali patulivu. Ni pahali palikuwa pamejitenga kiasi. Waliokuwa wanaishi hapo walikuwa na raha na furaha isiyoelezeka.

Walikuwa wanametameta kama jongoo. Mashavu yao yalikuwa makubwa na ya kuvimba. Tumbo kubwa la kudondoka na la kufura kana kwamba alikuwa anabeba mimba nne! Kizingiti cha shingo kilichopakata kichwa cha kusagika utosini namna ya kiwanja cha ndege! Macho meupe yaliyokuwa yaking'ara mfano wa bundi yalikuwa yakishindika kwao kikomoni.

Wateule peke yao waliruhusiwa kucheka. Asiye mteule kucheka ilikuwa inaonekana kana kwamba wamewapokonya madaraka watu hawa. Ti na Mtue walipojiunga na vicheko vya wateule, Ti anaachiliwa, naye Mtue anahukumiwa kunyongwa. Inaonekana kwamba Ti ni mzaliwa katika tabaka la wateule, lakini hakumbuki masharti ya wateule kama vile kutoruhusiwa kucheka.

Mtu akitaka kuwa mteule sharti atimize mambo fulani kama vile makafara, miiko na mazingaombwe. Kadhalika, kuwa mteule ulikuwa unakula kiapo kutotoa siri yao. Kufichua ukweli kulisababisha mtu kuadhibiwa.

Mandhari ya kitanda. Kitanda kilielea juu ya mti uliofanana mbuyu na Mtue aliambiwa alale chini ya kivuli cha kitanda hicho (uk85). Hapa ndipo ukweli wa uongo ulifafanuliwa. Walieleza

kwamba hakuna mteule yeyote hawezi kukilalia kitanda na kwamba mteule yeyote hawezi kukiri upumbavu wake. Hii ndio sababu walificha ukweli kwamba hawajakilalia kwa kusema kuwa wamekilalia.

Wateule walikiri uwongo. Uwongo huu ndio ulidumisha maslahi yao. Yasemekana kuwa kuna aina saba ya mafuta lakini ukweli ni kwamba kuna aina moja iliyotiwa kwenye vyungu na kupewa majina tofauti lakini yote ni ya aina moja. Asili ya mafuta ni mkojo wa paka. Haya yote hayana maana lakini kwa mteule yalipewa umuhimu. Lakini mwisho tutaona kitanda kikining'inia kikielekea kuanguka.

Tabaka hili lilihakikisha kuwa hata makombo na masazo ya chakula hayakuwafaidi wanyonge kwani walihakikisha waliajiri askari wa kuyalinda. Zaidi ya hayo, makombo hayo yalinunuliwa na matajiri kwenda kuwalisha nguruwe wao. Inaonekana walifurahia unyonge wa tabaka maskini. Walicheka walipomwona matope karibu kula chakula kilichotiwa sumu ya panya. Walionekana kufurahia mateso ya matope.

Mahakama ni taasisi ya wateule na ilitumiwa kuwaogofya wanyonge. Mtunzi alituambia ni mahakama ya uongo ukijidhihirisha ukweli ulijitenga (uk 21). Hata hivyo wana msimamo kwamba asemaye ukweli lazima anyamazishwe.

Maji na mafuta hayaendi pamoja. Hizi ni itikadi mbili tofauti. Yeyote aliyenajisi mafuta alihukumiwa kifo kwa kuyanajisi mafuta ya mama Fofi kwa maji. Wao walikuwa wakitumia kicheko cha kutisha na kuogofya wanyonge. Hivi vyote ni vitisho vya kulinda utabaka wao. Nguzo za tabaka hili ni kusema uongo. Hata hivyo uongo haudumu na mwisho kitanda kitaporomoshwa.

Katika hadithi ya mafuta, mwandishi anadhamiria kuwaletea wanyonge ukweli kama silaha yao ya kujikomboa katika utumwani wanaofungwa na uongo wa kujipaka mafuta na kukilalia kitanda. Wateule wana itikadi ya mafuta nao wachochole wana itikadi ya maji. Sheria zimeundwa kuyalinda maslahi ya wenye nguvu za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mkangi anadhamiria kuwafungua macho tabaka la wachochole ili waweze kujinasua kutoka kwa hizi sheria za wateule.

### 2.4.2 Kisasili cha Matope

Kisasili cha pili ni cha matope. Matope ni mhusika ama raia aliyeishi katika kidimbwi cha matope. Ametumika kuonyesha uhasama ulio katika mahakama. Alitumiwa kuwaosha wateule kwa maji. Hii ilikuwa siri ya njama kuwaondoa katika uteule.

Chanzo cha matope kulala matopeni ni vile hakuwa na mafuta.kwa hivyo kisa hiki kinaelezea chanzo cha kulala matopeni. Matope yanadhohofisha afya ya wanamatopeni. Matope yanasimamia tabaka la chini, tabaka la wanyonge lile linalonyanyaswa. Hawa ni wanyonge wa kisiasa na kiuchumi. Hawana ruhusa ya kukula hata makombo ya chakula.

Tabaka la matope linaamini maji kama chanzo cha uhai. Tabaka la wachochole lakini wakakamavu kwani linajiamini na lina matumaini na ushirikiano. Matope yanafanya hata vijana kuonekana wazee. Tabaka hili la matope halina ruhusa hata ya kucheka kwani wanawekewa vitisho ili kuogopa ndio wasilalamike. Wanakula chakula cha mapipani ingawa chaweza kudhuru lakini hawana budi.

Watu wa matopeni hawana namna ya kujistarehesha katika majumba ya starehe bali wao huishikilia kutupiana nguvu tu. Hili ni tabaka linalojumuiana na walio wengi. Hawana kazi ya kufanya. Hali yao ya kulala ni matopeni inabainisha kukata tamaa kukosa matumaini.

Wana matope kupitia kwa mhusika matope tunafahamishwa maisha ya tabaka la matopeni. Kwa mfano kuwania mabaki ya chakula ambacho mbwa, kuku na paka walikikataa. Walingángánia makombo hayo wakibishana na panya na komba mwiko (uk 38). Mtunzi anatuchorea uvundo wa mapipa.

(uk 40) hali ya mnyonge ni kukata tamaa kwa wanamatopeni kunadhihirika. Matope anafikiri kula chakula kilichowekwa sumu ili asifilie mbali maana hana maana yeyote. Lakini hata hivyo, matope ameanza kuona udanganyifu wa wateule anaposema,"mmefanya uwongo ukawa ukweli na ukweli uwongo, unyama wenu ndio utu na utu wenu ndio unyama" (uk48). Matope anabainisha kuwa maji ndio uhai na wala si mafuta na maji yatawasomba.

Kuna mwingilianomatini wa fasihi simulizi katika fasihi andishi la wachochole na kudhalilishwa na tabaka teule. Hili ni tabaka la chini, wanyonge maskini hohehahe. Hawakuwa na chakula bali walikula kutoka kwa mapipani kwa matope. Hata hawakuwa na mahali pa kulala, wanalala matopeni.

Wanyonge wana utu na waliheshimiana, kwa mfano kundi lililokutana kwa msati na watoto waliosoma mswada (uk 37-39), ulitupa taswira ya ulitima huu. Lugha ya uvundo, uchafu yenye kuleta hisia za kinyaa. Kwa mfano chakula cha matopeni ni kichafu na kingeweza kuwadhuru afya lakini walikuwa hawana budi kukila.

Akina Zuka walilazimika kuiba ili kunufaika na walingojea wapewe kwa ukarimu wa mwenye mkunazi, lakini huu si ukarimu wa haswa maana alihitaji ahudumiwe. Kwa hivyo mnyonge hakaribishwi kamwe. Jali alionyesha bidii katika kazi yake kama mkulima mdogo na alifahamu kuwa mahusiano ya kijamii hayamalizi mahitaji yake. Alipojaribu kuonja kunazi aliitwa mwizi

(uk 5) na umma ulijaribu kumvamia.Vita hivi ni kuwakilisha cha kutoelewana kwa wanyonge. Hawajui mwizi ni nani kwani walilaumiana wao wenyewe.

Tabaka la matopeni halina namna ya kujistarehesha katika majumba ya starehe bali wao hushikilia kutupiana ngano tu. Matope yalidhoofisha afya ya wanamatopeni. Umaskini, unyonge wa kisiasa na kiuchumi yalisimamia tabaka la chini.Tabaka la unyonge, lile lililonyanyaswa. Tabaka hili liliamini maji kama chanzo cha uhai. Ni tabaka la uchochole lakini wakakamavu kwani linajiamini na lina matumaini na ushirikiano. Matope yalifanya hata vijana kuonekana wazee.

Tabaka la wanyonge lilijumuisha walio wengi. Hawana kazi ya kufanya. Hali ya kulala matopeni ilibainishwa kukata tamaa. Kukosa matumaini. Lilihitaji umoja na ukweli ili kufikia ukombozi.

Mwandishi alitokeza mwingilianomatini wa fasihi simulizi katika fasihi andishi maudhui kati ya mapenduzi na ukombozi. Swala la mapenduzi lilijitokeza (uk 88). Haya ni mapenduzi yaliyokuja ghafla kiasi cha kwamba hayasadikiki kwa urahisi. Hatuoni maandalizi yoyote. Wateule kama vile mama Fofi na mama Shibe waliyaona mapenduzi kama mwisho wa dunia.Wataishije bila mazuri waliyoyaona?

Mwandishi alitoa taswira ya fasihi simulizi katika fasihi andishi. Hapa kuna mwingiliano wa maji na ukombozi. Taswira ya maji hapa ilionyesha kuwa maji ni ukombozi na huondoa uchafu. Maji yalitumika kijazanda kuonyesha kuwa kitu chochote chenye uhai lazima kilihitaji maji. Itikadi ya maji ina mashiko na haishindiki. Maji ni uhai na kwa hivyo iliendelea kupiganiwa. Mafuta ni itikadi isiyoweza kuwekwa katika mizani moja na maji kwani haina mashiko bali ni ya uongo. Kwa jumla mwingiliano huu wa *Mafuta* na maji mwishowe ulileta mapenduzi ambayo

matokeo yake ni ukombozi wa tabaka la chini. Kifungu hiki cha habari kuhusu asili ya mafuta kilileta furaha kwa tabaka la wachochole.

Kisa cha mhusika Matope na wale wote wanaolala matopeni kinadhamiria kuchochea hisia za kuleta ukombozi unaofungamana na maudhui nyinginezo zote. Ukombozi ni mabadiliko yanayodhamiriwa kuleta usawa. Katika riwaya, mapambano ya ukombozi yanafanywa. Baada ya ukombozi inatarajiwa kwamba haki itatawala na ukandamishaji, unyanyasaji na maonevu yote yataangaziwa huku watu wote wakifaidika.

### 2.4.3 Kisasili cha mama Fofi

Mama Fofi alihadithia wenzake kisa kuhusu mume wake. Marehemu mume wa Fofi alifanya juhudi kando na kuzaliwa katika mazingira ya ukame na hata jamii yao walikuwa maskini hohehahe. Ukame huo ulionekana ukienea jamii nzima na kuridhika katika ukame. Mume wake ndiye pekee yake aliyekuwa wa kwanza katika kujitoa katika hali hii ya kusikitisha.

Alizaliwa ngozini katika nyumba ya nyasi isiyo na madirisha. Mlango huo mmoja ndio kila kitu kuingilia na kutokea. Si watu si mifugo, si mbu si moshi, si kuku si nzi, si uvundo si marashi, si watoto si watu wazima.

Kutokea tumboni mwa mamake, mkunga akazika vyalio vyake pembeni humo nyumbani. Siku zake ilimbidi apitishwe. Kutokana na mila, mlangoni kuliwekwa uta, mshale, panga na jembe. Babuye somoye alimshika sikio na akamnyunyuzia dua la rehema huku akimkabidhi vifaa vya jukumu lake.

Babu yake alimwambia atokako na aendapo hapajui. Mtu kuzaliwa ukameni sio lazima afe papo hapo. Kwa kuvipokea vifaa vya kazi Sifa alianza kuchunga mbuzi na kondoo na marika wake walipokua wakikua.

Mwishowe alitiwa jandoni na utoto kuubwaga. Sherehe ambayo kina baba na kina mama walifurahia kwa vifijo na vigelegele. Ilikuwa ni harusi yao ambayo waliifikia kwa kisu kukata ngozi, damu kumwagika, meno kusagika na machozi kuyakausha. Hapo ndipo majukumu yalipoanza.

Kuenda kuwinda na kuleta nyama nyumbani ilikuwa sifa ya mwanaume. Alifuma wanyama wengi kisha bibi yake, mama Fofi. Posa, uchumba na ndoa ulitekelezwa kama desturi. Watoto walibarikiwa nao sita kwa ujumla. Hao watoto ndio waliowatia ari ya kutaka kujijenga.

Mwishowe kumbikumbi walivyoenea nchi mzima msimu wao uliposibu, walibahatika na wakapata vichuguu ambamo mchwa wenyewe walizaliana. Sifa alikuwa mmoja wao. Kwa bidii yake aliweza kujiingiza katika uteule wa kupewa kandarasi ya kukamata kumbikumbi baada ya kudondosha mbawa zao.

Shabaha ya mwandishi kupitia kisa hiki inadhihirisha juhudi alizonazo mama Fofi hadi kuingia tabaka la wateule. Kwa hakika yeye si mnyanyasaji, si mkandamishaji ijapokuwa hali yake ya kifedha ingemfanya kuwa hivyo.

Juhudi za Sifa mumewe mama Fofi ziliambulia patupu. Sifa, alitaka kuepuka ile hali ya kuzaliwa katika tabaka la chini na kufia katika tabaka hilo. Hata jamii nzima ilikuwa katika ulitima ulioridhishwa kutoka familia moja hadi nyingine. Hawakuwa na jinsi wangeweza kujitoa katika ulitima huu. Mama Fofi na mumewe walifanya jitihada katika kazi yao. Mwandishi anaonyesha matabaka kwa kusema, "…wako wale waliobahatika na wakapata vichuguu ambamo mchwa wenyewe walizaliana." Wao ilikuwa ni kulalia nundu tu basi. Pia kulikuwa wale ambao walipewa kandarasi ya kukamata kumbikumbi baada ya kudodosha mbawa zao. Hawa, chao

kilikuwa kidari. Nyama za mbavu zikawa zetu. Sisi tulipewa kandarasi ya kuzoa mbawa na kuziuza."

Kazi hii ilikuwa ngumu kwani mzoaji alihitajika kupigana na kudhibiti maumbile na mazingira ili apate chochote. Katika kufanya kazi hii, walipambana na vikwazo kama ndege, upepo unaopeperusha mbawa hizi na kuzitawanya kila pahali. Mvua na matope viliweza kuzorotesha kazi hii. Wazo hapa ni kuwa mwanadamu lazima apambane na mazingira magumu ili aweze kuyadhibiti. Lakini huwa ni vigumu wakati ambapo wanadamu wengine huwa vikwamizo kwa mfano wanapomiliki nyenzo za uzalishaji mali.Mwandishi anadhamiria kuwashauri wanyonge kuwa ukombozi hauji tu hivyo bali ni bidii yao itakayoweza kuwakomboa.

Mwandishi anawashauri wanyonge wawache kujidharau bali wajikomboe kimawazo na waweze kujitegemea kama mama Fofi ili wajinasue kwa juhudi na bidii zao. Nia yake Mkangi ni kuunda jamii mpya iliyo na usawa na kupiga hatua kimaendeleo.

## 2.5 Hitimisho

Sehemu hii iliongozwa na swali la kubainisha ikiwa visasili vilitumika katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Shabaha ya kwanza ilikuwa ni kubainisha visasili katika riwaya husika. Kulingana na usomaji na uchanganuzi, sehemu hii ilitambua visasili katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. *Walenisi (1995)* kuna kisasili kwa jina Moto, Kisasili kinachoitwa Mabavu na kisasili cha Mchawi. Katika riwaya ya *Mafuta (1984)*, mtunzi ametumia visasili. Mtunzi anaelezea asili ya mafuta, asili ya matope na kisasili cha mama Fofi akiwa katika mazingira ya ukame.

Wataalamu mbalimbali walitoa maelezo tofautitofauti katika kuelezea maana ya visasili. Kulingana na maoni yao kwa jumla, visasili ni visa ambavyo vinaeleza kuhusu chanzo cha suala fulani kama Imani, dini, utamaduni na mengine. Pia visasili katika uamilifu wake vilionyesha kuwa na majukumu muhimu katika jamii.

# SURA YA TATU: VISASILI KATIKA KUTOA MAUDHUI NA DHAMIRA

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inadhihirisha jinsi visasili vinavyoweza kutumiwa na mtunzi wa riwaya katika kutoa maudhui na dhamira. Mada ya mwingilianomatini kati ya visasili na fasihi andishi si ngeni katika fasihi simulizi na andishi ya Kiswahili. Visasili huingiliana na fasihi andishi katika kutoa maudhui; hivyo visasili husaidia katika kufahamu maudhui. Wasomaji hupata msisimko zaidi kunapotumika visasili ambavyo vimejaa burudani. Hili lafanya maudhui kueleweka kwa haraka zaidi. Kimani Njogu na Rocha Chimera (1999) wakimnukuu Roman Jackson wanaeleza kwamba fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida. Lugha inayodhihirisha zaidi katika visasili ni ya kinatharia, huburudisha zaidi wasomaji huku ikihadithia maudhui alionuia mtunzi wa riwaya teule. Ni katika muktadha huu ambapo utafiti huu umejikita.

Watunzi wengi wa riwaya ya Kiswahili wameandika mambo kadha kutegemea wakati katika historia na hali zao za kijamii na kisiasa. Visasili kama kigezo cha utanzu wa fasihi, umekuwa na uwezo mkubwa wa kumulikia maswala anuwai yamhusuyo binadamu na Mungu wake, mtagusano wake na mazingira anamoishi. Mathalani, maswala ya dini, dhuluma, ukoloni na ukoloni mamboleo, unyanyasaji, utabaka, ubaguzi na mengineo. Kwa hivyo utumizi wa visasili kama itakavyobainika humpa mtunzi wa riwaya wepesi wa kuakisi maswala haya yanayomhusu binadamu siku baada ya nyingine.

## 3.1 Visasili kudhihirisha maudhui katika riwaya ya *Walenisi (1995)*

Visasili ni hadithi za kale zenye kuwakilisha imani na mtazamo wa jamii inayohusu asili ya ulimwengu na mwendo wake-asili yao wenyewe na maana na shabaha ya maisha yao. Visasili kwa hivyo hutumiwa kuelezea asilia ya mambo yanayotokea katika jamii husika kama vile kifo, maafa, matendo, tabia, hali n.k. katika riwaya hii mwandishi anatutolea visasili kadhaa.

Mohammed (2002) katika Makala aliyowasilisha katika kongamano la kimataifa la CHAKITA lililoandaliwa na chuo kikuu cha Nairobi. Maoni ya Said ni kuwa riwaya mpya ya Kiswahili inazo sifa nyingi za mwingilianomatini na fasihi simulizi hata kuliko kazi za awali. Mwandishi Mkangi ametumia visasili katika riwaya hii. Visa hivi vimeingiliana katika kuelezea asili ya mambo. Mojawapo ni kuhusu asili ya moto. Anatueleza kuwa asili ya moto ilitokana na mwindaji aliyetega kulungu. Alijiwa na hamu ya kumtengenezea mpenzi wake shanga. Kisadfa alipokuwa akipekecha mti kutoboa mashimo, cheche za moto zililipuka. Aliweza kutumia moto kama ngazi ya kujipatia ubwana mkubwa na kujibatiza ukoo wa Tai.

Mwandishi akifafanua mwingiliano wa visasili katika andishi anaonyesha kuwa kuna uwezo wa mambo mawili kutokea kwa wakati mmoja. Kuna uwezo mambo haya kutokea sio tu msingi wa usawiri wao, bali pia katika kuelezea dhamira na maudhui pamoja na ujenzi wa msuko. Mambo haya kutokea kisadfa ni rahisi kufuatwa na yana uwezo wa kunata na kuibua hisia za huzuni au furaha kama zilivyotarajiwa. Ni kwa mujibu wa maelezo haya ndipo uchunguzi umefanywa.

Ngure (2003) anaelezea jinsi visasili kama neno linavyoelezea kufafanua maana kuwepo kwa vitu, uhusiano wa vitu au hali mbalimbali. Kwa hivyo, mtazamo huu unaingiliana kuchunguza hali ya mwanadamu na uwepo wake katika historia. Kadhalika, imeangazia uhusiano wake na vitu au hali mbalimbali katika mazingira anamoishi. Hali hii inatoa chemichemi ya mwingiliano wa mwanadamu na vitu vingine katika ulimwengu wake unaomzunguka na unaomwezesha kupata mawazo, fikira na dhana mbalimbali. Mambo mapya anayoingiana nayo yanaleta mabadiliko mageni ya kila siku. Yanaweza kuleta mwamko mpya kumwezesha kubadili mambo kutoka ya awali na kuingia enzi tofauti. Ni katika msingi wa mawazo haya ambapo utafiti umefafanua matumizi ya visasili katika kufanikisha maudhui uliokusudiwa.

Mtunzi anapoeleza yale yanayohusu jamii yake, mwingiliano lazima uwiane na maisha na utamaduni wa jamii hiyo. Kutokana na mabadiliko ya mazingira na maendeleo ya jamii. Kwa ujumla mwandishi huwajibika kutumia dhana ngeni kutokana na vitabu, magazeti, redio, majarida, simu na sinema ili kusawiri vyema maswali ya kijamiii. Visasili havina uhuru wa kutumia msamiati huo mpya kiingilianomatini bila hata kutafsiri.

Lugha andishi na mwingilianomatini katika matumizi yake hujitokeza bayana kutegemea mwandishi mwenyewe, jamii yake na utamaduni wake, lugha ya kidhana, kimaumbo, dhamira na lengo la kazi yake, aina ya uwanja wa matumizi, hadhira lengwa na jinsi ya kuiwasilisha.

Mwandishi mkangi ameteua mwingilianomatini wa visasili kwa ujuzi mkubwa katika riwaya ya *Walenisi (1995)* na *Mafuta (1984).* Mwandishi kwa kawaida anapoandika huweza kubagua kwa makini maana na vivuli vidogovidogo vya maana vinavyoingiana katika riwaya. Katika riwaya ya *Walenisi (1995)* kwa mfano, mwandishi wa visa ili kubainisha maana na kupata ziada ya vivuli vya maana kusisitiza maudhui.

Kuna baadhi ya vipengele vya mwingilianomatini vinavyotumika sana katika uandishi wa riwaya kama vile nyimbo, jazanda, majazi, mafumbo, misemo na vinginevyo. Hapo ndipo watunzi wa riwaya hufanya hivyo ili kutoa msisimko shupavu kama utangulizi wa riwaya zao, hivyo kuchangia maendeleo ya riwaya.

Riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)* zimefuata muundo wa kuwepo mwingiliano unaofuata mtindo wa visasili. Aidha, riwaya hizi zina mianzo na vimalizio vya visasili kwa njia ya mafumbo hasa riwaya ya *Mafuta (1984).* Riwaya hii imeandikwa kwa njia ya kimafumbo ambayo imeingiana na maandishi ya mtunzi katika kutoa maudhui yake. Visasili kama vitakavyodhihirishwa vimetumiwa kuendeleza riwaya hizi.

Aidha, visasili vina uhuru wa kutumia lugha katika kuingiliana kimaandishi kwa madhumuni maalumu. Visasili havimfungi msanii katika utumizi wa misamiati, sarufi na hata kutumia vipengele vingine vinavyoingiliana bali vinampa uhuru wa kuboronga mwingilianomatini kwa mahitaji yake ya kisanii ili kubadili viingiano na hata kutoa vipengele hivyo ili kumulika maswala ya kijamii kwa weledi zaidi. Msanii huhitaji kutumia vipengele vya mwingilianomatini kwa mujibu wa wakati. Mitindo hii ya visasili humpa mtunzi uwezo mpana wa kuyashughulikia maswala mbalimbali ya jamii.

Kando na misemo, jazanda, mafumbo na vipengele vingine katika riwaya hizi kuibua hisia za wasomaji, zinasisitiza na zinasaidia kuelezea maana kimaudhui. Waandishi hutumia visasili katika mkazo wa maudhui aliokusudia mathalan kisa cha Mabavu katika *Walenisi (1995)* na katika *Mafuta (1995).*

Kwa mujibu wa Matteru (1983:27), fasihi simulizi ni utanzu wa fasihi unaotumia mdomo katika kuumbua na kuwasilishwa kwa wasikilizaji. Visasili vikiwa mojawapo ya vipengele vya fasihi simulizi pia huwasilishwa kwa njia ya mdomo. Hata hivyo, visasili hutiwa naksi na fani zaidi za mwingilianomatini ili kukuza maudhui, kuzua hisia na kutimiza malengo ya mwandishi. Baadhi ya mwingiliano wa fani za visasili zilizotumika katika *Mafuta (1984*) na *Walenisi (1995)* zimetumika kufanikisha usawiri wa maudhui na dhamira.

Visasili ni sanaa moja ambayo hutumia mwingilianomatini kwa ufaafu mkubwa vikilinganishwa na tanzu nyingine kwa sababu ya uhuru wake mkubwa wa kutumia mwingilianomatini. Humsaidia mtunzi kusema aliyoyataka kuyasema kwa njia inayoacha athari kwenye sikio la msikilizaji, fikira na moyo wa msomaji. Mbinu hizi zinaelekea kuwa na msisitizo zaidi kwenye visasili kutokana na utanzu wenyewe. Mbinu zenyewe ni kama tashbihi, kejeli, kinzani, jazanda,

taswira, tashhisi, semi, methali na kadhalika. Zote hizi huwa na lengo la kushadidia maudhui katika riwaya. Ingawa mbinu hizi ni nyingi, jambo la muhimu si kuzitambua tu, bali ni kuonyesha mchango muhimu katika utungo unaohusika. Jinsi utumizi wake ulivyofanikisha uwasilishaji wa dhamira ya mwandishi kikamilifu.

Kutokana na maelezo hapo juu, sura hii ina lengo la kudhihirisha jinsi visasili vilivyotumika na mtunzi wa riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)* kutoa maudhui na kuonyesha kuwa visasili ni mojawapo ya mbinu muhimu zinazoweza kutumiwa na watunzi wa riwaya ili kukuza mwingilianomatini. Aidha sura hii itaonyesha matumizi ya visasili katika riwaya hizi na jinsi vilivyochangia usawiri wa maudhui na dhamira.

### 3.1.1 Maudhui ya Dhuluma

Maudhui makuu katika *Walenisi (1995)* ni dhuluma kwa wanyonge katika jamii zetu za kiasili za kiafrika. Mwandishi anaongozwa na dhuluma za kiuchumi, kisiasa, kisheria na kijamii. Wanawake kwa wanaume wanadhulumiwa. Anaangazia kwa kina kisasili cha moto uliozuka kisadfa tu kuangazia ukoo mmoja wa Wachuna uliozuka na kuweza kujipatia utukufu, uwezo na hekima kwa kutumia hila zilizoweza kuwapa utawala juu ya wenzao na kula jasho lao. Mwandishi ametumia ujuzi wake wa mwingilianomatini ya istiara kusawiri maudhui. Wachuna ni istiara ya wageni hasa waliotawala bara la Afrika. Pili amelitumia kimajazi kutokana na kitendo cha kuchuna, yaani kutoa ngozi mnyama. Kwa muktadha wa dhamira ya mwandishi inaweza kutafsiriwa kama kuvua hadhi, mali na heba na kumwacha mtu bila stara. Wanawafukarisha na kuwanyima utu na kuwadhulumu zaidi. Waliwatia woga na hofu na kutumia hali hiyo kujirundikia mali ya ziada.

Wachuna walitunga sheria ngumu zilizowalinda na wakaitumia njaa na shibe kama silaha. Matokeo yakawa ni makundi mawili mlaji na mliwa, wenye akili na wenye tani, tajiri na maskini na waishio mashambani na waishio mjini. Katika hali hii, Wachuna ndio walipata hali zote bora. Walipata nafasi kubwa ya kuwadhulumu wasiojiweza.

Mkangi ametumia istiara, majazi na visasili kimseto katika riwaya ya walenisi kwa madhumuni ya kukuza dhamira ya ukombozi na kama mbinu ya kuleta pamoja umma. Kama inavyodhihirika, maskini wanadhulumiwa lakini mwishowe wanapata kuelewa na kudai haki zao. Mwandishi anakiri kila mtu awajibike katika kudai haki kwa pamoja. Wanajamii bila kujua wamepoteza ile haki ya ujima na wakajipata wanalipa vipeto vya kula kwa matumizi ya moto. Polepole wamekua watumwa. Yote haya ni dhihirisho ya dhuluma wanazofanyiwa, hivyo kuamsha ari ya kutaka kujikwamua kutoka kwa minyororo hii. Utunzi wa mbinu hii ya visasili ulifanikisha mno maudhui aliyolenga mtunzi wa riwaya hii.

Wachuna wametumia dini kudhulumu na kunyanyasa wengi na kunufaisha wachache. Dini kulingana na Wachuna inafundisha kuwa kuna watu wenye akili wanaostahili maisha bora kuliko wengine. Kwamba usawa unaohubiriwa utapatikana tu huko mbinguni. Kwa hivyo wale maskini wasiwaonee wivu wenzao kwani hiyo ni dhambi. Dini hii ndiyo iliyotumika kuwapumbaza watu ili wazidi kunyenyekea kwa watawala. Mkangi ametumia suala hilo la dini kuwaerevusha maskini kuwa ni porojo mtu kudai kuwa Mungu ndiye anamfanya mtu mmoja maskini na mwingine tajiri au mmoja kuwa mtumwa na mwingine bwana wake. Amewaeleza kuwa Mungu ni mapenzi na mapenzi ni usawa na usawa ni zao la ushirikiano.

Ni wazi kuwa Mkangi ameathiriwa na dini. Anajaribu kutuonyesha jinsi mbingu ipo humuhumu duniani. Tunachohitaji kufanya ni kubadilisha uhusiano kati ya mtu, mtu na nyenzo za uzalishaji

mali. Ubinafsi walio nao Wachuna ndio unaoifanya dunia iwe jehanamu. Wachuna wamefanikiwa kuibadilisha nchi kuwa yao. Wamenyayasa, wamejinufaisha na kuishi maisha bora. Usawa umetoweka. Wenyeji wanatendewa madhara, mateso, unyanyaaji na dhuluma za watawala madikteta.

### 3.1.2 Maudhui ya ukoloni mamboleo

Mazingira hasa yaliyomwathiri mtunzi katika kutunga kitabu hiki ni yale ya ukoloni mamboleo. *Walenisi (1995)* ni kitabu cha kisasa, cha wakati huu. Ni matatizo yetu sisi waafrika ni kutofahamu siasa, tamaduni na mbinu za kigeni. Ubarakala na udikteta umetawala nchi zetu za Afrika. Watu ambao wanatawala ni watu wanaotumia mbinu zao wenyewe ni watumwa.

Kisasili cha moto kinatutolea maudhui ya ukoloni na ukoloni mamboleo. Maswali haya yanajitokeza pale ambapo Mkangi anatusimulia habari za duniani na pia za Wachuna. Katika *Walenisi (1995)* tunaelezwa kwamba Wachuna ndio waliorithi ardhi na nyenzo zote za uzalishaji mali. Ilibidi umma uwatumikie kutokana na vitisho walivyopewa.

Ukoloni ulichangia pakubwa katika kuwagawa watu katika matabaka. Tunaelezwa kua Wachuna waliishi mijini na wengine mashambani (uk 168). Jamii ikajigawa na kuwa sehemu mbili: tajiri na maskini. Dunia ikakoma kuwa moja

Bwana Moto alikua kupe, kadhalika alijulikana kama ukoo wa “Tai”. Kama ulivyojulikana ni jazanda ya ukoo wa waamerika. Mwandishi ametumia kisasili hiki kudhihirisha mbinu mpya ya kisasa na jinsi makundi fulani yanavyonyanyaswa. Ametumia jazanda katika kuelezea hali duni na kudai mabadiliko.

Ardhi yote ilimilikiwa na wakoloni nao wananchi wakashurutishwa kuwalimia. Tamaduni, lugha, dini, sheria, desturi, mawazo, maendeleo na hata majina ya watawalia yalipuuzwa na

kuitwa ya kishenzi. Athari ya hii ni kwamba, watawaliwa waliacha mila zao na kuanza kuiga watawala wao kwa kila jambo wakifikiri huo ndio ustaarabu. Hili linaonekana hata leo pale ambapo watu wanapendelea kuzungumza lugha za kigeni kuliko zile zao. Wanaiga mitindo ya mavazi na desturi nyinginezo. Hili laonyesha kuwa watu hawa wametekwa akili. Aghalabu jazanda imetumika kwa sababu hutumia maneno machache kuelezea wazo kubwa katika kule kuingilianamatini kimaandishi. Hujenga picha maalum katika fikira za wasomaji. Utumizi wa maneno machache yanayoleta picha mahususi inayoenda sambamba na matendo katika riwaya ya *Walenisi* (1995). Mbinu hii ilitumika kuelezea dhamira ya mwandishi. Ni baada ya kugundua haya ndipo wenyeji wanafunga safari ya kiakili kutafuta suluhisho. Mkangi anawashauri kupata afueni katika mfumo wa kiuchumi wa kijamaa ulionawiri katika maisha yao. Haya ndiyo ambayo mwandishi alidhamiria.

### 3.1.3 Maudhui ya uvumbuzi

Maudhui ya uvumbuzi wa dawa. Hiki ni kisasili kinachohusu mchawi ambaye anavumbua dawa ya kutibu sumu ya nyoka kutokana na vita kati ya bafe na chatu. Hali hii ya uvumbuzi wa dawa ilitarajiwa kua ya manufaa kwa kila mtu katika jamii. Ni tukio lililoleta furaha katika muktadha wa walenisi. Raia wa kawaida walinyanyaswa na kudhulumiwa. Madaktari walijaa ufisadi na uroho hasa walipodai kiasi kikubwa cha pesa kwa kufanya upasuaji. Ufisadi ulidhihirika katika riwaya ya Mohammed Nyota ya Rehema (1976).

Alama ya nyoka ni taswira kuonyesha magonjwa tofauti kwa sababu nyoka hua na sumu tofauti kutegemea aina yake na mahali anapopatikana. Mwandishi ametumia taswira katika visasili kutoa picha ya mambo yatakayokuja mbeleni. Alitaka wadhulumiwa wafungue macho na kukiri hali ambayo wanaishi. Mkangi alidhamiria wao wawe na maono na kubadili hali ambayo walikua wanaishi. Kuna kunyanyaswa, kudhulumiwa na ufisadi.

Lengo la mwandishi lilikua wengi wawe na maisha mapya. Waishi katika hali ya usawa. Mchawi alimfuatilia chatu na kugundua matawi aliyotumia kujitibu. Hali hii ilimfanya ainusuru jamii yake ambayo ilikua inawapoteza watu wengi sana kutokana na sumu ya nyoka. Uvumbuzi huu ndio mwandishi anataka wadhulumiwa na wanyanyaswaji wavumbue. Wawe na maono maishani mwao. Wagundue taabu walizozipitia na baadaye wavumbue mbinu ya kujinasua.

Kulingana na mwandishi uvumbuzi ni jambo la maana kwa sababu unaleta tiba na ukombozi kutoka kwa minyororo ya udhuluma na unyanyasaji. Anadhamiria waondoe ujinga wafikirie juu ya maisha mapya yasiyo na taabu na yaliyo na usawa. Mchawi alileta ukombozi kwa watu wake. Alizuia kifo kutokana na kuumwa na nyoka. Hata naye alipona kwa kurundukiziwa ziada.

### 3.1.4 Nafasi ya mwanamke katika jamii.

Mchawi alirithisha ujuzi wa uvumbuzi wa dawa kwa wavulana pekee yake. Historia ya kukandamizwa na kunyanyaswa kwa mwanamke katika jamii ni ndefu. Nayo inarudi nyuma hadi wakati jamii ya binadamu ilipogawanyika katika matabaka mbalimbali. Mara nyingi, mwanamume ndiye aliyemiliki nyenzo za uzalishaji mali. Basi mwanamume aliwakilisha nguvu za kiuchumi wakati ambapo mwanamke alilazimika kumtegemea mumewe. Uhusiano huu ulizidi kuimarishwa na kukuzwa na taasisi za kijamii kama ndoa (uk 135-136).

Mambo haya ndiyo yaliyokuwa yakitendeka kule walenisi kwa Wachuna. Wao hawakumchukulia mwanamke kama binadamu bali kama chombo cha kumfariji mwanamume

Mwandishi Mkangi ametumia kisasili cha mchawi akidhamiria kutuonyesha jinsi mambo ni tofauti kule Walenisi. Mwanamke ni sawa na mwanamume. Uhusiano wa usawa kati ya vijana wa kike na wa kiume ulitawala. Mtunzi anaonyesha kwamba hakuna kazi ya mke au mume. Kazi ni kazi. Taaluma ya udaktari ililindwa sana. Ni wachache wahitimu kutoka vyuo vikuu baada ya

kuacha kazi kondeni. Wote vijana kwa wasichana huingia katika taaluma hii. Hili ndilo lilikuwa lengo la Mkangi katika suala hili la jinsia. Anahimiza jamii ambayo inadhamiria kuendelea isiwe na ubaguzi wa kijinsia. Wote wawe sawa katika jamii. Huko kwa wachuna, wasichana wanaendesha matingatinga na kuburuta mapipa ya mbolea, kutengeneza mifereji ya kunyunyuzia mimea na kadhalika. Waliheshimiana na kudhaminiana. Kwa hivyo, mwandishi anashutumu ubaguzi dhidi ya wanawake.

Misemo imetumiwa kuelezea maudhui kwa mfano "kukata choo" (uk 160). Mwandishi ametumia mtindo wa semi kusisitiza ujumbe. Semi zitumiwapo kiathari zina maana sawa. Mchawi alipokuwa anaenda haja kubwa, kwa mshtuko alikata choo kwa vita aliyoona kati ya bafe na chatu. Kama vile nilivyoeleza hapo awali, sumu tofauti huonyesha magonjwa tofauti yanayoshtua. Kuna magonjwa tofauti na hata ya kufunga choo. Mchawi ni daktari anayetibu magonjwa kwa kutumia miti ya kienyeji.

Semi zimetumika kudhihirisha lugha komavu ya mwandishi na mazungumzo ya kimafumbo. Mwandishi anatumia mbinu hii kimwingilianomatini ili vijana wasielewe yale wayasemayo wazazi wao. Mbinu hii katika riwaya imetumiwa kuchochea mawazo kwa mahadhi ya visasili na kutia utamu wa maandishi katika kuingiliana na mawazo ya mwandishi kudhihirisha maudhui na dhamira.

### 3.1.5 Maudhui ya ulaghai

Kupitia kwa visasili hivi na kisasili kingine cha Mabavu, mwandishi anaendelea kutubainisha kisasili cha maanguko ya utawala wa Wachuna. Huyu Mabavu alikuwa mwindaji hodari na shujaa wa kupambana na wanyama wakali. Kisasili hiki kimetawaliwa na maudhui ya ujanja na uongo. Licha ya kwamba Mabavu alimwokoa msichana Kadzo, alizidi kutumia ujanja huohuo

kujipatia wasichana na kuwabikiri ili wazazi wao wapate ulinzi wake.Mabaru akatunga sheria na watu wakazifuata.

Wachuna walitumia ulagahai ili waweze kujidumisha. Waliwatia wenzao woga na hofu na wakatumia hali hiyo kujirundukia mali ya ziada. Walitunga sheria zilizowalinda. Mabavu ni majazi yenye maana ya kutumia nguvu, ulaghai na ile hali ya watu kutofahamu yale waliyodanganywa. Licha ya uongo na ulaghai, vitisho vilitumiwa kuhakikisha kuwa hawaulizi maswali yoyote. Kwa hivyo, asili ya uchuna ni ubinafsi unaopatikana katika watu wachache wanaotaka kujinufaisha wengine wakiteseka. Hali hii ndiyo mwandishi anadhamiria kufungua watu akili ili waweze kutoka kwa minyororo ya ulaghai, uongo na kunyanyaswa.

Wachuna walitumia ulaghai ili waweze kujidumisha. Kwa mfano walisema kuwe asili zao si za binadamu, damu yao si nyekundu bali ni buluu na hawakuzuiliwa kwa namna ya kawaida. Uchuna ulipoendelea zaidi kulitokea falme mbalimbali za Wachuna. Ndipo tunaelezwa juu ya madola manne yaliyopimana nguvu. Kila dola linajaribu kujipanua kushinda mengine. Wakati huu mila, desturi, utamaduni na lugha za watawala ndizo zilitambuliwa. Watawaliwa wakaanza kuwa watawala katika mambo hayo yote. Uchuna katika kilele chake waliwalaghai zaidi na kukiuka haki za mahitaji za kimsingi kwa binadamu. Walisema si lazima kula na kushiba bali kula kunategemea bahati nasibu, nyumba si kwa wote bali kwa walio na bahati kuzinunua.

Wachuna walianza kueneza uchuna baada ya kumiliki tambo la uchawi, moto na Mabavu na kuyaunganisha kuunda serikali. Utawala wao ulijikita nyoyoni na akilini mwa waja wao walipotumia mafiga ya ulafi, ujinga na uongo.

### 3.1.6 Maudhui ya siasa na utawala

Kamusi ya Kiswahili sanifu yaelezea kuwa siasa ni itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendeleza uchumi wake. Utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii hiyo. Ni mfumo wa mawazo yaongozayo utawala wa serikali ya nchi.

Riwaya ya walenisi inajishughulisha na jinsi watu wanavyoweza kutawaliwa kwa njia nzuri. Hii ni ile njia ambayo inawawezesha watawaliwa kushiriki katika utawala na kutendewa haki. Jambo hili linawezekana ikiwa wananchi wana nguvu za kumchagua mtawala wao na kumwondoa pale inapowalazimu. Lakini Mabavu alitawala kiumla. Hii ni siasa ya unyanyasaji, udhalimu na matumizi ya kimabavu. Mkangi hadhamiri siasa kama hii. Katika utunzi wake amedhamiria siasa iliyo na usawa. Siasa ya kimabavu imefungamana pamoja na mfumo wa kiuchumi wa ubepari ambao Mkangi anaona haufai.

Kwa upande mwingine, Mkangi amependekeza siasa za ujamaa kama siasa mwafaka kwa nchi zinazotaka kupiga hatua kimaendeleo. Anaamini kwamba jamii ya kisosholisti ndiyo jamii huru kabisa iliyo na demokrasia halisi. Kupitia kwa mfumo huu jamii hupevuka na kufikia kiwango cha juu zaidi cha ufanisi. Mfumo huu unaonyesha jamii isiyo na matabaka wala unyonyaji wa mtu kwa mtu.

Mkangi ametumia kisasili cha Mabavu kushtumu siasa na utawala wa kimabavu. Anaeleza kuwa usawa ndio msingi wa ujamaa. Kulingana na mtunzi, mali ni ya watu wote. Siasa nzuri inayohubiriwa na Mkangi ni ile inayofanya watu wa madaraka kubwa na majukumu mazito kutokuwa na kiburi.

### 3.1.7 Maudhui ya maendeleo.

Katika riwaya husika, mwandishi anaonyesha hali ya kupiga hatua na faida zake. Mtu moto alivumbua moto ambao ulitumiwa kuchoma kulungu na kufanya chakula kiwe kitamu. Moto uliangaza nuru kwenye nyumba za watu na pia kuivisha na kuunguza. Mchawi naye aligundua siri ya matibabu hasa kwa walioumwa na nyoka. Mchawi alitumia mizizi ya mti na kusaga unga na majani ambayo yalivurugiwa vuo. Hatimaye tiba dhidi ya kuumwa na nyoka na maradhi ilipatikana. Hii ilisaidia kupunguza idadi ya maafa kutokana na janga hilo.

Mwandishi anadhihirisha kuwa bila maendeleo watu hukwama katika ujinga wa hali ya juu ilhali maendeleo hufanya jamii kujiendeleza na kujiepusha na baadhi ya matatizo. Hivyo jamii kuendelea yafaa wanajamii kuwa mstari wa mbele kwa sababu kuna manufaa mengi. Mtunzi anapinga tabia zisizofaa katika jamii kama kupenda mali, pesa na uwezo pasi na kueneza ubinadamu kwa wanajamii. Kupitia visasili hivi, mwandishi anaonyesha hali kamili ya jamii. Anatumia visa hivi kuchochea fikira za jamii ili kujaribu kuunga au kupinga msimamo fulani. Pia anadhihirisha kuwa watu walio na mamlaka hutukuzwa hata wanapokosa tabia ya utu kwa wenzao. Katika riwaya husika, mwandishi anaonyesha kuwa kuna matatizo yanayokumba jamii yanayotokana na uwezo wa utawala.

Mwandishi anaeleza kuhusu uongozi wa Wachuna. Uongozi usio na usawa, uongozi wa kimabavu usio na uelewana usiopingika na ulijawa na masharti ya kudhulumu wanajamii. Mwandishi analenga kuonyesha kuwa jamii inahitaji kupinga utawala wa aina hiyo kwa sababu unawanufaisha wachache badala ya jamii nzima. Inafaa jamii kujitolea ili kujikomboa na kuwa na uhuru kamili.

### 3.1.8 Maudhui ya Uongo na Ujinga

Kuna ujinga wa asilia ambao kila mtu hupitia hasa akiwa mtoto. Hii ni pamoja na kujitapikia na kutegemea binadamu wengine. Pili ujinga wa kijamii unaomfanya mtu mwerevu kuonekana mjinga, mwehu kuonekana timamu, muuaji kuonekana mlinda usalama na msema kweli kuonekana mwenda wazimu. Tabaka la wachochole linaishi kijinga. Wanaishi katika hali duni inayotokana na kunyanyaswa na Wachuna. Wanapitia matatizo mbalimbali, wanaiga mambo ya kigeni na hata kutumia lugha za kigeni. Katu hawajifahamu. Ubaguzi kwa misingi mbalimbali kama dini, kabila, jinsia na rangi unawaangamiza kwa sababu ya kutojua.

Kuna tofauti kubwa kati ya Wachuna na wenyeji. Wachuna wamejinyima kimaendeleo hata wana uwezo wa kuongea kwa mawazo. Wametumia akili kuwalaghai na kuwafanya wenyeji kuwa wajinga ili wazidi kuwanyanyasa na kuwafanya vipofu. Hawajui kuwa mambo hayatokei tu kwa kibahati bali hupangwa na kushughulikiwa. Wameteseka kwa kukosa maarifa.

Wachochole wanafananishwa na popo na ni vipofu. Wao ni mapopo kwa kuwa hawawezi kuona dhuluma kati yao, hawawezi kunusa uvundo wa magonjwa ya kitabaka kati yao, hawawezi kusikia mayowe ya njaa na umasikini kati yao. Wanaishi kichwa chini miguu juu. Haya yote yanadhihirisha jabali la ujinga walio nalo. Ujinga unaletwa na kutokuwa na ushirikiano, uelewano na wengi kutotimiza kazi yao vilivyo. Mtunzi anayaangazia masuala yanayowafanya watu wa tabaka la chini kukosa kuyaona yale Wachuna wanawatendea. Mtunzi anataka wajifunze wenyewe. Wamepewa nafasi ya kuchagua kuchunguza na kudadisi ili wajivumbulie wenyewe.

Kuna ujinga pia. Kwamba ujinga ukimtawala mtu, kumbe anaishi ujinga, anakula kijinga, anakunywa kijinga na kufa ujingani. Eti ujinga ni raha, ni starehe na hausumbui. Maskini

wamevumilia wakiwa katika hali ya ujinga. Ujinga unajidhihirisha katika riwaya ya *Walenisi*. Riwaya za *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)* zinaonyesha jinsi imani fulani zinavyokuzwa na kuendelea kumwathiri maskini. Katika *Walenisi (1995)* mwanamke ana ashiriwa kuwa ndizi, kuwa hindi, muwa, dau, samaki na anaaminika kuwa hivyo kabla ya ufyanduzi.

Wachuna tayari wamechukua usukani. Sasa wanataka kujiimarisha. Wanaonekana wakitumia ulaghai kwa mfano walisema asili zao si za kibinadamu, damu yao si nyekundu bali ni buluu, waliwalia wenzao uoga na hofu. Pia walitumia sheria, shibe na njaa kuwanyanyasa na kuwachuna wengine. Mwisho kulitokea makundi mawili ya mla na mliwa, wenye akili na akili pungwani. Hawa ndio walioleta madola manne yanayopimana nguvu. Wakati huu mila, desturi, utamaduni na lugha za watawala ndizo zilitambuliwa. Watawaliwa wakawa kinga tu kutoka kwa watawala.

Watawala hawa waligeuka mahitaji ya kimsingi ya binadamu wakasema, "si lazima kila mtoto aelimishwe." Wachuna hawa waliunganika baada ya kumiliki tambo la uchawi, moto na Mabavu ili kuunda serikali. Tambo la moto linahusu ufundi, uhandisi na teknolojia ya Mabavu ikachukua nguvu, vyeo na madaraka. Pia walitumia mafiga ya ulafi na ujinga kuwalaghai maskini. Wao walipata ujasiri, ukinaifu na ufahamu.

Mwisho wananchi walitumia zile silaha za wachuna kama uoga, ulafi na ujinga na kuikomboa nchi yao wakiita Walenisi. Kwa hivyo kunaonekana kuwa watu wasipokufa moyo hufanikiwa katika kuyafikia yaliyo moyoni mwao.

Katika mchango wake, Mkangi alifaulu kuunda jamii mpya aliyodhamiria iliyo na usawa. Kupitia kwa maudhui ya riwaya teule ubainishaji wa ujenzi wa jamii mpya ulipatikana jamii

yenye utu na usawa iliweza kuumbwa. Mkangi alituonyesha umuhimu wa ukombozi kama njia ya kujenga jamii mpya. Mapenduzi yalileta ufanisi mkubwa.

Mkangi alitufahamisha jinsi jamii zetu zilivyo pungufu na mbovu na jinsi utu wetu ulivyofifia. Hata hivyo alikuwa na lengo kudhihirisha kwamba jamii zetu duni zinaweza kubadilishwa na kuboreshwa kufikia viwango vya juu sana.

## 3.2 Visasili katika kudhihirisha maudhui na dhamira katika riwaya ya *Mafuta (1984)*

Riwaya ya *Mafuta (1984)* iliandikwa na Katama Mkangi wakati wa serikali ya ukandamishaji. Alikiandika ili kuondoa udhalimu mkubwa uliokuwepo wakati huo. Alikuwa katika mapambano ya kuona kwamba nchi yetu inajitoa katika hali iliyokuwepo. Ilibidi mwandishi aandike *mafuta* (1984) kimafumbomafumbo kwa kutumia visasili. katika mafuta. Katika mafuta mwandishi ametumia visasili kuweka fasihi ya kale ya ndani kwa sababu alikuwa anachambua serikali na jamii.

### 3.2.1 Hali ya utabaka

Kisasili cha mafuta kimetanda riwaya nzima huku kikisimulia visa mbalimbali. Riwaya hii kupitia visasili inasimulia mikinzano inayoletwa na maudhui ya utabaka katika jamii. Kuna tabaka la wateule na tabaka la wachochole. Wateule wanafuata itikadi ya mafuta na wachochole au tabaka la matope linafuata itikadi ya maji.

Mwandishi ametumia mafuta kama fumbo kumaanisha pesa, nguvu za kiuchumi zinazoweza kumpa mtu utawala juu ya wengine. Mafumbo yameingiliana kimatini na kimaandishi kuelezea hali ya tabaka katika jamii husika.

#### 3.2.1.1 Tabaka Teule

Tabaka hili limesawiriwa katika viwango viwili. Kuna wale ambao walizaliwa katika uteule. Hao ni wenye mafuta ya kurithiwa au kutokana na urithi kama vile Ti. Wazazi wao walikuwa wateule. Kuna wateule wa juhudi wamefika uteuleni kwa kutegemea juhudi zao kama vile mama Fofi. Hawa wametumia ujanja na uwezo wa kinyama kuufikia uteule, wametumia mbinu mwafaka.

Hali ya utabaka yatuonyesha kuwa ni wachache tu wenye uwezo wa kuyapata mafuta (uk.13) kisasili cha mafuta kina mtoa mhusika Ti kuwakilisha tabaka la wateule. Mandhari yao ni maskani ya wateule na yamesawiriwa katika (uk.14) chumba cha kuvutia, madirisha ya vioo na mbwa wakali wanawalinda. Mwandishi ametumia jazanda ya mafuta, kuelezea maudhui ya unyonyaji katika riwaya hii. Dhana ya unyonyaji inajitokeza katika tabaka hili. Usiku kuna makelele lakini mchana ni shwari kwa sababu nunda wala watu huwa wameshiba na wamelala (uk 15). Taswira ya wateule inayotolewa ni watu wenye sura za furaha, wakimetameta kwa mafuta. Wateule hao ndio waliomiliki hoteli kubwa kubwa.

Kutokana na ukatili wa tabaka hili, walihakikisha kwamba makombo na masaza ya chakula hayakuwafaidi wanyonge/maskini kwani walihakikisha waliajiri askari kuyalinda. Zaidi ya hivyo, makombo hayo yalinunuliwa na matajiri kwenda kuwalisha nguruwe wao. Inaonekana wateule wanawachukia wanyonge au maskini wa tabaka la matopeni (uk.40). Wanacheka wanapomwona Matope karibu kula chakula kilichotiwa sumu ya panya. Huu ni ukatili na kukosa utu kwa binadamu wenzao. Wanaonekana kufurahia mateso ya Matope. Wamesahau kwamba wanamatope ni watu kama wao.

Mahakama ni taasisi ya wateule na inatumiwa kuwaogopesha wanyonge. Mtunzi anatuambia ni mahakama ya uongo ukijidhihirisha ukweli hujitenga (uk. 21).wanyonge kama vile Matope, Ti na Mtue, wanahukumiwa. Matope anahukumiwa kifo kwa kuyanajisi mafuta ya mama Fofi kwa maji. Nao Ti na Mtue wanatupwa korokoroni kwa kosa la kucheka, kumaanisha walivunja sheria ya mahakama. Baadaye, Mtue anahukumiwa kifo ilihali Ti anaachiliwa huru kwa kuwa ni mmoja wao. Hapa mwandishi anadhihirisha maudhui ya ubaguzi. Mtue anaachiliwa huru ilihali maskini anateswa.

Tabaka teule linazingatia sheria, kanuni au mila fulani (uk.20) kama vile kujipaka mafuta kabla ya kukilalia kitanda. Mwandishi ametumia jazanda ya kitanda katika visasili kuonyehs itikadi ya uongo. Kitanda kimechukuliwa kama kilele cha ufanisi. Kitanda kinaonekana kikining'inia kuonyesha kuwa kitaanguka. Yaani wateule ingawa waliweka masharti magumu ili kudumisha uteule bado unayumbayumba.

Mtunzi anatumia visasili simulizi ili kudhihirisha jinsi ukweli unavyoogopewa. Wateule wana msimamo kwamba asemaye ukweli lazima anyamazishwe. Kicheko cha kutisha na kuogofya ni mbinu mojawapo inayotumiwa na wateule kutisha na kuogofya wanyonge. Hata hivyo kuna dalili ya kuporomoshwa kwa kitanda na itikadi ya uongo ni dhihirisho kuwa uongo haudumu. Nguzo za tabaka hili ni kusema uongo.

Viongozi katika tabaka hili wanataka kuvishwa vilemba vya ukoka. Mawaziri majemedari wote wamo katika mbio za kujipendeza kwa viongozi. Kwa hivyo, hawasemi ukweli. Hawana utu na hawajali wanyonge.

#### 3.2.1.2 Tabaka la chini

Hii ni maudhui inyozungumzia tabaka la wanyonge, maskini hohehahe. Hawa wamedharauliwa na tabaka teule. Hawana chakula na wanakula kutoka mapipani kama vile matope. Hata hawana mahali pa kulala, wanalala matopeni. Mwandishi anaelezea hali yao ya kuhuzunisha sana ili kuamsha hisia za msomaji. Taswira hii ni ya ajabu kwa sababu kweli. Si jambo la kawaida binadamu aliye na akili kamili kulala matopeni.

Mwandishi ametumia kisasili cha matope katika kutoa maudhui ya tabaka ya chini. Katika kule kuingiana kimaandishi Mkangi ametumia lugha ya uvundo, uchafu yenye kuleta hisia za kinyaa kwa mfano chakula cha mapipani ni kichafu na kingeweza kuwadhuru afya lakini walikuwa hawana budi kukila.

Ya kwamba vumilia ni jibu la ndani. Hii ni aina ya udanganyifu na mchezo katika mawazo ya sitofahamu za binadamu. Yote haya hufanya mawazo kutulia lakini katika dhiki, majonzi na majuto ya kila aina katika jamii. Haya mawili pia yanajionyesha katika kitabu ya *Mafuta (1995) na Walenisi (1995)*.

"Meno hucheka mabaya," kucheka tena kulileta uvumbuzi. Baada ya kulaumiwa sana, Ti aligundua kuwa kucheka mabaya kunafananishwa na ugonjwa wa sufura. Ulimfanya kugaagaa kitandani kiasi cha kumuonea huruma.

Sasa hapa kuna kisasili cha magonjwa yasiyotibika aina fulani ya kifafa. Ti anagaagaa mate yakimdondoka kutoka kinywani, kujikojolea na hata kukimbia msalani. Hata Ti alionekana kuwa mwehu (uk 49, mafuta). Mtu hacheki peke yake, na akicheka basi ni kichaa. Mwandishi anaonyesha kisasili kuhusu magonjwa ambayo hayatibiki na yale yanayosababisha hayajulikani. Hayawezi kuongelewa wala kupelekwa kwa madaktari wale wengine.

Tabaka la matopeni halina namna ya kujistarehesha katika majumba ya starehe. Hawana la ziada ya starehe yao. Hili ni tabaka la wanyonge linalojumuisha walio wengi. Hawana kazi ya kufanya kwa hivyo cha kuweka mdomoni ni bahati tu. Wengi wa hawa maskini wamekata tamaa. Hali hii imedhihirishwa na hali ya kulala matopeni. Wamekosa matumaini. Hata hivyo mwandishi amedhamiria jambo hili liangaziwe kwa ndani na zaidi linahitaji umoja na ukweli ili kufikia ukombozi wa wachochole. Hili ndilo lililokuwa lengo la mwandishi kupitia kisasili cha wanamatope kupitia kupigania usawa katika jamii. Ukombozi hauwezi kupatikana bila kuona umuhimu wake. Mkangi amedhamiria kutuonyesha umuhimu wa ukombozi kama njia ya kujenga jamii mpya.

### 3.2.2 Maudhui ya mapenduzi

Mapenduzi haya yanakuja ghafla kiasi cha kwamba hayasadikiki kwa urahisi. Mwandishi kupitia kisasili cha matope hatuonyeshi maandalizi yeyote ya mapenduzi. Wahusika wengine kama vile mama Fofi na mama Shibe wanayaona mapenduzi kama mwisho wa dunia. Hawaelewi wataishije bila mazuri waliyoyazoea. Hawa wanaona kwamba maisha yatakuwa magumu bila uteule. Mapenduzi haya yanaletwa na wanyonge. Mtunzi anatumia jazanda ya maji katika kuleta yale ambayo alidhamiria. Ametumia jazanda ili kuonyesha kuwa kitu chochote chenye uhai lazima kihitaji maji. Itikadi ya maji ina mashiko na haishindwi. Kwa hivyo, kulingana na mwandishi maji ni uhai na huendelea kuwepo. Mafuta ni itikadi isiyoweza kuwekwa katika mizani moja na maji kwani haina mashiko, ni ya uongo. Kwa ujumla mwandishi amedhamiria kuonyesha kwamba uongo na ukweli havitangamani.

### 3.2.3 Maudhui ya ubepari

Kisasili cha mama Fofi kinadhihirisha maudhui ya ubwanyenye na ubepari. Mahakamani, mama Fofi analalamika jinsi alivyonyimwa uteule tonge likiwa mdomoni. Haya yalimaanisha

ubwenyenye na ubepari uliokita mizizi katika nchi nyingi za kiafrika na kuzua matabaka. Kulikuwa na kunyonywa na kudhalilishwa kwa wafanyakazi. Mabadiliko yaliyoletwa na wanaharakati kama vile Ti, Mtue na za mama Fofi za kutumia wengine kama ngazi ili afikie kilele cha ufanisi kwa wanyonge (uk 30-31). Mama Fofi alieleza jinsi bwana wake alizaliwa katika mazingira ya ufukara. Mama Fofi Analia haki itendeke ilhali alikuwa amenyonya wafanyikazi waliomsaidia katika kazi yake. Faida iliyopatikana ilikuwa mali ya kibinafsi haki kwa kula jasho la wengine. Hili ndilo mwandishi alidhamiria kupinga. Suala la unyonyaji kwa wengine, mtunzi analipinga vikali. Anahitaji usawa katika jamii.

### 3.2.4 Maudhui ya Uongo

Kitanda alichokiona Mtue na ambacho wachochole waliaminishwa kwamba kipo na hadi wajipake mafuta ili wakilalie ni uongo ambao umekuwa ukweli sababu hakuna mteule yeyote ambaye angelitaka kuelezea upumbavu wake. Uongo huu ndio uliodumisha maslahi ya watawala. Kutokana na maelezo haya, msomaji anapata hisia za kuhadaiwa na kupuuzwa na viongozi walio mamlakani. Kupitia kwa hisia hizi msomaji anatiwa mwamko wa kutaka kupendua mfumo wa siasa ambao umejengwa kwenye misingi ya uongo na unafiki.

Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji kuhusu ushirikina unaojengwa kudumisha Imani katika jambo fulani. Wale wanaopata jambo hilo huwa wanajijua na huchelea kutoa siri hizo kwa wengine. Kwao huwa ni siri kali. Katika taswira hii, unafiki wa viongozi walio katika serikali unafichuliwa. Mwamko huu mpya kwa wasomaji unalenga kumtia hisia za kimapenduzi na ujasiri ili apiganie mabadiliko yatakayoleta ujenzi wa jamii mpya iliyo na haki na usawa.

Uongo huu ndio unaotumiwa na viongozi walafi, wakatili na wenye kukandamiza jamii ili waweze kujisitiri katika utawala dhalimu. Mafuta na kitanda vinawakilisha falsafa ya uongo

iliyotumiwa na kina Pwagu, Pwaguzi, Dubwana na Dubwaha ili kuendeleza dhuluma dhidi ya wanyonge wasio na mafuta wala uwezo wa kukilalia kitanda.

Kukilalia kitanda ni kujua siri za wateule. Siri ya kitanda ilikuwa ikitumiwa ili kuwapumbaza raia. Kutokana na maelezo ya wateule, Mtue alitambua kuwa mafuta ni ya aina moja na yalitiwa katika vyungu saba na kubandikwa majina tofauti. Jambo lililokuwa la kustaajabisha sana ni asili ya mafuta. Mafuta haya yalikuwa mikojo ya paka. Wateule waliojipaka mafuta haya walikuwa wakitaka kudhimisha hadhi yao. Mikojo ya paka kumithilishwa na mafuta ni jambo la kuaibisha. Kuonekana kwa mkojo huu unaibua mnuso unaoathiri moyo ili uhisi uzito wa uongo wa viongozi.

Kitanda na mkojo wa paka ni kichocheo cha zinduo. Msomaji anafafanuliwa na uhalisia kwamba mara nyingi viongozi walio mamlakani hutumia uongo ili kuwaweka mamlakani. Wengi wao hawana hekima. Wateule wamekula yamini ili wasifichue uongo huu (uk 87). Kupitia kwa taswira hii, Mkangi alitaka kuwazindua wasomaji kwamba katika kitengo cha utawala kuna mambo yasiyochukuliwa kama serikali.

### 3.2.5 Maudhui ya Ubwanyenye

Jamii ya kibepari wanadhihirisha maudhui ya udhalimu na ukatili. Katika jamii za kibepari, wafanyikazi ndio wanaofanya kazi za sulubu ili kutoa mazao. Nyenzo za kuzalisha humilikiwa na mabwanyenye na mabepari. Mahali hapa hupatikana kwa kunyonya umma hasa wafanyikazi. Hao wafanyikazi waweza kuungana na kuleta mabadiliko (mapenduzi). Tabaka la wafanyikazi ni tabaka linalodhulumiwa.

Hapa ni mahakamani ambako mama Fofi analalamikia alivyonyimwa uteule tonge likiwa mdomoni. Kunyimwa uteule tonge likiwa mdomoni inadhihirisha ubwenyenye na ubepari

uliokita mizizi katika nchi nyingi za kiafrika na kuzua matabaka. Upesi baada ya jamii kugundua kuwa walikuwa wakinyanyaswa na kundi la wachache, mabadiliko katika jamii yaliletwa na wanaharakati kama vile Ti, Mtue, Matope na wengine yaliweza kuukomesha ubwenyenye na ubepari. Wakati njama zake zilizimwa kwa upesi ndipo mama Fofi alihiari kuleta mashtaka yake mbele ya mahakama ili imsaidie kuendeleza kuwadhalilisha wafanyikazi. Wakati huohuo, mahakama zilikuwa zimepoteza hadhi ya kudumisha haki na kuwa chombo cha ukandamizaji. Juhudi za mama Fofi za kutumia wengine kama ngazi ili afikie kilele cha ufanisi kwa kuwanyang'anya wachochole zilizimwa.

Mama Fofi alileta mashtaka yake kwa sababu bidii zao zilitumbukia nyongo. Mwandishi anaonyesha juhudi zao na uhasama wa mahakama. Katika kueleza hadithi yake anaonyesha mabadiliko katika jamii kutoka kwa ubwenyenye hadi kwa ubepari. Mama Fofi alitaka kuingia katika hali hii (ubepari kwani wao waliweza kupata faida nyingi kutoka kwa kazi yao. Karl Maxx akinukuliwa na Huberman (1968: 85) anasema;

> Mabepari hawaoni kitu kingine ila faida. Katika kutaka kutekeleza shabaha hii, wao huwalipa wafanyikazi pesa kidogo… wakati huo mabepari hutaka kujilimbikizia utajiri.

Kwa maoni ya mwandishi, mama Fofi na bwanake Sifa walikuwa ni mabepari baada ya kuishi katika ulitima. Licha ya kuanza biashara ya kumbikumbi wenyewe, kulikuwa na matatizo kutoka kwa ndege na kumbikumbi wenyewe kupotea. Bidii yake ilifanya ajinunulie kichuguu chake mwenyewe. Kifo cha Sifa kilisababishwa na mashindano ya kibiashara baina ya mabepari. Kezilahabi (1974: 1) katika shairi lake jinamizi anasema;

> …samaki ambaye hupata hewa,

Utawala wa chuma ulimtoboa fuvu

La kichwa na kutupwa mtumwbini

Halafu nilifikiria Afrika

Na siasa kwa ujumla.

Lakini mara mambo kwa maelfu

Mtumbwi waliukimbilia kwa fujo

Mtumwi kupasuka wakapasuliwa

Vipande vipande

Halafu samaki wote waliinua

Vichwa vyao juu ya ,maji

Na pamoja wakaimba wimbo wa uhuru.

Maelezo haya ya Kezilahabi yanatuonyesha kuwa kifo cha bwana Sifa kilisababishwa na mashindano. Punde katika hatima ya riwaya hii tutaona wanajamii wakiimba wimbo wa maji kuonyesha ushindi wao dhidi ya dhuluma. Mama Fofi analilia haki itendeke ili aweze kupata haki yake. Lakini ukweli ni kuwa haikua haki bali alikuwa ananyonya wafanyikazi waliomsaidia katika kazi yake. Pili, faida iliyopatikana ilikuwa mali yake binafsi. Jambo hili la kutaka haki kwa kula jasho ndilo mwandishi anapinga kupitia kwa kisasili hiki. Huu uongo wa maji kuwa mafuta na kitanda kukilalia ulikuwa umefika kikomo kama wasemavyo wambao kwamba, “unaweza kuwadanganya watu lakini sio wakati wote.” Mama Fofi hakupata lolote kutoka kwa

mahakama wakati kulitokea mshindo wa ‘maji tu!’ ‘maji tu!’ ndipo mama Fofi alijua kuwa ukweli ukijidhihirisha uwongo hujitenga.

Kupitia kwa kisa cha mama Fofi, mwandishi anadhamiria kufahamisha maisha ya tabaka la matopeni. Kwa mfano, kuwania mabaki ya chakula ambacho mbwa, kuku na paka walikikataa. Waling’ang’ania makombo hayo wakibishana na panya na kombamwiko. Anadhamiria kudhihirisha hali ya unyonge na kukata tamaa kwa wanamatopeni. Kula chakula kilichotiwa sumu ili ajifilie mbali maana hawana maana yoyote.

Mkangi bado nia yake ni ujenzi wa jamii mpya iliyo na usawa. Wanyonge wamechoka na maisha haya yasiyo na raha wala matumaini. Wameanza kuona ukweli mahali ambapo umefichwa. Mwishowe wamebainisha kuwa maji ndio uhai na hayo tu ndiyo yataleta ukombozi. Unyama utatoweka, ukweli na usawa utatawala.

### 3.2.6 Maudhui ya Udhuluma na Ukatili

Matope ni raia aliyeishi katika kidimbwi cha matope. Ametumika kuonyesha uhasama ulio katika mahakama. Alitumiwa kuwaosha wateule kwa maji. Hii ilikuwa ni siri ya kuwaondoa katika uteule. Kuingia kwake kulileta mshtuko mahakamani, ‘…Mara tu walipomkata macho’ (Uk 33). Mwandishi ametumia jazanda kuelezea maudhui haya. Waya ya seng’enge za miiba iliyokaa kama makucha ya tai. Hii ni hali yao ya kuonyesha jinsi watu wa tabaka la juu huwa wanajitenga na watu wengine. Matope alipigwa na kudharauliwa, mate alitemewa, damu zikamchuruzika, maumivu yakimchoma kama miiba huku mashavu na viungo vikimwiva kwa sababu ya makofi, mateke, bakora na marungu. Haki za matope kama binadamu zilidhalilishwa na mahakama. Akiwa mahakamani alizidi kuteswa. Matope na Mtue waliwakilisha kundi la

wafungwa hapa barani Afrika bila sababu. Waliweza kuwekewa mashtaka ya uongo. Mahakama hizi zilikosa unyoofu na mahakimu wake walikosa uadilifu.

Hadithi hii ya Matope inatoa muhtasari wa shida za wanyonge katika jamii. Waonyeshao huruma kama Mtue huwekwa kizuizini kwa kusingiziwa kuwa wao ni washiriki na wachochezi.

## 3.3 Hitimisho

Sehemu hii ilishughulikia maudhui na dhamira. Kulingana na Okpewho (1963), visasili hutumiwa kueleza kuhusu mtazamo na utamaduni wao kutoka kizazi hadi kingine. Kupitia riwaya ya *Walenisi (1995)* na *Mafuta (1984)* kulibainika kuwa visasili vilichangia katika usawiri wa maudhui na dhamira. Mwandishi alishughulikia maudhui yafuatayo; utabaka, unyanyasaji, maendeleo, siasa na utawala, ufisadi, ubwanyenye, dhuluma na uongozi.

Dhamira ni mambo yanayoingiliana na maudhui, ni lengo au shabaha ya kazi ya mwandishi. Sehemu hii ilithibitisha na kubainisha dhamira kuu ya mwandishi katika *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)* kuwa ujenzi wa jamii mpya, jamii iliyo na usawa na utu. Mkangi kupitia visasili alionyesha namna jamii yenye utu na usawa inavyoweza kuumbwa. Alitokeza umuhimu wa ukombozi kama njia ya kujenga jamii mpya. Pia alieleza kuwa baada ya mapenduzi kizazi kipya kitazaliwa.

## SURA YA NNE: MCHANGO WA VISASILI KATIKA *WALENISI (1995)* NA *MAFUTA (1984)*

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inachunguza na kudhihirisha mchango wa visasili katika *Walenisi (1995)* na *Mafuta (1984)*. Visasili kama mbinu nyingine za fani hutumia sanaa kuelezea hisia mbalimbali kuhusu maswala tuyashuhudiayo na ambayo yanatupendeza au kutukera katika jamii. Mtunzi Mkangi alitumia visasili ambayo ni kiwakilishi cha wanajamii halisi kuwakilisha matendo hayo kwa mguso ili kufanikisha malengo aliyokusudia.

Ili kubaini dhima ya visasili katika riwaya teule, ni muhimu kufahamu uwezo wa mwingilianomatini katika kutoa mchango wa mtunzi. Uwezo wa kutumia mwingilianomatini unatuingiza katika sifa muhimu za mwingiliano katika visasili. Aidha, visasili huibuliwa kwa suala na tendo la kuzuka na kuendelezwa kwa matendo yanayotoa mchango katika riwaya hizo. Wamitila (2003) anasema kisasili ni hadithi ambayo haikuzwi na mwandishi maalum bali hupatikana katika imani zilizoko katika jamii fulani. Kwa hivyo, imani hii ndiyo inajenga mchango alioutoa Mkangi katika kazi yake.

Visasili ni hadithi zinazowahusisha watu, wanyama au vitu katika kazi ya sanaa ya kifasihi. Visa hivi hata vihusishe wadudu, wanyama, mashetani, miungu na kadhalika, lazima viwakilishe tabia na viwe na mchango maalum inayokusudiwa jamii. Visasili huendeleza maudhui ya kazi ya mtunzi huku zikitoa mchango maalum katika jamii husika. Utafiti ulitumia visasili kutoa mchango katika riwaya. Utafuata mkabala maalum wa Mkangi wa lugha ya kinathari katika historia.

Mtunzi Mkangi alitumia visasili vitatu katika *Walenisi (1995)* kutoa mchango wake. Kisasili cha asili ya moto, kisasili cha mchawi ambaye alivumbua dawa ya kutibu sumu ya nyoka kutokana

na vita kati ya bafe na chatu, na mwisho kisasili cha Mabavu ambaye ni mwindaji hodari. Katika *Mafuta (1984)*, mwandishi anatoa mchango wake kupitia kisasili cha mafuta, kisasili cha matope na mwisho kisasili cha mama Fofi. Kupitia kwa visasili hivyo vyote, mtafiti atabainisha mchango alioutoa mwandishi katika kazi yake.

Kufuatia nadharia inayoongoza utafiti huu, tunatambua kwamba utunzi wa tanzu katika matini huchangia pakubwa kueleweka kwa ujumbe. Kwa mujibu wa Fowler (1989), tanzu huleta muwala katika matini na kufanya kazi ieleweke kwa urahisi. Anafafanua zaidi kuwa mwingilianomatini huburudisha. Wallek na Warren (1963) wanaongezea kwamba kufuata mitindo iliyozoeleka tu haina ladha. Kutokana na misingi hii, tumebainisha utumizi wa visasili katika riwaya kama njia bora ya kusawiri ulimwengu unaowazunguka jamii.

## 4.1 Mchango wa visasili katika riwaya ya *Walenisi (1995)*

Riwaya ya *Walenisi (1995)* imetuchorea visasili mbalimbali ambavyo vimechangia katika kuendeleza riwaya. Mwandishi ametumia visa hivi kutoa mchango aliokusudia pamoja na ujumbe aliodhamiria. Visasili ni hadithi za kale zenye kuwakilisha imani na mtazamo wa jamii inayohusika kuhusu asili ya ulimwengu na mwenendo wake, asili yao wenyewe na maana na shabaha ya maisha yao. Visasili kwa hivyo hutumiwa kuelezea asili ya mambo yanayotokea katika jamii kama vile lugha, kifo, maafa, matendo, tabia, hali na kadhalika

Katika riwaya hii, mwandishi anatuchorea kisasili cha asili ya moto. Mwandishi anatuelezea kuwa asili ya moto ilitokana na mwindaji aliyetega kulungu. Alijiwa na hamu ya kumtengenezea mpenzi wake ushanga. Kisadfa alipokuwa akipekecha mti kutoboa mashimo, cheche za moto zililipuka. Aliweza kutumia moto huo kama ngazi ya kujipa ubwana mkubwa na kujibatiza ukoo wa Tai.

### 4.1.1 Kisasili cha moto

Kisasili hiki kinatangulia kwa kutoa mchango wa mhusika mmoja kwa jina Moto. Jina hili limetumika kijazanda kuashiria Wachuna. Mwandishi ametumia jazanda ya visasili katika kutoa mchango wake. Jazanda hii imeingiliana kimatini katika andishi kuelezea jinsi Wachuna walivyozuka na walivyojiimarisha. Ni muhimu kuelewa asili ya Wachuna katika riwaya hii. Kisa cha Wachuna kimetanda katika riwaya ya *Walenisi (1995)*. Hawa ni watu ambao ni wageni kutoka Marekani (uk 154-158). Katika hali ya kutofahamu, waliwadanganya wenyeji na kupata wafuasi wengi. Licha ya uongo, walihakikisha kuwa hawaulizwi maswali.

Mkangi kwa kutumia kisasili cha moto aliona umuhimu wa wenyeji kuelewa jinsi hawa Wachuna walivyouingia nchi yao. Alikuwa na lengo la kufahamu hali yao ilivyokuwa. Katika kutoa kisasili cha moto, alichangia kuwafungua macho ili waweze kuerevuka na kujikomboa kutoka kwa Wachuna.

Kisasili cha moto kilichangia kuelezea umuhimu wa uvumbuzi wa moto. Tangu jadi wenyeji hawakuwa na moto. Katika hali hiyo, mtu moto alivumbua moto kisadfa. Ni muhimu kuelewa kwamba si kila siku mambo yote hutokea kwa mpango bali mengine huja kighafla tu. Mtu moto alitaka kumtengenezea mpenzi wake shanga. Katika kutoboa mti, kisadfa cheche za moto zilitokea ambazo zilitambaa kila mahali. Jambo ambalo lilishangaza jamii nzima. Ndipo baadaye moto huu ukawa wa maana katika jamii. Huu ni uvumbuzi wa kihistoria unaoingiana katika andishi. Haya ni matukio ya kihistoria yaliyotoa mchango wake katika kuleta mabadiliko katika maisha ya mwanadamu. Uvumbuzi huu ulichangia pakubwa kufanya maisha kuwa bora.

Kutokana na mabadiliko haya, wenyeji sasa walikuwa wakijikinga dhidi ya wanyama wakali. Kisasili cha moto kilichangia kuweka msingi dhabiti ambao unatumika hadi sasa. Moto

hutumika katika upishi wa aina tofautitofauti. Mtu moto alitumia moto kuchoma nyama ya kulungu ambayo ilikuwa tamu zaidi. Hata alipowagawia sehemu ya nyama na kuwaambia wale, walizidi kuitamani. Kuanzia siku hiyo, kila mmoja wao alitamani kaa la moto kupeleka kwao kwa matumizi mbalimbali.

Mwandishi alitumia kisasili cha moto kudhihirisha kuwa uwindaji ulikuwapo tangu jadi. Kisasili hiki kiliingiana kimatini kuelezea kuwa katika historia ya mwanadamu kulikuwa na ujuzi wa uwindaji. Mtu moto alikuwa msasi hodari wa kutega kulungu. Uraibu wake huu ulikuwa kupitia njia fulani aliyoizoea. Alikuwa mtu mwenye juhudi katika kazi yake. Alikuwa mvumilivu kwa sababu alikuwa anasubiri kulungu baada ya kutega. Kwa hivyo kupitia kwa mtu moto, kisasili hiki kinachangia kumhimiza msomaji kujifunza kuwa mvumilivu katika maisha yake. Kupitia kwa mtu moto msomaji anajifunza kuwa 'mvumilivu hula mbivu' na 'mtaka cha mvunguni sharti ainame'. Hivyo kisasili cha moto kinachangia kuwatia moyo wasomaji katika hali ya kutafuta riziki zao kwa kila siku.

Kuna kuingiliana kwa matukio ya uzuri na ubaya katika matumizi ya kisasili cha moto. Mwandishi kupitia kisasili cha moto anatoa mchango kuelezea uzuri na ubaya wa moto. Moto ni muhimu katika ukawaida wake kwa sababu hutusaidia katika upishi wa vyakula ili viwe vitamu na kutukinga wakati wa baridi. Moto pia kwa upande mwingine huwa na madhara makubwa katika jamii. Cheche ndogo za moto zinaweza kusababisha hasara kubwa. Mtu moto hakuwa ameona cheche ndogo za moto zikianguka juu ya majani makavu yaliyokuwa katikati ya mapaja yake. moto ukawaka. Ulienea kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Kwa upesi ilimeza vichaka na misitu iliyokuwa mbele yake (uk 156). Mtunzi anajaribu kutoa mchango wake kuhatarisha jamii dhidi ya matumizi ya moto. Kwa kweli moto huleta hasara kwa vile ambavyo tumeshuhudia katika vibanda mijini na kwenye vituo kadhaa.

Mwandishi ametumia kisasili cha moto kutuelezea umuhimu wa mtu kuwa wa kwanza katika uvumbuzi wa jambo fulani. Mtu moto alijionea fahari katika uvumbuzi huu. Ndipo alizidi kuwaambia kuwa ni malaika ndiye aliyemtunukia uwezo huo. Punde si punde akaweka masharti magumu. Masharti haya yalifuatwa naye akawa mgawaji wa moto pekee. Mtunzi ametumia tukio la kuwa wa kwanza katika uvumbuzi, kuingiliana na kutunukiwa na malaika kuonyesha mbinu ya uongo ambayo mhusika moto alitumia kujipatia mali. Uwezo huu ukamtia hisia za ukubwa wa utukufu pia. Mtu moto alizidi kugawiwa chakula na alipata uwezo wa kurundika ziada. Katika kutoa mchango wake, mtunzi kupitia kwa kisasili cha moto anatuhimiza kuwa tuwe wa kwanza katika kufanya jambo fulani.

Kisasili cha moto kilichochea hisia za wanajamii. Kiliamsha akili ya waliolala. Kilitoa mchango wa kuleta mabadiliko kwa muda mrefu. Watu walierevuka na wakaona unyama waliokuwa wakitendewa. Walipata ujasiri, ukinaifu na mapenduzi. Walitaka mwanzo mpya na maisha ya usawa.

Mwandishi alitoa mchango kupitia kisasili cha moto kuonyesha hali ya kupiga hatua mbele na faida zake. Mtu moto alivumbua moto kwa kutumia vifaa butu vya mawe, vijiti na majani ambavyo vilitoa cheche za moto. Moto huo ulitumika kuchoma nyama ya kulungu na kufanya vyakula kuwa vitamu. Pia moto huo uliangaza nuru kwenye nyumba za watu, kuvisha na kuunguza. Mkangi alitoa mchango kupitia kisasili cha moto kuhimiza watu kusonga hatua mbele kimaendeleo. Uvumbuzi wa moto ni maendeleo katika jamii. Anashtumu jamii inayokwama mahali pamoja bila kusonga mbele. Kila mmoja katika jamii anastahili kupiga hatua mbele ili kuondoa umaskini uliopo katika jamii zetu.

Mwandishi anatoa mchango wake kudhihirisha kuwa bila maendeleo watu hukwama katika ujinga ilhali jamii yenye maendeleo hujiendeleza na kujiepusha na baadhi ya matatizo. Hivyo, jamii kuendelea yafaa wanajamii kuwa mstari wa mbele kwa sababu kuna manufaa mengi watakayopata. Mwandishi katika kutoa mchango wake alipinga tabia zisizofaa katika jamii kama kupenda mali, pesa na uwezo wa kueneza ubinadamu kwa wanajamii. Mkangi kupitia kisasili cha moto alionyesha hali kamili ya jamii. Alitumia kisa hiki kuchochea fikira za jamii ili kujaribu kupinga mambo fulani.

### 4.1.2 Kisasili cha mchawi

Kisasili hiki kinahusu mchawi ambaye anavumbua dawa ya kutibu sumu ya nyoka kutokana na vita kati ya bafe na chatu. Anamfuata chatu na kugundua matawi anayotumia kutibu. Hali hii inamfanya ainusuru jamii yake iliyokuwa inawapoteza watu wengi kutokana na sumu ya nyoka.

Kuna mwingiliano wa matukio ya uvumbuzi wa dawa na maendeleo ya taaluma ya udaktari. Mwandishi kupitia kwa kisasili cha mchawi anatuchorea dunia ambayo inaanza kujikwamua kimaendeleo kupitia kwa uvumbuzi mpya wa dawa ya nyoka. Anatoa mchango kuonyesha kwamba taaluma ya udaktari hufanya kazi muhimu katika jamii. Taaluma hii huokoa maisha ya watu kutokana na magonjwa mbalimbali.

Kadhalika, Mkangi anatoa mchango wake kwa kutumia kisasili cha mchawi kwamba taaluma hii wengi waitumia vibaya kwa njia ya ufisadi ili waweze kutoa huduma yao. Shida hii imewakumba sanasana tabaka la wachochole. Mtunzi anatoa mchango kuwashtumu wanaotumia ufisadi katika taaluma hii. Mwandishi anatumaini na kudhamiria jamii mpya iliyo na usawa.

Mchawi katika jamii ni mtu anayesadikiwa kuwa anaweza kuwadhuru watu kwa kuwavuruga. Lakini mchawi tunayeangazia katika kisasili cha Mchawi, riwaya ya *Walenisi (1995)* kinasimulia mchawi kama daktari aliyeokoa maisha ya binadamu hasa wale walioumwa na nyoka.

Kuna kuingiliana kwa matukio ya daktari na umuhimu wake katika jamii. Mwandishi anatoa mchango wake kutuchorea katika jamii kwamba kazi ya daktari ni kutibu wagonjwa akitumia dawa. Sio kila mtu ni daktari bali ni yule tu ana hiyo kipawa na amehitimu katika kazi yake. Daktari pia ana ujuzi wa kuwahudumia wagonjwa. Mchawi aligundua siri ya matibabu hasa kwa waliougua kutokana na kuumwa na nyoka. Alitumia mizizi ya mti na kusaga unga na majani ambayo aliyavuruga vuo. Hatimaye tiba dhidi ya kuumwa na nyoka au maradhi mengine ilipatikana. Hii ilisaidia kupunguza idadi ya maafa kutokana na janga hilo. Mtunzi katika hali hii anajaribu kutoa mchango wake kuonyesha umuhimu wa daktari katika jamii. Vifo vingekuwa vingi kama taaluma ya udaktari haingekuwa. Hii ni idara ya maana sana katika jamii kwa ujumla.

Mwandishi katika kazi yake ametumia taswira ya nyoka katika kisasili cha mchawi kutoa mchango wake. Taswira ya nyoka ni magonjwa tofauti yanayoikumba jamii. Jamii inaishi katika hali ya taabu lakini mwishowe suluhisho linapatikana kutokana na uvumbuzi wa dawa za kutibu magonjwa hayo. Hapa binadamu hupata nafuu na kuishi mustarehe. Mkangi anatoa mchango wake kudhihirisha jinsi dunia inavyosonga ndivyo uvumbuzi nao unaendelea. Magonjwa ni mengi madawa nayo yameongezeka. Mtunzi anazidi kuwapa jamii moyo waendelee kuvumbua zaidi ili waweze kuokoa maisha ya mwanadamu.

Kuna mwingiliano wa miti na faida zake katika andishi. Miti ina faida nyingi katika jamii. Miti ni dawa. Mwandishi anatoa mchango wake kuhimiza jamii iweze kuhifadhi misitu ili binadamu

aendelee kufaidika. Mchawi anatumia miti kutibu. Akikosa miti basi kazi yake haitaendelea. Hivyo basi, mchawi hatatibu na mwishowe vifo vitakuwa vingi kwa kukosa dawa. Mchawi hata naye ataumia kwa kukosa kutunukiwa chakula. Kupitia kisasili hiki anatoa mchango kuonyesha jinsi jamii inategemeana. Mchawi anaendelea kutoa huduma ya kutibu ilhali wanajamii wanamlisha pamoja na jamii yake.

### 4.1.3 Kisasili cha Mabavu

Kisasili cha mabavu kinatangulia katika riwaya ya *Walenisi (1995)* kutoa mchango na kudhihirisha dunia ambayo imekwama kimaendeleo kwa sababu ya uongozi na sera mbaya za kiuchumi. Dhamira yake ni kusawiri uongozi bora usio na ubinafsi. Ametoa mchango wake kuonyesha jamii iliyochoka na utumwa wa kubebeshwa mizigo. Katika jamii ya Wachuna wale ambao ni matajiri wanarundukisha ziada.

Ni kisasili kilichofuata mwingiliano wa matukio kama vile ukombozi, kukwama kwa maendeleo, uongozi wa nguvu na unyanyasaji. Ni kisasili kilichofuata mwingilianomatini wa majazi ili kutoa sifa ya mhusika Mabavu. Mabavu alikuwa mwindaji hodari ndipo baadaye akatumia nguvu kujipatia utajiri. Mtunzi ametumia mbinu hii kutoa mchango wake ili kuonyesha jamii inayostahili kuhurumiwa na kufarijiwa.

Mtunzi anachochea msomaji pamoja na jamii iliyoteswa katika kutoa mchango wake ili wang'amue uwezo wao wa kupinga tuhuma dhidi yao. Anajaribu kuwaonyesha kuwa kujinasua kutoka katika uongozi huu wa nguvu ni kupitia kwa njia ya ukombozi. Maskini wanastahili kuinua macho yao na kuona kwamba wamepokonywa haki zao, mashamba yao yametawaliwa. Wamepotezwa na kunyang'anywa kupitia nyanja mbalimbali kama vile historia yao na utamaduni wao. Hivyo, kuna haja ya kujipigania kimaisha. Hii ndiyo lengo kuu ya mwandishi.

Ametoa mchango wake kuwa maskini apate haki yake. Analilia usawa katika jamii iliyodhamiriwa.

Mwandishi ametoa mchango katika kuhimiza jamii kutokufa moyo wakati wa kupigania ukombozi. Ni juhudi ambayo huchukua bidii na uvumilivu mwingi ili kuzaa matunda. Matukio haya yameingiana na Mabavu jinsi alivyoweza kupambana na wanyama wakali na kuwashinda. Alipambana na simba na mwishowe kumwokoa msichana Kadzo. Kwa hivyo wenyeji nao wajue kwamba si rahisi kupata ukombozi bali ni kwa njia ya kujitolea kwa sababu kuna kuteswa na wengine kufa kwa njia hiyo. Lakini wawe wavumilivu na kujitoa mhanga ili ukombozi huu uweze kupatikana.

Mtunzi katika kutoa mchango ametumia istiari katika kisasili cha Mabavu ili kuchochea fikra za jamii waweze kuona haja ya kushirikiana na kubomoa mipaka isiyofaa. Msichana Kadzo alinyakuliwa na simba. Simba ni istiari kuashiria wakoloni walionyakua nchi za waafrika. Hivyo, wanajamii walionyesha umoja kumwandama huyo simba ili wamwokoe msichana Kadzo. Kwa bahati mbaya aliwashinda werevu na mbio nao wakafa moyo. Tukio hili ni kuhimiza jamii kuwa na juhudi na kushirikiana ndipo waweze kupambana na adui kwani ‘umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu’. Mkangi alitoa mchango wake kwa wanajamii waliodhulumiwa waweze kuwa na umoja ili waweze kujikomboa.

Mtunzi alitoa mchango kuelezea jukumu la mzazi kwa mwanaye na pia kuonyesha kuwa ‘damu ni nzito kuliko maji’, wazazi wake Kadzo walimjia Mabavu kwa unyenyekevu na huzuni mingi wakimsihi aende kumwinda huyo nunda na kumuua. Waliongezea kuwa, ikiwa Kadzo angepatikana hai, wangemuoza awe mkewe. Hili lilisawiri jukumu la mzazi kwa mwanawe. Walijaribu juu chini kuona kuwa msichana wao ameokolewa. Wazazi wa Kadzo walichukua

hatua ya busara kumwendea Mabavu ili aweze kumsaidia Kadzo. Ni dhihirisho kuwa hata kama jamii hushughulikia mambo pamoja, kuna pia mambo ya familia inayobidi. Tukio la Kadzo kunyakuliwa na simba linaingiana kimaandishi katika kuelezea jinsi Wachuna walivyonyakua ardhi ya mwafrika. Kupitia tukio hili mwandishi anatuelezea chanzo na kuenea kwa Wachuna. Kwa njia ya busara na uerevu walitawala polepole na mwafrika kuwa chini yao. Akiwa na lengo la kumwonyesha maskini mwafrika jinsi alivyonyanyaswa kiasi ya kwamba atafute mbinu ya kurudisha mali yao kwa njia ya kukuja pamoja kama ndugu na dada.

Kama jina linavyodhihirisha, Mabavu linamaanisha nguvu. Tukio la uongozi linaingiana na nguvu katika kuelezea na kutoa mchango wa aina ya uongozi. Ni uongozi usio na usawa, wa kimabavu, usio na uelewano usiopingika na uliojawa masharti ya kuwadhulumu wanajamii. Mwandishi alilenga kutoa mchango kuonyesha kuwa jamii ilihitaji kupinga uongozi wa aina hiyo kwa sababu uliwanufaisha wachache badala ya jamii nzima. Ilifaa jamii kujitolea ili kukomboa na kuwa na uhuru kamili. Mabavu alitumia uwezo wake dhidi ya wasichana aliotaka na kuwaoa kila apendavyo. Kisha kuwalazimisha watu wampe chakula kama malipo ya kuwalinda.

Mkangi kupitia kwa kisasili cha Mabavu ametoa mchango kuwafundisha wanajamii kuwa na maadili mema kama vile utiifu, uvumilivu, huruma, kujikakamua, ujasiri na mitazamo ya jamii dhidi ya familia na jinsia. Mabavu alionyesha kuwa wanawake wanalindwa na wanaume. Jamii haiwezi kuendelea bila ndoa. Mabavu alizidi kuoa wasichana ingawa kupitia kwa njia ya ujanja na ila zake. Ndoa ni muhimu katika jamii na vizazi vijazo. Mkangi ameonyesha jinsi tukio la ndoa lilivyoingiana na jamii katika kutoa mchango wake kupitia kisasili cha Mabavu. Hiki ni kisasili kinachohimiza jamii iendelee na mpango wa ndoa kila kuchao.

Katika kutoa mchango, Mkangi ametoa tukio la kufaulu kuingiana na kutumia nguvu. Kulingana na kisasili cha Mabavu, sio mambo yote tunaweza kuyafaulu kwa kutumia nguvu kama mhusika Mabavu. Mtunzi ametumia semi 'nyama na ulimi' katika kuelezea matukio haya. Kadzo alimpenda Dutu kwa sababu alimpa nyama ya ulimi. Kuna mambo tunayoyafanya kwa njia ya upole kwa kutumia maneno matamu, kubembeleza, kunyenyekea na hata kwa njia ya kushawishi. Tabia za Dutu zilikuwa za upole na alitumia maneno ya upole ya kupendeza ndipo Kadzo akampenda. Kwa hiyo, mwandishi alichangia kutuonyesha kuwa katika maisha ya kila siku kuna yale tunafaulu kwa kutumia Mabavu na mengine kwa njia ya kutumia maneno matamu ya kupendeza.

Kisasili cha Mabavu kinachangia katika kuleta mwamko mpya wa kisiasa. Haya ni matukio yanayoingiana kimatini katika andishi. Yanaelezea jinsi Wachuna walioriithi nyenzo zote za uzalishaji mali. Ilibidi umma uwatumikie kutokana na vitisho walivyopewa. Kisasili hiki kinatoa mchango kuonyesha jinsi umma ulivyogundua hayo ndipo ukawa na mwamko wa kupata afueni katika mfumo wa kiuchumi na kisiasa ulionawiri. Mchango huu uliwafanya kutambua kuwa mateso waliyopata hayatokani na bahati mbaya bali ni kwa sababu ya uhusiano wa kijamii uliodunishwa na sheria za utawala wa kimabavu. Uliwafanya kuhimizana kuwa wasiikubali hali yao ya taabu kuwa ni majaliwa na lazima wajibidiishe kusaka uhuru wao.

Matukio ya kimabavu, yameingiana na hisia za jamii. Matukio haya yametoa mchango wake kwa kuamsha hisia za jamii. Yanaonyesha kwamba hisia za binadamu hubadilika kulingana na mazingira yalivyo. Kwa mfano kisa cha Kadzo kilifanya wanajamii kuwa na hisia za majonzi. Msichana Kadzo ambaye alivamiwa na simba na akachukuliwa kuwa amekufa. Wengi wakajazwa na huruma wengine walionyesha dalili za kutoa machozi au kulia kutokana na huruma iliyowajia. Kwa ujumla kisasili cha Mabavu kilitoa mchango kudhihirisha kuwa hisia za

binadamu hubadilika kulingana na hali ilivyo. Kadzo aliponusuriwa hali ya machozi ilibadilika na ikawa ya furaha, vifijo na nderemo. Furaha iliyoje kumwona tena akiwa anapumua. Kisa hiki pia kinatoa mchango kuonyesha kuwa kulikuwa na uhaba wa kina 'mabavu' wa kutoa ulinzi, ndipo watu walimiminika kwake ili waweze kupewa ulinzi. Ulinzi huu ulizua ubinafsi kuhusu jambo hili la wachache kumiliki nyenzo zote za uzalishaji.

## 4.2 Mchango wa visasili katika riwaya ya Mafuta

Katika riwaya ya *Mafuta (1984)* mwandishi ametumia visasili katika kutoa mchango wake kwa namna nyingi. Kwanza vinaelezea kuhusu asili ya tabia fulani katika jamii. Kwa mfano, inatoa mchango kudhihirisha mwanzo wa imani kuhusu watu waliotunukiwa kuwa na mafuta kwa uzao au kwa bidii zao. Matajiri walitukuzwa na hata kutukuza ubinafsi uliochangia kukosa utu ilhali wenzao walidunishwa, walidhoofishwa na hata kukwama na kufa katika umaskini.

Kupitia kisasili cha mafuta, mwandishi anatoa mchango kuonyesha chanzo cha taabu za wanajamii. Shida hizi zimechangia binadamu kuwa na mitazamo tofauti kimaisha kwa.walio na matitizo, wakajiona wamelaaniwa ilihali waliofaulu wanajionea afueni na waliobarikiwa na Mungu. Hivyo kuwa wateule. Anaonyesha kuna haja ya kufanya uchunguzi na uvumbuzi kuhusu masuala yanayoathiri jamii ambayo yanachukuliwa kama utamaduni usiopingika. Pia kisasili hiki kinatoa mchango zaidi kudhihirisha kuwa ujinga na ulaghai ni masuala yanayotatiza jamii kimaendeleo. Hivyo, kuna haja ya jamii kuelimishwa kuhusu utu na usawa kwa utawala wa wanajamii.

### 4.2.1 Kisasili cha Mafuta

Mwandishi ametumia kisasili cha mafuta kimafumbo katika kutoa mchango wake. Anaelezeda kuwa mafuta yako kila mahali. Mafuta inamaanisha pesa ambazo ni muhimu sana katika starehe zote za mwanadamu. Tukio hili la mafuta limeingiliana na mahali. Yanapatikana chini ya kitanda, ndani ya nyumba na hata pia matopeni yapo. Mtunzi anachangia kuwa mafuta yanaleta raha ndani ya moyo wa binadamu. Yanafanya mandhari yanukie vizuri na yanaweza kukupea furaha na buraha zote ulimwenguni. Ukitaka kuenda nchi za ulaya mafuta yatakupeleka, mavazi mazuri mafuta huleta. Hakuna kitu binadamu atakosa akiwa na mafuta. Mafuta ni tunda la roho na tena ni dawa. Yanafanya maisha yanakuwa mema na ya kutamanika.

Tukio la mafuta limeingiana na bidii ya mchwa. Mtunzi anatoa mchango wake hapa kutuonyesha kuwa wanamafuta hawalali bali wanazunguka usiku kucha kuyatafuta. Wanapoyapata, uchoyo unawatawala, hawataki mwingine kufanikiwa nayo. Wanaongozwa na wivu pamoja na uongo. Mtunzi anachangia zaidi kupitia kisasili hiki kuonyesha jinsi hata wale wanaotafuta pesa usiku na mchana hawako tayari kufichua siri zao jinsi wanavyopata mafuta (pesa). Nchi nyingi za Afrika ya leo tunazifananisha na nchi za wateule kwa njia ya kutumia uongo na kuficha ukweli. Leo hivi maskini bado anaumia kwa ajili ya kukosa mafuta (pesa). Hawakilalii kitanda, wanalala sakafuni sawa na kulala matopeni.

Mkangi anatoa mchango wake kupitia Mafuta kudokezea ya kwamba dhuluma inatawala. Wananchi hawana haki ya kutoa maoni yao na wanapozungumza huambiwa kwamba wanaropoka. Hakuna anayewasikiliza. Mahakama nayo imekua chombo cha kuwanyanyasa. Hakuna haki inayotendeka. Wanaitumia mahakama ili kukomesha wale wote wanaopinga utawala wao.

Kisasili hiki cha mafuta kinadokeza kwamba jamii inakabiliwa na vitisho viwilli, uhuru wa kusema na ukweli. Wateule hawakuruhusiwa kusema ukweli. Ingawa mafuta ilikuwa ya milki yao, wateule wana kasoro. Kujigawa mafuta peke yao na kutawaliwa na uongo. Mchango huu unajitokeza tangu jadi na mpaka wa leo. Walio matajiri bado wanajigawia mali peke yao na hata hawasemi ukweli. Hii ni kwa sababu wanataka kujirundukia utajiri peke yao ilhali maskini wa Mungu akiendelea kula mwata.

Kisasili cha Mafuta kinatoa mchango kuonyesha jinsi kuna unafiki na uendelezaji wa uongo. Kuwa mteule sharti utimize mambo fulani kama kafara, miiko na mazingaombwe. Jambo ambalo halikuwa na maana bali ni vikwazo vya kuendelea kupata nafasi ya kujitajirisha.

Mchango wake pia unadhihirisha kuwa mafuta yalikuwa milki ya watu wachache. Waliokuwa na uwezo huo walikuwa matajiri waliotukuzwa na hata kutukuza ubinafsi uliochangia kukosa utu ilhali wenzao walidunishwa, kudhoofishwa na hata kukwama katika umaskini. Waliomiliki mafuta walikuwa na uwezo wa kukilalia kitanda. Kitengo hiki kiliwaruhusu kuwa wateule waliofanikiwa katika jamii. Yalionyesha mwanzo wa imani kuwa na mafuta kwa uzao au kwa bidii zao.

Kisasili cha mafuta kilichangia katika kuleta utabaka katika jamii. Kuna tabaka la matajiri na tabaka la maskini. Wateule ndio walioriithi nyenzo zote za uzalishaji mali. Ilibidi umma uwatumikie kutokana na vitisho walivyopewa. Wateule hali yao ya maisha ilikuwa bora. Waliishi katika mazingira masafi, nyumba nzuri, magari makubwa makubwa, chakula kizuri na mengineyo. Tabaka la wachochole hali yao ya kimaisha ilikuwa mbaya, kukula makombo kwa mapipa, kulala matopeni, hata hawakuruhusiwa kucheka na mahakama iliwekwa kwa ajili yao. Kwa ujumla mwandishi alionyesha tofauti kubwa kati ya tabaka hizi mbili.

Mwandishi katika kutoa mchango wa kisasili cha mafuta alitaka kuleta mwamko mpya wa kisiasa. Wateule ndio walioritihi nyenzo zote za mali. Ilibidi umma uwatumikie kutokana na vitisho walivyopewa. Ni baada ya kugundua hayo ndipo umma ukawa na mwamko wa kupata afueni katika mfumo wa kiuchumi ulionawiri, kwa hivyo, kisasili hiki kiliwazindua wachochole katika riwaya ya mafuta. Walitambua kuwa mateso waliyoyapata hayatokani na bahati mbaya bali ni kwa sababu ya uhusiano wa kijamii uliodunishwa na sheria za utawala wa wateule.

Kupitia kisasili cha mafuta mwandishi ametoa mchango wake kuonyesha kuwa ukweli unapodhihirika uwongo unajitenga. Tumeona fani moja ya maji katika riwaya hii ya mafuta. Maji ni ukweli unaufichua uwongo wa wateule. Maji haya yanaweza kukomboa, kutakasa na pia kuunajisi uteule. Yanawakilisha itikadi ya Imani ya wafanyikazi. Uchafu wote wa wateule uliondolewa ukweli ulipopatikana. Hapa hatuna budi kutumia methali, 'kilicho na mwanzo kina mwisho.' Ukweli ulipodhihirika uwongo ulitoweka. Mambo yao ya uwongo yalifika ukingoni.

Kisa cha mafuta kinatoa mchango kuwa hakuna jambo lisilo na mwisho. Lililo na mwanzo lina mwisho wake. Ujanja, unafiki, dhuluma, unyanyasaji na kadhalika, vyote hivi vimefikia mwisho. Madhulumu wanaonekana wakijikunyata kwa hofu na baadaye ghafla mlio wa 'maji' tu unasikika. Maji yanaashiria dhoruba ya mabadiliko, uhuru na udhabiti wa kweli. Mapinduzi haya yanalazimika wakati mhusika Mtue anaokolewa. Ukombozi unakuja kwa nguvu.

Mtunzi ametumia wahusika wateule sambamba na wachochole. Ametuchorea wahusika wanaoishi hali tofautitofauti kwa kutumia mbinu ya ukinzano ili kutoa mchango wake kuonyesha tofauti iliyopo baina ya matabaka haya mawili. Wahusika wateule wanaonekana makaazini mwao palipo na ufahari ikilinganishwa na ya wachochole wanaoishi katika vidimbwi vya matope. Inasisimua ari ya wasomaji ya kutaka kuangusha mfumo wa kisiasa wenye matabaka ya

uteule walio na mafuta, walio uwezo wa kukilalia kitanda na watu wenye nyuso zinazoonyesha kuridika na maisha. Alichangia kwamba kuwa mteule ni kuingia katika tabaka la matajiri viongozi. Uteule huo unawapelekea kuwa na nyuso zinazometameta kutokana na kuridhika kwao. Mafuta yanawakilisha ule uwezo wao wa kulimbikiza mali.

Mwandishi ametumia tamathali ya tashbihi katika kutoa mchango wake. Anasema mtu huyu anametameta kama jongoo. Jongoo ni mdudu ambaye ngozi yake hung’ara kiasi kwamba inametameta kutokana na wororo huo. Kuashiria kwa kawaida binadamu ambaye amepata lishe bora na anapata mahitaji muhimu ya maisha kama chakula, mavazi na ana pesa za kutosha, huwa pia na wororo wa ngozi. Baadhi ya wateule katika riwaya ya *Mafuta (1984)* wamesawiriwa kuwa na ngozi nyororo kutokana na uteule wao. Pia uvimbe wa tumbo lake unamithilishwa na mama aliyebeba mimba nne. Kubeza sura za viongozi walio na utambi kutokana na tabia ya uporaji. Wororo huu unaashiria kuridhika. Shibe yake imesababishwa na unyonyaji wa wanyonge. Macho makubwa kama ya bundi yanaashiria kutisha kwake na ishara ya bahati mbaya. Watu wengi wana imani kuwa ndege huyu anayeitwa bundi huashiria kifo, hivyo basi macho ya mteule huyu yanaashiria kifo kwa mhasiriwa ambaye ni Matope. Katika hali hii, mtunzi alitaka kutoa mchango wake katika sura ya mteule huyu kuchochea uzinduzi. Kwanza kuvimba kwake ni ishara ya unyonyaji, huwa radhi kumtia yeyote yule hatiani atakaye hutumiwa na kisirani cha kujaribu kumtoa mahakamani. Kupitia sura ya mteule huyu, Mkangi anatoa mchango hasa kwa tabaka la wachochole ili kuwatamanisha akidhamiria kuamsha akili zao kujiandaa katika uzinduzi uliopo mbele yao.

Mwandishi ametumia jazanda nyingi katika riwaya ili kuuficha ujumbe wake na kulazimisha ufafanuzi kwa wale wanaotafuta kuelewa. Mwandishi ametoa mchango akitumia fani ya mafuta. Anajaribu kuelezea mafuta kama kigzo cha kulalia kitanda. Mafuta yanajitokeza kama kalabaa

kwani ni kijengo kilichowaruhusu wateule kukilalia kitanda. Pengine wachochole hawakuelewa maana ya fani hii. Mtunzi amechangia kuwa yanawakilisha nguvu za kuweza kutawala wengi. Anataka kuchangia kuwa mafuta ya milki ya watu wachache. Mafuta ndiyo nguzo ya maisha kwa hivyo ni mbinu ya kufikia kilele cha uteule.

Kila mara katika riwaya hii ya mafuta, mtunzi ametaja fani ya mafuta kuwachangia wachochole waweze kuelewa hali yao na ni nini kimewafanya waishi katika hali duni isiyopendeza. Anataka waweze kuelewa sifa ya mafuta kuwa ya udanganyifu kwani ni vikwazo ambayo mtu anawekewa na wanaofikia kule ni wale walioshinda wengine kwa ujanja. Wanaopata mafuta hayo mbinu yao ni ya uongo na adui wao mkubwa ni ukweli.

Katika utangulizi wake, Mkangi anatoa tofauti ya utangulizi huu na hadithi yenyewe. Hadithi ya mafuta inaanza na mswada unaoachwa na Jali. Mkangi ametumia mbinu ya hadithi ndani ya hadithi kwa kutumia aina hii ya muundo. Kwa kufanya vile, mtunzi anadhihirisha umuhimu wa fasihi kwa jamii au dhima ya fasihi katika jamii. Kisa cha mafuta kimechangia kuwazindua wengi, watoto kwa wakubwa kama viongozi wa kesho. Katika mafuta vimetumia mbinu simulizi ili kubainisha na kurahisisha ujumbe wake. Kwamba kila mteule ni kipofu (wanajiita vipofu) lakini raia wana macho. Wanaona ukweli ilhali wateule wanajilazimisha kwani ni uongo.

### 4.2.2 Kisasili cha matope

Mwandishi ametumia tukio la mahakama kutoa mchango wake. Alidhamiria kuonyesha hali ya mahakama ambayo inatoa maamuzi yake kuegemea upande wa tabaka la wateule. Mahakama hii ilikuwa ya tabaka la chini ili kuwatesa na kuwaogofya wasije wakagundua siri ya wateule. Tabaka hili lilikuwa na itikadi ya maji ambayo baadaye inaleta ukombozi. Mahakama hii ilikuwa inakata kauli kwa wanyonge. Tabaka la mabwanyenye liliruhusiwa kucheka. Mtue kwa kucheka

alikatiwa kesi na mahakama anyongwe. Kucheka si kitu walikuwa wakichukulia hivi hivi. Kucheka kulikuwa ni kitendo cha nadra sana ikiwa fursa hiyo ilipewa wateule rasmi lakini si wanamatope. Kwa maskini kucheka ni kashfa na uasi.

Kawaida ya hawa wachochole ilikuwa kutupiana ngano kila baada ya maankuli ya jioni. Hadithi hizi zilikuwa za kusisimua sana kimawazo na kwa kilumbi pia. Lao lilikuwa kusikiliza, kuambiwa, kutazama na mwisho kuwa magudulia yakingojea kumiminiwa takataka zozote.

Tuki (2003), tope ni udongo wa majimaji unaonata. Matope kulingana na muktadha huu aliashiria uchafu na dhiki iliyowakumba wanamatope katika jamii yenye utabaka. Jina lake ni la kimajazi lililoangazia sifa za wazi na za kuonekana kwa mhusika anayeitwa matope.

Mkangi kupitia mhusika Matope alidhamiria kuchochea hisia za msomaji. Taswira ya mhusika Matope hasa akiwa amelala matopeni ni ya huzuni mno na ya kustaajabisha. Taswira hii pamoja na jinsi alionekana mahakamani hata na kula chakula cha mapipani kilichonuka ni cha kutisha na kuhurumisha. Hii ni taswira iliyowafungua macho na kutaka mapenduzi. Mapenduzi haya yalikuja ghafla kiasi kwamba hayasadikiki kwa urahisi. Hatuoni maandalizi yeyote lakini mwishowe yataunda jamii mpya ambayo Mkangi alidhamiria yenye usawa. Yameletwa na wanyonge kama njia ya kuleta ukombozi. Maudhui mbalimbali yametumiwa kuendeleza dhamira hii ya ujenzi wa jamii mpya.

Kisasili cha matope kilitoa mchango wake kuonyesha dhuluma kwa walio wachache katika jamii. Matope alikuwa amedhulumiwa mno na watesaji kiasi ya kwamba alipoletwa mahakamani, kutokana na tuhuma ya kuwaosha wateule kwa maji alitemewa mate, akachapwa na bakora, mashavu yalivimba na kubadilika rangi kutokana na makofi na kitendo cha dhuluma na kunyanyaswa.

Kupitia kisa cha wanamatope, mwandishi ametoa mchango wa kuamsha hisia za wasomaji au umma kulingana na vile hali ilikuwa. Hali nzima ya matope inampelekea msomaji kulengwalengwa na machozi. Inachora hali za kuchukiza. Waliohudhuria mahakama waliajabia hali mbaya ya matope, mwandishi anasema.

> Kuingia kwake kulileta mshtuko…
>
> Mara tu walipomkata macho (uk 39)
>
> Waliohudhuria mahakamani walipomwona hali ile ya kusikitisha, walishtuka (uk 45).

Katika kutoa hali kama hii, mwandishi ana lengo la kuwazindua wasomaji wa mafuta. Ili tuweze kupata mwamko mpya, unachochewa na hisia fulani ya kushangaza, kuhuzunika na kukera wengi. Hatuwezi kupata mabadiliko mpya hadi watu wachochewe na hali fulani. Wanamatope wamepata mwamko mpya.

Uchi wa matope ni taswira inayomzindua msomaji. Ilionyesha tofauti ya tabaka zilizopo katika jamii. Uchi ni ishara ya usafi wa kiroho aliokuwa nao matope licha ya kwamba anateswa. Dubwana ni mmoja wa watesaji wa matope aliyemkagua kama vile mnunuzi wa kipande cha nguru alivyofanya. Mwandishi anatumia tashbihi kusawiri jinsi Dubwana alivyomuona Matope kama kiumbe asiyekuwa na thamani yeyote. Mwandishi alisema macho ya Dubwana yalimpekua ingawaje kiwiliwili cha Matope kilikuwa kinakaa kama zimwi (uk 43). Wahusika Matope na Dubwana walitoa mchango wa maudhui ya ukinzano. Tofauti yao ililenga uzinduzi wa mkinzano wa kitabaka kati ya wateule na watawaliwa. Ilidhihirisha dhima ya mahakama kama nguzo ya utawala katika mfumo wa kibepari. Lengo la Mkangi ni kuwazindua wasomaji wa *Mafuta*.

Kisa cha matope kinatoa mchango wake kudhihirisha kuridhika na kile ambacho uko nacho. Matope hataki kuhurumiwa. Anahiari kulala matopeni kuliko pahala pakavu. Maanake ni kwamba yeye anaridhika na pale alipo. Hataki kusumbuliwa kwani amelala katika usingizi mnono. Mtue alikumbana na mtu aliyelala matopeni. Anapojaribu kumwamsha anakasirika sana. Haoni sababu ya kumwamsha. Kwake yeye ni sawa amezoea kulala matopeni. Ameyakubali maisha hayo wala hamna haja ya kujisumbua kutafuta pazuri.

Mchango wa kisa cha wanamatope ulitolewa wazi kupitia kwa matope kutufahamisha kwamba maisha ya tabaka la matopeni ni maisha magumu, ya kuhurumisha, kudhulumiwa na kukosa mahitaji ya kimsingi. Kusudi lake Mkangi ni kutaka suluhisho kwa tabaka hili la wachochole. Wanahitaji ukombozi kwa haraka.

Mhusika Msati anawapigia wenzake mfano kwamba ukimuua nyuki mmoja (matope) uwe ukifahamu kuwa kwenye mzinga kuna wengi. Usione umewamaliza kwa kumuua mmoja. Mfano huu unatoa mchango kuwa hakuna aliyezaliwa peke yake, anao wenzake na wanahitaji kuungana ili waushambulie uongo. Umoja, kwa mfano wa nyuki unahitajika ili ukombozi upatikane. Umoja ni nguvu na kidole kimoja hakimuui chawa. Tabaka la wanyonge linadhihirisha walio wengi.

Mwandishi ametumia taswira ya maji katika kisa hiki cha matope kutoa mchango wake. Taswira ya maji hapa inaonyesha kuwa maji ni ukombozi na huondoa uchafu. Chochote kilicho na uhai lazima kitumie maji. Itikadi ya maji ina mashiko na haishindiki. Maisha hayawezi kuendelea bila maji. Maji ni lazima, husafisha, hung’arisha na hurahisisha maisha katika jamii.

Mkangi katika kutoa mchango wake katika kisa hiki, anadhihirisha uhalisia wa kijamaa. Mapenduzi yanaletwa na wanyonge. Hawa ndio tabaka inayoteswa katika jamii nyingi za

kiafrika. Baada ya muda mrefu wa mateso, wanaamua kuleta mabadiliko. Mabadiliko ambayo hayana maandalizi, yanakuja kama upepo uvumapo baharini bali baada ya dhiki kuna faraja. Mwisho, jamii hii ya wachochole ina sababu ya kufurahi katika jamii mpya.

Mwandishi ametumia tashbihi kutoa mchango wake. Dubwana mmoja wa watesaji wa Matope anamkagua kama vile mnunuzi wa kipande cha nguru anavyofanya. Mwandishi anatumia tashbihi kusawiri jinsi Dubwana alivyomuona Matope kama kiumbe asiyekuwa na thamani yeyote. Mwandishi anasema macho ya Dubwana yalimpekua ingawaje kiwiliwili cha Matope kilikuwa kinakaa kama cha zimwi (uk 43). Hapa mtunzi analenga wahusika Matope na Dubwana kuzua ukinzano. Tofauti yao inatoa mchango kulenga uzinduzi wa mikinzano ya watawaliwa. Inadhihirisha dhima ya mahakama kama nguzo la utawala.katika mfumo wa kibepari. Lengo la Mkangi ni kuwazindua wasomaji wa *Mafuta (1984).*

Kitanda ni kifaa kinachotumiwa kulala. Mwandishi ametoa mchango kwa kutumia taswira ya kitanda. Imetumiwa katika riwaya ya *Mafuta (1984)* kijazanda ili kuwapa wasomaji mwamko mpya wa kuwafahamisha baadhi ya viongozi ambao hutumia hila na ujanja kujiweka mamlakani. Anataka kuwaonyesha kwamba kitanda kinawakilisha mbinu za ujanja zilizotumiwa na wakandamizaji ili kujidumisha katika ngazi za utawala. kuwa uteule ni utabaka huko ndiko kukilalia kitanda. Mkangi anachangia ili kutoboa siri ya kitanda kilichokuwa kitumiwe ili kuwapumbaza na kuwanyanyasa raia. Hili ndilo Mkangi alilenga kuwafafanulia wasomaji wake. Raia walinyimwa haki zao na kukandamizwa kupitia uongo huo.

### 4.2.3 Kisasili cha mama Fofi

Kupitia kwa kisa cha mama Fofi, mwandishi anadhamiria kufahamisha maisha ya tabaka la matopeni. Kwa mfano, kuwania mabaki ya chakula ambacho mbwa, kuku na paka walikikataa. Waling'ang'ania makombo hayo wakibishana na panya na kombamwiko. Anadhamiria

kudhihirisha hali ya unyonge na kukata tamaa kwa wanamatopeni. Kula chakula kilichotiwa sumu ili ajifilie mbali maana hawana maana yoyote.

Mkangi bado nia yake ni ujenzi wa jamii mpya iliyo na usawa. Wanyonge wamechoka na maisha haya yasiyo na raha wala matumaini. Wameanza kuona ukweli mahali ambapo umefichwa. Mwishowe wamebainisha kuwa maji ndio uhai na hayo tu ndiyo yataleta ukombozi. Unyama utatoweka, ukweli na usawa utatawala.

Kisa cha mama Fofi kinatoa mchango wake katika kuelezea maudhui ya ufukara. Bwana ya mama Fofi alizaliwa katika mazingira ya ufukara. Lakini inaonekana kuwa kuzaliwa katika ufukara haimaanishi kufa maskini. Kwa juhudi yake alitoka mazingira haya na kuenda kuurithi ufalme. Hatima ya riwaya hii inaonyesha ushindi dhidi ya dhuluma.

Mama Fofi alilia haki itendeke ingawa alikuwa amewanyonya wafanyikazi waliomsaidia katika kazi yake. Mwishowe faida ilipopatikana ilikuwa mali yake binafsi. Kwa hivyo, kisasili cha mama Fofi kilitoa mchango kuwa haki kwa kula jasho la wengine ndilo mwandishi anapinga. Mtu akule jasho lake kwa juhudi yake mwenyewe bali si kwa wengine.

Mwandishi pia kupitia kisasili hiki cha mama Fofi alijaribu kutoa mchango kudhihirisha harusi nne katika maisha ya mwanadamu. Kuzaliwa, kutahiri, kuoa na kufa. Katika harusi hizi zote huwa kuna kusherekea na kufurahi isipokuwa harusi ya mwisho ambayo huwa ya sherehe na majonzi. Katika sherehe hizi zote, watu huja pamoja ili kusaidiana katika njia mbalimbali ili kuzifanikisha.

Tunaweza kuelezea mchango wa kisasili hiki kwa kutumia methali ‘ukweli ukidhihirika uongo hujitenga.’ Hii uwongo ya maji, mafuta na kitanda ilikuwa imefika kikomo. Mama Fofi hakupata

lolote kutoka kwa mahakama na badala yake kulitokea mshindo “maji tu! Maji tu!” maji yameleta ukombozi na furaha kwa tabaka la wachochole

## 4.3 Hitimisho

Uwezo wa kuingiliana kimatini katika visasili umejitoeza katika sehemu hii kupitia matukio mbalimbali. Katika kutoa mchango wa visasili, kwa vile visasili vilisheheni sifa halisi za kijazanda, mafumbo na semi zilizotokana na upangaji stadi wa lugha katika uandishi. Mathalan, michango kemkem ilielezewa kupitia usambamba wa visasili katika riwaya zote mbili.

Visasili huweza kuibua suala la kutoa mchango kwa kuchochea hisia za wasomaji pamoja na familia lengwa ili kupata msukumo wake unaostahili kwa kuzingatia kauli za waathiriwa hasa jamii ya umaskini. Kando na kuwapa hekima na busara katika mchango wake, anaazimia kuleta mabadiliko katika jamii. Pia, anaazimia kuleta ukombozi. Mchango huu unawafungua macho polepole hadi kufika kiwango cha kuona umaana wa jamii ulio na usawa. Mwishowe wao wenyewe watatafuta ukombozi kwa njia ya ushirikiano.

Visasili vimetumiwa kwa namna nyingi. Mwandishi amevitumia kutoa mchango wake kwa kuelezea asili ya tabia, chanzo cha matukio fulani, chanzo cha taabu za wanajamii, kuwatia moyo, kuchochea fikra na kufundisha jamii maadili mema.

## SURA YA TANO; HITIMISHO NA MATOKEO YA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Sura hii itahitimisha kazi yote kwa ujumla. Inatoa muhtasari wa kazi iliyofanywa katika sura zote. Muhtasari wa kazi umepitiwa kwa kuelezea shabaha kuu ya utafiti, upeo wa utafiti na yaliyomo katika kila sura. Matokeo ya utafiti yamejadiliwa kwa kina kwa kuelezea jinsi utafiti huu ulivyofanikiwa katika kuyafikia malengo yake. Mapendekezo pia yametolewa katika kuhitimisha kazi hii.

### 5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulichunguza mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi kwa kuegemea riwaya ya *mafuta (1984)* na *walenisi (1995)*. Utafiti ulizingatia kipengele cha visasili kwa sababu ni sehemu ambayo haijatafitiwa ipasavyo hasa kwa kurejelea vitabu husika. Visasili ni visa ambavyo vinaelezea kuhusu mianzo ya masuala fulani katika jamii kwa kuegemea historia ya wahusika. Utafiti ulijikita maktabani kusoma vitabu vinavyorejelewa na sehemu inayohusu visasili.

Utafiti huu uliongozwa na malengo ya kubainisha jinsi visasili vilivyotumika katika riwaya za *mafuta (1984)* na *walenisi (1995)*. Aidha, utafiti ulinuia kutoa mchango unaotolewa na visasili katika usawiri wa dhamira na maudhui katika riwaya husika. Mwisho, utafiti ulikusudia kutafiti mchango wa visasili katika vitabu hivyo. Ulilenga usomaji wa vitabu hivi kwa sababu viligusa matatizo yanayokumba jamii na yafaa kushughulikiwa.

Nadharia ya mwingilianomatini ulitoa mwongozo kamili katika vipengele vya visasili. Nadharia hii hujihusisha na ule uwepo wa sifa mbalimbali katika fasihi. Kulidhihirika kuwa kazi ya

visasili huwa na sifa za tanzu nyingine ndani yake katika kupitisha ujumbe. Kisha matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kunukuu mahali ambapo visasili vilitumika.

Tulichunguza jamii ya kisasa vile huchukulia visasili. Wanaangazia visasili kama jambo la kihistoria na wakati. Visasili vimeenezwa kupitia filamu. Hii ni teknolojia ya kisasa inayoelezea malengo asilia ya jamii kupitia visasili. Filamu nyingi zilizoendelea hutegemea visasili vya jadi. Tulibainisha majukumu muhimu ya visasili katika jamii husika. Visasili katika uamilifu wake huleta burudani, huelimisha, huleta ushirikiano, huadhibu na kurekebisha jamii, hutumika kupokezana kizazi hadi kingine katika hali ya kuhifadhi utamaduni wao.

Tuliongozwa na malengo ya kubainisha ikiwa visasili vilitumika katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*. Kulibainika kuwa visasili vilitumika katika vitabu hivi kupitia kisa cha moto, kisa cha Mchawi na kisa cha mabavu. Visasili hivyo vilitumika kutoa maudhui mbalimbali katika *Walenisi.* Maudhui hayo yalitimiza malengo ya mwandishi aliyonuia. Katika *Mafuta* kulibainika visasili vya mafuta, matope pamoja na kisasili cha mama Fofi. Vyote vilitoa dhamira pamoja na maudhui ya mwandishi na matarajio yake ya kuunda jamii mpya isiyo na ubaguzi.

Utafiti pia ulibainisha mchango wa visasili katika riwaya ya *Walenisi* na *Mafuta.* Mwandishi alitoa mchango wake kuwachochea wasomaji na kuwafungua macho na kuangazia taabu ambazo walizipitia na jinsi walivyobaguliwa na tabaka la mabwenyenye. Kisha baadaye waweze kuleta mabadiliko. Mabadiliko haya ndiyo yataunda jamii mpya iliyo na usawa kwa kila mtu. Jamii iliyofurahiwa na isiyo na matatizo. Jamii itakayomaliza unyanyasaji na dhuluma. Utafiti ulielezea Wachuna ni kina nani. Vilibainisha kwamba Wachuna ni imani fulani iliyoanzishwa na wenye kuwanyima haki zao za kimsingi. Chochote walichoonyesha mkono wa kutoa kilikuwa

cha malipo. Walinyimwa haki za kimsingi kama chakula bora, nyumba nzuri afya bora na nguo safi.

Utafiti huu uliongozwa na malengo ya kubainisha ikiwa visasili vilitumika katika riwaya za *Walenisi* na *Mafuta*. Aidha utafiti ulinuia kubainisha mchango unaotolewa na visasili katika usawiri wa dhamira na maudhui katika riwaya husika. Na mwisho ulikusudia kutafiti mchango wa visasili katika vitabu hivyo. Usomaji wa vitabu hivi pia ulilengwa kwa sababu utafiti uligusia matatizo yaliyokumba jamii na yafaa kushughulikiwa.

Tabaka la wachochole unakabiliana na jabali la ujinga ambacho chanzo chake hakidhihiriki vilivyo. Kuna ujinga wa asilia ambao kila mtu hupitia hasa akiwa mtoto. Kunaonekana kwamba asili hii ya ujinga ni mtu kufanya mambo ambayo si ya kawaida kama vile kujitaabikia na kuwategemea watu wengine.

Katika hali ya jamii, kuna ujinga unaomfanya mwerevu kuonekana mjinga. Maskini walionekana wakifumbwa na itikadi ya ujinga ambayo ilifanya maisha yao kuwa duni. Ujinga huo uliwaletea njaa, kulala matopeni, kula chakula cha mapipani, kudhulumiwa pamoja na kunyanyaswa.

Mwandishi Mkangi anaonya kuwa hatuwezi kufaulu ikiwa tutaendelea kuiga mambo ya kigeni na hata kutumia lugha za kigeni, katu hatutajifahamu hivyo. Ubaguzi kwa misingi kama dini, kabila, jinsia na rangi utatuangamiza. Hataki kamwe kusikia kuwa tunayazoea matatizo. Himizo lake ni kwamba tufanye jambo lolote litakalosaidia kuyamaliza matatizo haya.

Wachuna ‘wamebahatika’ ni swala ambalo linamkera mwandishi kwani mambo hayatokei kibahati tu bali hupangwa na kushughulikiwa. Ngano ya wachuna iliingia tu polepole na mwisho ikatanda kotekote na kuanza kuwanyanyasa watu. Vilevile kuondoka kwao kutakuwa kisadfa tu

kama vile visasili vinatokea kisadfa. Moto ulitokea kisadfa na mabadiliko haya pia yalikuja ghafla.

Tabaka la maskini linafananishwa na popo. Ni vipofu. Wao ni vipofu kwa kuwa hawawezi kuona dhuluma kati yao. Hawawezi kunusa uvundo wa magonjwa ya kitabaka kati yao wala hawasikii njaa na umaskini. Kati yao wanaishi kichwa chini miguu juu, lakini kabla waanguke, mwandishi Mkangi ameshikilia usukani kuwaondoa upofu huu ambao unawatawala tabaka la chini. Anahitaji jamii mpya isiyo na upofu. Jamii yenye macho, jamii yenye shibe, jamii inayonusia uvundo wa ugonjwa wa utabaka.

## 5.2 Matokeo

Imedhihirika kuwa visasili vinapotumika huweza kuleta muuwala katika matini ya riwaya na kufanya kazi ieleweke kwa urahisi mno. Aidha, visasili vinapotumika katika kuendeleza riwaya huchangia pakubwa katika kueleweka kwa ujumbe. Hivyo, tuliweza kuchunguza jinsi visasili vilivyobainika katika riwaya na sababu ya mtunzi kuvitumia visasili hivyo.

Utumizi wa visasili huwafanya wasomaji kuwa na hamu zaidi kuliko kuwapa tu kile wanachotarajia katika riwaya teule. Hususan visasili husaidia kuchochea hisia za wanajamii, kuwatia moyo, kuwaleta pamoja na kutambua hali yao ya maisha yasiyopendeza na mwisho kuwa na hamu ya kuleta mabadiliko. Hii inaashiria kwamba utumizi wa mtindo mmoja huchosha, hivyo visasili katika kule kuingilianamatini kama vile jazanda, semi, mafumbo majazi na mengine hutumiwa kuleta msukumo mpya katika riwaya ya *mafuta (1984)* na *walenisi (1995)*.

Matumizi ya visasili huwapa wasomaji msisimko kwa mfano visasili kama kipengele kilichojaa burudani unapofululiza masimulizi ya visa mbalimbali katika riwaya teule kama vile kisa cha Moto, cha Mchawi na cha Mabavu katika *Walenisi (1995)*.

Kutokana na usomaji wa riwaya za *mafuta (1984)* na *walenisi (1995)*, utafiti ulibainisha matumizi ya visasili. Visasili hivyo vilielezea asili ya uchuna kupitia kisasili cha Mchawi ambaye alianzisha tiba ya walioumwa na nyoka. Mwandishi alitumia kisasili cha Mabavu aliyegundua hoja ya kulinda wanajamii hasa wanawake. Pia kisasili cha moto kilielezea kuhusu asili ya moto. Aidha kuna kisa kuhusu asili yaa wateule na masikini kupitia Matopeni na Sifa.

Kupitia visasili, kulibainika kwamba haya ni matukio ya kihistoria yaliyotokea kisadfa. Lakini yaliweka msingi dhabiti katika historia ya mwanadamu. Matukio haya yalifanya maisha katika jamii kuwa bora zaidi. Kwa mfano kitivo cha afya ambacho husaidia na kupunguza vifo, msingi wake ulikuwa katika ugunduzi wa dawa ya kutibu ndipo utafiti wa madawa ukaendelea hadi sasa.

Utafiti ulibainisha kuwa visasili vilitoa mchango katika kusawiri maudhui na dhamira. Baadhi ya maudhui ni utabaka na ubinafsi kati ya matajiri na masikini, uvumbuzi na maendeleo, unyanyasaji na dhuluma, ufisadi na mengine mengi. Dhamira ya riwaya hizi mbili ni ubainishaji wa ujenzi wa jamii mpya. Kupitia kwa visasili, Mkangi ametuonyesha namna jamii yenye utu na usawa inavyoweza kuumbwa. Kadhalika kupitia visasili, mtunzi anatuonyesha umuhimu wa ukombozi kama njia ya kujenga jamii mpya. Mapenduzi hayo yalileta ufanisi mkubwa.

Pia utafiti ulionyesha kuwa visasili vinachangia pakubwa katika kufanikisha upasho wa ujumbe wa mtunzi. Kulibainika kuwa visasili hutoa mchango mkubwa katika kuelezea dhamira yake bila kukata tamaa.

Kupitia kwa visasili, kulibainika kuwa historia imechukua nafasi kubwa hasa kwa misingi ya nyenzo ya kuwakilisha masuala ya kisiasa, kiuchumi na utamaduni wa jamii hata mpaka leo.

Kwa hivyo, haliwi jambo geni kuona utawala wa kimabavu kwa sababu ilikuwa hivyo tangu jadi ama katika historia ya mwanadamu.

Kupitia visasili, mwandishi alitoa mchango wake kuelezea chanzo cha taabu katika jamii. Aliwapa moyo kupigania ukombozi. Aliwahimiza na kuchochea fikira za jamii kushirikiana kupigania haki yao. Aliwapa mwamko mpya. Kwa hivyo, kwa jumla kulibainika kuwa visasili vilitumika katika riwaya ya *mafuta (1984)* na *walenisi (1995)*. Shabaha ya kwanza ya utafiti ulikuwa kubainisha matumizi ya visasili katika riwaya husika. Alitufahamisha jinsi jamii zetu zilivyo pungufu na mbovu na jinsi utu wetu ulivyofifia. Alikuwa na lengo la kudhihirisha kwamba jamii zetu duni zinaweza kubadilishwa na kuboreshwa ili kufikia viwango vya juu sana.

## 5.3 Mapendekezo

Kutokana na utafiti kuhusu mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi kwa mfano wa visasili, utafiti ulipendekeza kuwa utafiti ufanywe zaidi kuhusu mbinu za kisanaa zilizotumiwa katika visasili na mchango wake.

Sehemu nyingine ambayo inaweza kushughulikiwa na utafiti wa baadaye ni maadhiriano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi kwa muktadha wa riwaya hizi mbili kwa kutazama ni kwa nini kumetokea ukiukaji wa mambo kutoka fasihi simulizi hadi fasihi andishi.

Watafiti wengine wanaotaka kutafiti, wanaweza kuchunguza matumizi ya lugha na fani katika kutoa msukumo wa visasili au maudhui, kama ilivyo kawaida lugha ni chombo muhimu kwa mwanadamu.

## 5.4 Hitimisho

Sura hii ya utafiti ilikuwa inadhibitisha malengo ya utafiti. Utafiti ulikuwa na haja ya kujua ikiwa visasili vilitumika katika riwaya hizi mbili. Kulibainika kwamba visasili vilitumika katika riwaya

ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Utafiti ulitambua visasili katika riwaya ya *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*. Katika *Walenisi (1995)* kuna kisasili kwa jina moto, mchawi na Mabavu. Katika *Mafuta (1984)*, kuna kisasili cha mafuta, matope na mama Sifa.

Pili, utafiti ulilenga kudhihirisha maudhui na dhamira. Kupitia visasili tulitambua maudhui ya utabaka kati ya maskini na tajiri, uvumbuzi na maendeleo, dhuluma, unyanyasaji na kadhalika. Dhamira na maudhui ni mambo yanayoingiliana. Hata hivyo, dhamira ya Mkangi likuwa ubainikaji wa ujenzi wa jamii mpya kupitia njia ya ukombozi.

Mwisho, kulibainika kuwa visasili vilichangia kwa namna nyingi. Vilieleza asili ya tabia fulani, chanzo cha taabu za wanajamii, anaonyesha hali ya kutokufa moyo wakati wa kupigania ukombozi, kuchochea fikira za jamii ili kuona haja ya kushirikiana kubomoa mipaka isiyofaa kupitia mapenduzi na kufundisha maadili kama vile utiifu, uvumilivu, huruma na kujikakamua kwa ajili ya jamii.

## MAREJELEO


Barthes, R. (1972). *'Mythologies':* Hill and Wang Publishers

Campbell, J. (1988). "*The Power of Myth*". New York: double-day

Dundes, A. (1997). "*Binary opposition in myth*: The Propp/Levi-Strauss Debate in Retrospect". Western folklore.

Dundes, A. (1984). *Introduction. Sacred narrative: Readings in the Theory of Myth*: University of Carlifornia Press.

Eliade, M. (1963). *Myth and Reality.* Trans. Willard R. Trask. New York: harper & Row.

Eliade, M. (1967). *Myths, Dreams and Mysteries*. Trans. Phillip Mairet. New York: Harper & Row.

Encyclopaedia Britannica. (2009). "Myth". Encyclopaedia Britannica Online, 21 March 2009

"Euhemerism". The Concise Oxford Dictionary of World Religions. Ed. John Bowker. Oxford University Press, 2000. Oxford Reference Online. Oxford University Press. UC-Berkeley Library. 20 march 2009.

Frazer, J. (1922). *The Golden Bough*. New York: Macmillan.

Graves, R. (1955). *Greek Myths.* Penguin Books Ltd.

Graves, R. (1969). *Larousse Encyclopaedia of Mythology.* Barnes and Noble Incorporated.

Honko, L. (1984). "*The Problem of Defining Myth*". Sacred Narrative: Readings in the Theory of Myth. Berkeley: University of Carlifornia Press.

Ions, K. (1987). *The Worlds Mythology in Colour*. Chartwell Books Incorporated.

Kahara, I. (2011). *Tamthilia Kama Utendi, Uchanganuzi Linganishi wa Tamthilia za Kinjekitile na Mzalendo Kimathi*: Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.

King'ei, K. (2000). *Miale ya Uzalendo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

King'ei, K. na Kisovi, C. (2005), *Msingi wa Fasihi Simulizi*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kristeva, J. (1980). Desire in language asemeotic approach to literature and art: New York, Colombia University.

Longhorn (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*, Nairobi: Longhorn Publishers

Matteru, M. (1987). *"Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi katika Mulika 19*." Dar es Salaam Tuki.

Masinde, E. (1992). Mashairi huru: Uchambuzi wa dhamira na mtindo. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mbughuni, P. (1978). *From Oral to Written*; *The Politicization of Kiswahili Literature*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Indiana.

Mkangi, K. (1975). *Ukiwa*. Nairobi: East Africa Educational Publisher Limited

Mkangi, K. (1984). *Mafuta*. Nairobi: East Africa Educational Publisher Limited

Mkangi, K. (1995). *Walenisi*. Nairobi: East Africa Educational Publisher Limited

M'ngaruthi, N. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: JKF.

Mohamed, S. (1960). *Mzimu wa Watu wa Kale*: East African Publishers.

Mohamed, S. (1976). *Mwana wa Yungi Hulewa*: East African Publishers.

Mohamed, S. (1989). *Asali Chungu.* Nairobi: East Africa Educational Publisher Limited

Mohamed, S. (1990). *Tata za Asumini.* Nairobi; Longhorn Publishers

Mohamed, S. (2001). *Babu Alipofufuka.* Nairobi; Jomo Kenyatta Foundations.

Mohamed, S. (2006) *Dunia Yao.* Nairobi; Longhorn Publishers.

Mohamed, S. *(*2010*) Nyuso za Mwanamke*. Nairobi*;* Oxford University Press.

Mugullu, R. (1999). *Mtaala wa Isimu*, Longhorn Publishers.

Muller, M. (1866). *Lectures on the Science of Language, Longmans, Green*

Mulokozi, M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi katika Mulika 21.* Dar es Salaam: Tuki.

Musee, M. (2007). Matumizi ya Majazi Kama Mkakati wa Kuepuka Upigaji Marufuku Katika Riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Musembi, N. (2008). Matumizi ya Taswira na Ukinzani Kama Kichocheo cha Zinduko Katika Riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Ngure, A (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule ya Sekondari*, Nairobi: Oxford University press.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*: Jomo Kenyatta Foundation.

Okpewho, I. (1983). *Myth Africa*. London: Cambridge University Press.

Olrik, A. (1999) "*Epic Laws of Folk Narrative*" International Forkloristics, Dundes, A (Ed) Boston: Rowman and Littlefield publishers.

Omari, .K. na Mvungi (1981). *Urithi wa utamaduni wetu Dar-es-salaam*: Tanzania publishing house.

Omotimbia .C. (2015). Usimulizi katika fasihi. Uchanganuzi wa riwaya ya *Walenisi* (1985), *Babu Alipofufuka* (2001) na *Adili na Nduguze*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa)

Plekhanov, .G. (1957)*Art and social life* Moscow; Progress Publishers.

Robert, S. (1991). *Kusadikika*: Mkuki na Nyota Publications.

Robert, S. (2008). *Kufikirika*: Mkuki na Nyota Publications.

Saussure, R. (1911). *Course in General Linguistics*: Open Court Publishers

Saussure, R. (1982*). Course in general linguistics* New York: philosophical library.

Sengo, S. (1973). *Hisi Zetu*: Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili.

Stevenson, T. (1969). *History of Myths*: Seabury Publishers.

Thiong'o, N. (1982). *Shetani Msalabani*. East African Educational Publishers.

Tuki, (2006). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Fotoform ltd, Nairobi.

Tuki, (2012). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*: Oxford university press.

Tylor, E. (1871). *Primitive Culture*: *Researches Into the Development of Mythology, Philosophy, Religion, Art and Custom.* Murray publishers, London.

Vonyoli, .A. (2004). *Hadithi kama chombo cha maudhui katika fasihi; uchanganuzi wa riwaya za Mkangi, Mafuta (1984) na Walenisi (1995)*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Hakijachapishwa)

Wallek, R. na Warren, A. (1956). *Theory of Literature*: New York Harcout Brace and World publishers.

Wamitila, K. (1999) *What's in a name: towards literary onomastics in Kiswahili literature*.

Wamitila, K. (1999). *Unlocking Katama Mkangi's Walenisi*: Journal of The Institute of Kiswahili Research Dar-es Salaam, Tanzania.

Wamitila, K. (2003). *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi: East Africa Educational Publisher Limited.

Wamitila, K. (2002). *Bin-Adamu*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K. (2002) *Uhakiki wa fasihi msingi na vipengele vyake* Nairobi, phoenix publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istillahi na Nadharia*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.